ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria

		na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa

		na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini

30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi – Tarehe 20 Februari, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii):
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Hati ya Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 38

Amana Zinazosimamiwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kisheria inasimamia na kuzitunza mali zote zilizo chini ya kamisheni hiyo, jambo ambalo linasaidia kupatikana kwa haki kama ilivyotarajiwa na kwasababu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mashamba ya aina tofauti kama vile mashamba ya minazi, mikarafuu n.k.

(a) Je, kwa sasa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mashamba mangapi ambayo yalitolewa wakfu wa Misikiti.

(b) Je, shamba la Baziadi iliyopo Bwagamoyo Mtambwe ilitolewa Wakfu kwa ajili ya kushughulikia misikiti mingapi.

(c) Je, kuna utaratibu gani uliopangwa wa kupanda miti mengine mashamba yote ya Wakfu ambayo kwa sasa inaonekana kwamba miti ya asili iliyokuwemo kwa wakati huo imeshakuwa mikongwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake lenye Nam. 38 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa sasa Kamisheni ya Wakfu ina mashamba manne (4) ambayo yalitolewa wakfu wa misikiti na yote hayo yako Pemba.

(b) Mhe. Spika, Shamba la Baziadi iliyopo Bwagamoyo Mtambwe ilitolewa wakfu kwa ajili ya kushughulikia misikiti mitatu (3) nayo ni:-

1. Mhe. Spika, Msikiti wa Ijumaa uliopo Miembeni Chake Chake na unapata 2/5 ya mapato.

2. Msikiti wa Ijumaa uliopo Chachani Chake chake na unapata 1/5 ya mapato.

3. Msikiti wa Ijumaa uliopo Wete na unapata 1/5 ya mapato hayo.

(c) Mhe. Spika, upandaji wa miti mengine hufanyika kwa vipindi kwa mujibu wa mapendekezo ya wakaguzi na inapojiri haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwakuwa Mhe. Naibu Waziri umesema mashamba haya yapo 4 na umeliulizia moja tu shamba la Baziadi. Je, hayo mashamba mengine yaliyobaki yapo katika maeneo gani wilaya na shehia gani.

b) Kwakuwa shamba la Baziadi ni kubwa na kuna sehemu nyingi zilizokuwa ziko wazi hazijapandwa. Je, ni lini Kamisheni ya Wakfu na Maliamana itachukuwa juhudi za makusudi ya kulipanda miti kujaza sehemu zote zilizowazi katika shamba hili, ili kurudisha uhalisia wake kama pale mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Ni kweli nimesema kwamba yapo mashamba manne na mashamba hayo yote yapo Pemba, lakini maeneo halisi kwa sasa hivi sitoweza kumwambia lakini nimwambie tu kwamba nitakujibu kwa njia ya maandishi.

b) Kwamba ni lini upandaji miti tutaufanya katika shamba la Baziadi ambalo liko Bwagamoyo kule Mtambwe.

Mhe. Spika, taarifa ni kwamba shamba hili kila baada ya muda fulani huwa tunafanya utaratibu huwo katika hayo mashamba ambayo huwa tunapanda miti, basi na hilo shamba ambalo liko Baziadi la Bwagamoyo huko Mtambwe basi tumeshapanda miti mbali mbali. Kwahivyo, tutaendelea kupanda miti kadri vile ambavyo wale wakaguzi wetu watakavyotuelekeza lakini tayari shamba hilo tumeshapanda miti.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwakuwa katika majibu yake ya mgawanyo wa mapato wa shamba lile la Baziadi napenda nimnukuu amesema kwamba 2/5 inakwenda kwenye Msikiti ulioko Miembeni Chake chake, 1/5 Msikiti wa Chachani Chake chake na 1/5 Wete ukizisam kwa pamoja unakuta ni 4/5 ambayo imebakiya 1/5. Sasa je hii 1/5 inakwenda wapi ahsante

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Hiyo idadi au hicho kiwango ambacho ulichokitaja kilichobakia hicho kinakwenda katika uwendeshaji wa shamba kama tujuavyo kwamba, mashamba yanahitaji kushughulikiwa vyenginevyo mashamba hayo yangeweza kuwa na msitu mkubwa hata hayo mazao yasiweze kuenea zaidi. Kwahivyo, hichi kiwango ambacho kilichobakia huwa kinaendesha usafi na mambo mengine yanayohusiana na shamba ili kulirutubisha zaidi.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwakuwa, msimu huu uliopita wa uchumaji wa karafuu kulikuwa na utata uliojitokeza baina ya ukodishaji wa mashamba wa Wizara ya Kilimo na watu wa Wakfu na inasemekana kwamba Wizara ya Kilimo imeyakodisha mashamba ya Wakfu bila ya ushauri mzuri baina ya wao na watu wa Wakfu. Je, kwanza swali hili ni kweli, na ikiwa ni kweli utata huo uliingia kwa njia gani

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, taarifa hiyo sisi kama Wizara bado hatujaipata, kwa hivyo nikwambie tu bado taarifa hiyo bado, lakini kama lipo basi tungeweza kulishughulikia lakini hadi sasa hivi taarifa hiyo bado hatujaipata afisini kwetu.

Nam. 59

Tatizo La Mawasiliano Katika Mtandao Wa Zantel

Mhe. Said Omar Said - Aliuliza:

Ahsante Mhe. Spika, kwanza nataka nifanye marekebisho magodo tu kama ifuatavyo:-
Katika vijiji vya Sizini, Kijichame, Mitungujani, na Ziwatuwe baada ya marekebisho hayo naomba swali langu Nam. 59 lijibiwe kumejitokeza tatizo la mawasiliano kupitia mtandao wa *Zantel* kwa kipindi cha miezi minne (4) sasa.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuibuka kwa tatizo hilo ambalo huko nyuma halikuwepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa nafasi hii kumjibu Mhe. Said Omar Said suala lake Nam. 59 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, *Zantel* ilikuwa na jukumu kuanzia mwanzo wa mwaka 2017 la kuimarisha huduma za mawasiliano kwa visiwa vya Unguja na Pemba na hivyo kuzindua mradi wa *"Modernization"* ambao ulihusisha kubadilisha vifaa vikongwe vya minara yote na kufunga vifaa vipya vya aina ya *"Ericsson".*

Moja katika changamoto kubwa ya mradi huu ni kuifanya kazi hio bila ya kuzima mawasiliano, na hilo limechangia katika baadhi ya sehemu kujitokeza matatizo madogo madogo ambayo *ZANTEL* huwa inayashughulikia na kuyatatua kwa haraka.

ZANTEL inakubali kuwepo kwa tatizo la mawasiliano katika sehemu hizo zilizotajwa na nyenginezo ambazo chanzo chake ni hicho kilichotajwa hapo juu cha *"Modernizaton".*

ZANTEL imekuwa ikipeleka mafundi kwa ajili ya kutatua matatizo hayo na hivi tunavyojibu suali hili tayari mafundi wapo Pemba na wamo katika kushughulikia matatizo hayo na kwa baadhi ya sehemu wamemaliza kutatua, mfano ni katika eneo la Makangale na wanashughulika na hivi sasa wapo katika Shehia ya Sizini. *ZANTEL* haitoishia hapo tu lakini mwisho wa wiki hii, itafanya uchunguzi kwa kutumia kipando *"Driving Test"* na kupitia minara yote ya kisiwani Pemba kwa ajili ya kubaini kama kuna tatizo lolote na kulitatua kikamilifu.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo. Kwakuwa, utakapotaka kuwasiliana na mtu yeyote aliyemo katika vijiji hivi kwa kutumia mtandao wa *ZANTEL* hapatikani hata kwa bahati mbaya mpaka umuandikie barua. Kwahiyo, ni lini Mhe. Waziri atafanya ziara katika vijiji hivyo, ili nikamuoneshe eneo la kutuwekea mnara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa Said Omar Saidi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni juzi tu mimi nilikuwepo Pemba na ninakiri kabisa katika kujaribu mawasiliano sehemu zote alizotaja Sizini, Kijichame, mawasiliano yalikuwa magumu mpaka Kilindini. Kwahiyo, ni kweli tatizo hili lipo na tunakiri kama lipo na *ZANTEL* wako katika hatua ya kulitatuwa na pia niko tayari baada ya kumaliza Baraza tukarudi Pemba kuangalia kama tayari lile tatizo lishatatuliwa.

Nam. 72

Ongezeko la Vitendo vya Udhalilishaji

Mhe. Asha Abdalla Mussa (Kny: Suleiman Sarahan Said) - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetunga sheria kali katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Hatahivyo, yapo mambo yanayosababisha kuendelea kwa udhalilishaji kama watoto kuachiliwa kutembea usiku na wanawake kutovaa mavazi ya heshima.

(a) Je, suala la watoto kutembea usiku bila kikomo na suala la wanawake kutembea na mavazi

yasiyokuwa na heshima hayachangii udhalilishaji huo.

(b) Kama hauchangii miaka ya nyuma iliyopita kulikuwa na kikomo cha muda wa kutembea usiku na wanawake kuvaa nguo za heshima. Je, ilikuwa na sababu zipi kufanya hayo.

(c) Katika juhudi zote za serikali na bado suala hili kama limetiwa mafuta ya petroli na moto serikali imeona nini sababu zake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Bismilah Rahmani Rahim Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahani Said swali lake Nam. 72 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hakuna utafiti au tathmini iliyofanyika kuonyesha kuwa kutembea bila kikomo na kuvaa mavazi yasiokuwa na heshima yanachangia udhalilishaji. Wizara inatowa nasaha kwa wazazi kutowaacha watoto wao kutembea nyakati za usiku na pia wanawake kuvaa nguzo za stara. Vilevile, Vyombo vya Ulinzi na Usalama viwajibike kuwalinda raia kwani nchi ipo huru.

(b) Mhe. Spika, kuhusu miaka iliyopita kuwa na kikomo cha muda wa kutembea usiku na wanawake kuvaa nguo za heshima. Ushauri huo tutauchukuwa na kuufanyia kazi kwa kushirikiana na taasisi husika. Hatahivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu

tusaidiane katika kuhakikisha mila, silka na desturi za Kizanzibari zinaendelezwa katika jamii. *(Makofi)*

(c) Mhe. Spika, ni kweli kuwa pamoja na juhudi zote za serikali bado suala hili kama imetiwa mafuta ya petroli na moto. Sababu zinazochangia hayo ni kutokana na anaopatikana na hatia kushindwa kupewa adhabu kali ambayo itakuwa ni funzo kwao na kwa wengine wenye kutenda vitendo hivyo. Vile vile mmong'onyoko wa maadili katika jamii unachangia katika suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nipongeze kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na katika jibu lake (c) ametuelezea ni sababu ambazo zinazochangia kuongezeka kwa petroli hii ambayo ya uzalilishaji hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, juzi na jana kuna matukio ya uzalilishaji au ya ulawiti kwa mtoto wa kiume na katika mitandao yote ya kijamii swali hili linaeleweka. Lakini cha kuskitisha mtuhumiwa yule mtuhumiwa (x) inasemekana ametolewa yuko nje. Kwa hiyo nataka kwa Mhe. Waziri, Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Je, swali hili ni kweli, na kama ni kweli limechukuliwa hatuwa gani mpaka hivi sasa ili jamii nayo ijue. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tusikilizane. Naomba nimpe Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ili ajibu swali hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Asha Abdalla Mussa kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mtuhumiwa anayemsema Mhe. Asha Abdalla Mussa naamini ni Hassan Aboud Talib maarufu Kiringo, ambaye yuko chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi katika Kituo cha Madema. Kwahivyo, yuko ndani Mhe. Spika. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza, lakini nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kulithibitishia Baraza hili kwamba mtuhumiwa bado yuko ndani baada ya kuachiwa na kurejeshwa tena swali langu liko hapa.

Hivi karibuni Baraza la Wawakilishi lilipitishwa Mswada wa Sheria ambao ulitoka kuweka wasiokuwa na dhamana kutoka makosa 6 mpaka 11na miongoni mwa kosa ambalo halina dhamana ni la ubakaji na ulawiti. Je, serikali tayari imeshatia saini sheria ile na kama bado haraka gani zitafanywa ili kutiwa saini sheria ile. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Machano Othman Said kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi ni juzi tu tumeipitisha sheria hapa Mswada wa Sheria wa Mambo mbalimbali unaohusiana yakiwemo na hayo ambayo Mhe. Mjumbe ameyasema yote, hiyo ni jitihada ya serikali katika kuhakikisha wahalifu wanachukuliwa hatuwa kali, ili kudhibiti makosa mbalimbali yanayotokea yakiwemo ya ubakaji na udhalilishaji.

Hivyo, Mhe. Spika kama unavyoelewa taratibu zetu zinavyokwenda baada ya kumaliza utaratibu wa hapa Barazani na Waheshimiwa Wajumbe kuipitisha sheria ile napenda

niwapongeza kwa mswada huu kupitishwa hapa na Waheshimiwa Wajumbe napenda niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kupitisha Mswada ule, lakini kama kawaida ni lazima mswada huo usainiwe na Mhe. Rais kwa hiyo taratibu zinafanywa na naamini ukifika tu kwa Mhe. Rais shughuli itafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika majumuisho yangu yaliyomalizika jana juu ya kadhia hii ya kudhalilisha watoto wetu na wanawake nilishindwa kuendelea nilitoka machozi mpaka presha ikanipanda hasa nikizingatia kwamba mtoto anatekwa au anachukuliwa na mwenye uwezo wa fedha kwenda kuwafanyia vibara watoto hawa na kuwaweka katika mazingira magumu katika maisha yao. Swali langu liko hapa.

Kwakuwa, tunasubiri sheria hii itiwe saini lakini tunajua kama petroli imetiwa moto yanazidi kuendelea maovu haya na baadhi ya wadau wakubwa wa kuchangia kwenda kuwaokoa wanaofanya maovu ni sisi humu tuliomo ndani. Je, kama serikali itachukua hatua gani kwa kiongozi yeyote kuanzia mtu wa kawaida, sheha, diwani, mwakilishi, waziri na wengineo pindi akienda kulitetea suala hili atachukuliwa hatua gani za kinidhamu, ili ajute maisha yake. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza nisema sheria ni msumeno hakuna aliye juu ya sheria, si sheha, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, waziri, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, na

wala sio mwananchi yeyote ambaye yuko juu ya sheria. Kwahivyo, yeyote yule atakayekwenda kinyume na sheria hatua za kisheria zitachukuliwa na adhabu kali dhidi yake itamkuta. *(Makofi)*

Ningependa nitoe wito, kwa sisi viongozi na kwa wananchi wote kutii sheria bila ya kushurutishwa. Hivi sasa tunaandaa na tayari operesheni maalum zimeanza kupitia Jeshi la Polisi na vikosi vyengine kuwashughulikia wale wote wanaovunja sheria hususan ya udhalilishaji na ubakaji . Kwahivyo, nitoe wito kwa wananchi kwamba hakutokuwa na muhali katika kutekeleza sheria kwenye jambo hili. Hivyo wale wote wanaofikiria kutenda makosa kuacha mara moja, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote. Nataka nimhakikishie Mhe. Ali Suleiman Ali serikali iko macho haitamuonea muhali yeyote yule hata akiwa kiongozi wa namna gani. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Nam. 48

Chombo cha Kuhifadhia Maiti Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa, hivi karibuni kumekuwa na habari njema za kupatikana kwa "*mortuary freezer"* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, jambo ambalo litasaidia sana kuhifadhi maiti na ni faraja kubwa kutokana na kuwa tulikuwa na tatizo hilo.

(a) Je, kifaa hicho kina uwezo wa kuhifadhi maiti wangapi kwa wakati mmoja.

(b) Je, thamani ya kifaa hicho ni kiasi gani.

(c) Je, *"mortuary freezer"* hiyo ni msaada kutoka wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali, naomba kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wanadaispora wenye asili ya Kizanzibari popote walipo, kwa misaada yao mbalimbali wanayotupa ya hali na mali kwa nchi yetu. Tunawashukuru na tunawaomba waendelee kuwa na moyo huo wa kizalendo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo kwa ndugu zetu hawa sasa naomba kujibu swali Nam. 48 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Ni kwamba kifaa cha kuhifadhia maiti, yaani *mortuary freezer* tulilolipata hivio karibuni katika Hospitali ya Mnazi Mmoja lina uwezo wa kuhifadhi maiti wawili kwa wakati mmoja.

b) Thamani halisi ya kifaa hicho ni shilingi 52,470,000/=

c) Kifaa hicho, ni msaada kutoka Shirika lijulikanalo kwa jina la *Zanzibar International Development Organization (ZIDO)* la Canada ambao ni Wanadaispora wenye asili ya Kizanzibari na wengi wao wanaishi nchini Canada.

   Mhe. Spika, kifaa hichi ambacho ni *freezer* maalum la kuhifandhia maiti lilipatikana baada ya mazungumzo baina ya wanadaispora hawa na Mhe. Waziri wa Afya kuhusu mambo mbali mbali yenye maslahi na wanachi wa

Zanzibar likiwemo hili la upatikanaji wa chombo hicho cha kuhifadhia maiti.

Mhe. Spika, wizara yangu pamoja na wananchi wa Zanzibar tunawashukuru sana kwa msaada wao huo.Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Nashukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwakuwa, *freezer* hiyo ina uwezo wa kuchukua maiti wawili, swali langu lipo hapa. Je, itakapotokea vifo vingi vya viwili na *freezer* hii inabeba maiti wawili tu. Kuna utaratibu gani wa kuhifadhi zile maiti nyengine pindi zikitokea kwa wakati mmoja.

(b) Je, gharama halisi ya ununuzi wa kifaa hicho chenye uwezo zaidi ya kubeba maiti wawili ni kiasi gani na lipi lengo la Wizara ya Afya la kununua kifaa chengine kikubwa ambacho kitakuwa na uwezo wa kubeba maiti zaidi ya wawili kwa wakati mmoja, ili kukidhi haja pale litakapotokea tatizo hilo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, tunalo *freezer* jengine ambalo halikidhi sana mahitaji kwasababu lina dosari kidogo, limeshapitiwa na muda ni la muda mrefu. Kwahivyo, hilo tunalitumia bado linafanya kazi lakini kwa kusuasua kidogo. Sasa tunalitumia kwa kuhifadhia maiti na linahifadhi.

(b) Lengo na madhumuni ya wizara tumeshaanza mpango wa kupata *freezer* jengine lenye uwezo mkubwa zaidi, pengine linaloweza kuchukua maiti zaidi ya kumi na gharama yake tunategemea itapita zaidi ya shilingi 52 milioni.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Awali ya yote nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya kwa dhati kabisa kuona huduma za afya katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja inatekelezeka.

Je, ni muda gani *freezer* hilo limekaa mpaka kuweza kutiwa umeme na kuanza kazi. Na tatizo gani lililopelekea kuchelewa kutiwa umeme au kutengenezewa chumba kwa ajili ya kuwekwa *freezer* lile mpaka wale wafadhili waliotusaidia wakaanza kupiga kelele.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, *freezer* hili sina jawabu sahihi la kumwambia ni muda gani nisimwambie uongo hapa ni pahali patakatifu hapapaswi kusema neno ambalo huna uhakika nalo. Lakini hili naomba Mheshimiwa aridhike nimjibu kwa maandishi.

Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakili: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambayo yenye kuleta faraja na kupokea habari njema ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kupatikana kitu muhimu. Je, ni utaratibu gani uliotumika aidha hii *freezer* au mashine hii kuitia pale pale katika *installation* ya mwanzo au kuna utaratibu wa kujengewa pahali pengine ili kusudi tuwe tuna *two unit*, ile *old unit* na *new unit*.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa hayo yaliyoulizwa

pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa masuala yao mazuri sana ambayo yanaonesha umahiri wao katika ufuatiliaji hadi kutaka kujua muda ambao *freezer* limefika mpaka limefungwa. Kwahivyo, hayo niyashukuru ni masuala mazuri sana ya kufuatilia.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakili swali la nyongeza kama ifuatavyo. Hivi sasa tayari tumeshapitisha mpango maalum wa kuhamisha *mortuary* nzima pale ilipo Mnazi Mmoja, kwasababu pale hapafai tena. Hapa pana jengo la *Neuro*, hapa pana Mapinduzi Kongwe, huku kuna jengo kubwa na huku kuna Mapinduzi Mpya ambayo inafanyiwa ukarabati mkubwa wa kuwa *VIP*. Sasa pale mote katika maeneo hayo ukiwa unapitisha maiti na wagonjwa wa *Neuro* wameshafanyiwa operesheni ya kichwa ama uti wa mgongo kule wakawa wanaona maiti zinaingia inaweza kusababisha mshituko na watu kupoteza roho zao. *Mortuary* haitakiwi kukaa pale inatakiwa kidogo iwe kwenye sehemu stara iliyojistiri na iko mbali. (*Makofi)*

Kwahivyo, tunashukuru sana kwa muongozo wa Mhe. Rais mwenyewe Dkt. Ali Mohamed Shein, tumepata eneo lile lote kuanzia majengo mapya mawili wanaita UDOM wenyewe, lakini jengo moja la watoto na kinamama tumepata eneo lile lote mpaka Kizingo. Kwahivyo, *mortuary* sasa na *incinerator* zitapelekwa eneo hilo tayari upimaji wa eneo umeshafanyika. Mamlaka ya Mji Mkongwe kushirikiana na Idara ya Upimaji pamoja na sisi tushakamilisha na wakati wowote hivi sasa ujenzi utaanza.

Pia amejitokeza mfadhili ambaye ametaka kushirikiana nasi katika kujenga jengo la kuosha maiti pale pale, kwenye *mortuary* pembeni yake kutakuwa na jengo la kukosha maiti. Amesema hiyo ni sadaka yake bado hajanipa ridhaa ya kumtaja, lakini

atakaponipa ridhaa ya kutaja nitakuja kumtaja katika Baraza lako tukufu la Wawakilishi. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona na nimpongeze waziri mwenye dhamana ya wizara hii kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar mara nyingi tunapata matatizo katika masuala ya umeme na miaka nenda, miaka rudi vifaa vingi ndani ya serikali hata katika Mnazi Mmoja ukienda kuangalia masuala ya *CT-Scan* na mengineyo yamekuwa yanapata hitilafu hasa inapotokea tatizo la umeme na kupelekea serikali kupoteza fedha nyingi sana.

(a) Ni kwa nini serikali haiangalii utaratibu rasmi wa kuhakikisha mashine nyingi kama hizi ambazo zinagharimu fedha nyingi zinakatiwa bima, ambapo pia zitasaidia kuleta kidogo unafuu kwa serikali pamoja na gari yenyewe anayopanda Waziri wa Afya haina bima.

(b) Ukiangalia kwa upande wa Pemba pia, ukienda Pemba mara nyingi tunapopanga mikakati kama hii ya kujenga *mortuary* maeneo mengine tunakuwa tunaangalia kwa upande wa Unguja. Je, Mhe. Waziri anaweza kututhibitishia hapa kwamba *mortuary* kama hiyo pia itakwenda sambamba wakati inajengwa Unguja pia itakwenda kujengwa na Pemba. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi na kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake yenye (a) na (b). Ni kweli kabisa serikali inaponunua hivi vifaa inakuwa na *warrant*, tunafanya *warrant* na zile kampuni. Kwahivyo, *CT-Scan* iliponunuliwa ilikuwa na *warrant period* yake ambayo baada ya muda huwa inamalizika. *MRI* mpaka hivi sasa ipo kwenye *warrant* ina

warrant ya miaka miwili, lakini kuvikatia bima baada ya hapo kwa kweli hiyo bajeti yetu inakuwa kidogo haituruhusu.

Mara nyingi ukishavikatia bima vifaa kama vile panapotokea maharibiko yoyote, basi haya mashirika nayo huchukua muda mrefu sana kulipa zile bima kwa ajili ya mashine hizo. Kwahivyo, utaratibu huo bado haupo wa kukatia bila kila kilichokuwepo, utaratibu huo bado unafanyika katika *private sector*, lakini katika *public sector* bado haupo utaratibu wa kukatia bima. Lakini tutachukua kama ushauri na tutakwenda kulikalia kitako tutalizungumza na kujadiliana nini tufanye upande wa bima. Kwa sababu kila siku serikali inaongeza bajeti yake kwenye vifaa vipya na vya kisasa.

La pili, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi la kuwa na *mortuary* Pemba. Sisi tumeshalichukua wazo hilo tumeanza kulifanyia kazi tunalifikiria. Hivi sasa Pemba wanahifadhia maiti zao kuna kituo kimoja cha jeshi cha afya ambacho kinaambiwa kina *mortuary*. Mimi bado sikubahatika kukitembelea hicho, lakini sisi tunataka *mortuary* yetu ya Wizara ya Afya pia nayo iweko Pemba angalau ya kuhifadhia maiti watatu mpaka wanne. *(Makofi)*

Shirika hili ni la Canada ambalo mimi nimefanya mazungumzo nao, tuliwakaribisha na bahati nzuri Mhe. Rais aliwatunukia cheti siku ile ya shughuli ya *Hits* iliyofanyika katika ukumbi wa *Hyatt*. Na wao pia tumeshawaomba wakatwambia turidhisheni kwa hili la kwanza tulilokuleteeni kwamba mnalifunga vizuri, mnalitunza linafanya kazi vizuri basi na la pili nalo tutakupatieni.

Kwahivyo, Mhe. Spika Pemba hatukuiacha nyuma Pemba iko ndani ya moyo wetu na ndani ya moyo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, nasimama kwa kanuni ya 37, "Waziri au mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali alililoulizwa waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Spika, suala la gari la Waziri wa Afya halina bima wananchi wanakata bima za magari yao atueleze kwa nini gari la serikali halina bima. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Sijafamu, sijui kama umemfahamu labda unaweza kujibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mimi sikulifahamu swali lake Mhe. Mjumbe na sidhani kama gari langu halina bima iko nje pale kwa hiyo tukitoka akaliangalie.

Mhe. Spika: hilo halihusiani na gari la Waziri wa Afya tu, ni magari ya serikali kwa ujumla haiwezekani kwamba Waziri wa Afya peke yake awekewe bima kwenye gari lake wengine hayana, nafikiri haliko vizuri sana swali lako. Waheshimiwa maswali yamemalizika na hatuna wageni. Katibu shughuli inayofuata.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2017/2018

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, nachukua fursa hii

kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima na kuweza kutukutanisha tena katika ukumbi huu kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wetu.

Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru kwa dhati kabisa Mhe. Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwasilisha kwa muhtasari juu ya kile kamati yetu ilichowasilisha katika ripoti ya mwaka 2018, ambayo imesambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote, kwa wizara mbili ambazo tunazizimamia, Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, kamati inachukua nafasi hii adhimu kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi inayoendelea kuchukua kuimarisha huduma za afya na elimu kwa kuamua kutoa kipaumbele kikubwa. Pia semta hizi mbili kwa mfano ununuzi wa vifaa vya kisasa katika hospitali zetu, ongezeko kubwa la pesa za kunuunlia dawa na vitendea kazi hadi kufikia asilimia mia moja ni ushahidi tosha kwamba serikali hii ya Awamu ya Tano inaendelea kuwajali wananchi wake. *(Makofi)*

Aidha, uimarishaji wa mioundombinu ya elimu katika wilaya zote Unguja na Pemba, kukimu ongezeko kubwa la wanafunzi kamati inaiunga mkono serikali kwa asilimia mia moja. Pia ugatuzi ambao kwa kiasi kikubwa umeanza kuonesha mafanikio katika sekta hizi mbili katika baadhi ya maeneo yaliyogatuliwa.

Mhe. Spika, kamati pia inapongeza hatua zilizochukuliwa na serikali za kuimarisha sekta ya afya kwa kujenga majengo mapya ya kisasa ya hospitali na vituo vya afya kwa lengo la kutoa huduma bora za afya likiwemo jengo jipya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mafanikio haya kwa dhati kabisa naomba kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye amesimamia na kuongoza kwa ufanisi mkubwa juhudi hizo za kupatikana maendeleo makubwa katika sekta za afya na elimu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati yangu imefurahishwa na kupongeza hatua aliyochukua Mhe. Rais kuzitatua changamoto mbali mbali katika sekta ya elimu ambazo kamati imeziona katika ziara zetu. Mhe Rais amebainisha wazi mikakati ya kuzitatua changamoro hizo wakati akifungua mkutano wa Chama cha Walimu (*ZATU*) uliofanyika marehe 10-Februati mwaka 2018. Vilevile, siku ya Mahafali ya Chuo cha Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) yaliyofanyika katika Ukumbi mpya wa Mikutano katika Kampasi ya Tunguu tarehe 15-Feb 2018. Nachukuwa fursa hii kumuahidi kuwa kamati yangu itandelea kushirikiana naye bega kwa bega katika kufikia mafanikio ya utatuzi wa changamoto hizo.

Mhe. Spika, kamati yangu pia inazipongeza wizara zote inazozisimamia ambazo ni Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia kamati katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo bila ya mashirkiano yao, kamati hii isingeweza kufanya kazi zake kwa umakini. *(Makofi)*

Pongezi maalum nazitoa kwa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Waziri wa Afya ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki. Pia Mhe. Riziki Pembe Juma, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Manaibu Mawaziri wao. *(Makofi)*

Aidha, nachukuwa fursa hii kuwamba viongozi wa wizara hizi mbili kuwabana wafanyakazi wachache wanaoharibu kazi nzuri zinazofanywa na wizara zao.

Mhe. Spika, naomba niwatambe Waheshimiwa Wajumbe wa kamati hii kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
   Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
   M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
   Mjumbe
4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
   Mjumbe
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
   Mjumbe
6. Mhe. Hidaya Ali Makame
   Mjumbe
7. Mhe. Makame Said Juma
   Mjumbe
8. Ndg. Aziza Waziri Kheir
   Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji
   Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi naona sasa nijielekeze au n ijikite katika ufafanuzi wa baadhi ya mambo muhimu yalielezewa katika ripoiti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2018, nikianza na Wizara ya Afya.

Wizara ya Afya

Mhe. Spika, Katika kipindi chote cha kazi za Kamati, Kamati imefanyakazi ya kusimamia utekelezaji wa bajeti inayotumia mfumo wa programu katika utekelezaji wake ambapo kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara ilikua na

programu ya Programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Programu ya Tiba, Programu ya Usimamizi wa Sera ya Afya na Utawala na Programu ya Hospitali ya Mnazi mmoja.

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii katika ripoti ya mwaka huu 2017/2018, ilipita na kukagua miradi mbalimbali ya kimaendeleo na kubaini mafanikio na changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja ama nyengine zinakwamisha utekelezaji wa malengo ya Wizara iliyojipangia. Miongoni mwa taasisi zilizokaguliwa na Kamati ni hizi zifuatazo:-

Hospitali na Vituo vya Afya vilivyotembelwa na Kamati- Unguja

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii imehabatika kukaguwa kazi katika Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) iliyopo Bububu, Kituoa cha Afya cha Rahaleo, Kituo cha Afya cha Tumbatu Gomani na Kituo cha Afya Bumbwisudi pamoja na ukaguzi wa Jengo la Kituo cha Afya cha Mbuzini.

Mafanikio

Mhe. Spika, mafanikio makubwa yamepatikana katika uimarishaji wa majengo na kuwepo baadhi ya vifaa. Tunapongeza kwa dhati kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka miundombinu mizuri ya afya kote Unguja na Pemba tena katika masafa mafupi chini ya kilomita 5.

Mhe. Spika, mafanikio mengine ambayo kamati imeyaona ni kuwa vituo vingi vya afya vimepiga hatua kubwa ya maendeleo kwa kutoa huduma mbalimbali za afya kwa wananchi ikiwemo huduma za matibabu ya awali, huduma za kliniki za mama na mtoto na huduma rafiki kwa vijana. Vituo vyengine vimeimarisha

Bodi za Afya ya Jamii na kuwa mfano mzuri kwa vituo vyengine, kama vile Kituo cha Afya Rahaleo.

Changamoto za Jumla zilizobainika na Kamati

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo bado sekta ya afya inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na serikali kama ifuatavyo:-

Idadi ndogo ya Wafanyakazi Na Uchakavu wa Majengo

Mhe. Spika, **k**atika maeneo yote kamati ilipopita imekuta bado kuna changamoto kubwa ya uhaba wa wafanyakazi wa kada mbali mbali jambo ambalo linapelekea kuzorota ama kutopatikana kabisa kwa huduma kwa baadhi ya wakati. Kwa mfano, katika Hospitali ya Abdalla Mzee, kamati imeona kuwa pamoja na ukubwa wa jengo na upya wa jengo hilo lenye vifaa vya kisasa, hospitali inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wa kada mbalimbali muhimu.

Mhe. Spika, wachache zaidi ni wafanyakazi wa usafi ambapo hadi kamati inafanya ziara ya mwisho imebaini kuwa jengo zima lina wafanyakazi watatu tu wa usafi jambo ambalo hupelekea baadhi ya maeneo kutosafishwa kwa wakati na maeneo mengine kukosa kabisa kusafishwa na kuharibu haiba ya jengo hilo ambalo limejengwa kwa gharama na nguvu kubwa za serikali.

Mhe. Spika, tumekuta changamoto ya uchakavu wa majengo na miundombinu ya hospitali na vituo vya afya kama vile paa, dari, uzio na kuta ni tatizo sugu kwa vituo vingi vya afya hasa vilivyopo maeneo ya vijijini, na hata baadhi ya hospitali za mijini kama vile Chake Chake na Wete. Vilevile, kamati ilikaguwa jengo la Kituo cha Afya cha Mbuzini, ujenzi ambao ulianza

mwaka 2004 hadi sasa haujakamilika pamoja na agizo la Mhe. Rais la kufanywa kuwa Hospili ya Wilaya.

Mhe. Spika, **k**atika ziara hiyo kamati ilielezwa kuwa lilitoka agizo la kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi "A" kukabidhi hati miliki ya eneo hilo kwa Wizara ya Afya jambo ambalo lilifanyika. Sambamba na hayo, kamati imebaini kuwa vituo vingi vya afya havina hati miliki ya maeneo yao na hali hiyo inaweza kuchochea kuvamiwa maeneo ya vituo hivyo.

Mahusiano kati ya Jamii na Hospitali

Mhe. Spika, kamati katika ziara zake imegunduwa kuwa baadhi ya wanajamii wamekua hawatoi mashirikiano ya kutosha kwa watendaji hasa wa vituo vya afya vilivyopo vijijini na kusababisha kuzorota kwa utoaji wa huduma za afya kwa wanajamii. Katika Kituo cha Afya cha Kojani, kamati ilibaini kuwa baadhi ya wana jamii wanamsumbua Muuguzi na Mkunga Mkuu wa Kituo hicho ambaye anaishi katika nyumba iliyojengwa na *TASAF* jirani na kituo hichom cha aafya.

Stahiki za Wafanyakazi

Mhe. Spika**,** changamoto ya malipo na stahiki za wafanyakazi hasa likizo imejitokeza kwa ukubwa wake. Kamati imegunduwa baadhi ya wafanyakazi hawajapata likizo zao kwa muda mrefu jambo ambalo linawatia unyonge wafanyakazi hao kutokana na kukosa likizo ambayo ni haki yao ya kisheria. Wapo wafanyakazi waliopata likizo zao lakini kumekuwa na ucheleweshwaji wa fedha za likizo kwa muda mrefu sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati imepata malalamiko kutoka kwa baadhi ya wafanyakazi wa vituo vya afya kukosa nafasi za masomo, ambapo baadhi yao tayari walilipia gharama zao na baadae walipatiwa

taarifa kuwa wasubiri wasiendelee na masomo hayo hadi mwaka mwengine wa masomo jambo ambalo hadi leo hii halijafanyika na muda wa masomo walioambiwa wasubiri tayari umeshapita. Pia, kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya wauguzi wanapomaliza masomo yao hasa *"General Nurse"* hawataki kufanya kazi za uuguzi na ukunga na wengi wao hubakia kliniki tu na kazi kubwa huwaachia wanafunzi au *junior staff* na hata *Ordals* baadhi ya vituo.

Changamoto Mahususi katika Hospitali na Vituo vya Afya vilivyotembelewa na Kamati

Mhe. Spika**,** zipo changamoto mahususi zinazokabili uendeshaji wa hospitali na vituo vya afya tulivyovitembelea kwa mfano Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyopo Bububu kutopatiwa mgao wa dawa kutoka Bohari ya Dawa ya Zanzibar. Kamati, ilipofanya ziara katika Hospitali ya Jeshi iliyopo Bububu ilielezwa kuwa yanapopelekwa maombi ya dawa kwenye Bohari ya Dawa ya Tanzania Bara yaani (*MSD*) hawapatiwi mgao wa kutosha kwa vile wao wapo Zanzibar.

Mhe. Spika**,** wakati huo huo wanapofanya maombi kwenye Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar (*CMS*) pia hawapati mgao vile wanaonekana ni Taasisi ya Muungano na huduma zao zinatolewa kwa malipo ambapo ni kinyume na Sera ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo huduma za matibabu kwa wananchi ni bila ya malipo bure.

Mhe. Spika, kamati imefahamishwa zipo huduma zinazotolewa bila ya malipo yoyote katika Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ya Bububu ikiwemo huduma za kupima VVU ambazo dawa na vipimo ni bure lakini lakini tatizo bado hawapatiwi msaada wa vitendanishi vya maabara na Wizara ya Afya angalau kwa huduma hizo, hali hii inalazimisha wananchi ambao si askari kutozwa kwa huduma hizo.

Mhe. Spika, vile vile Kamati imewahi kuripoti tatizo hili kwa Hospitali za Idara Maalumu za SMZ mfano Hospitali ya KMKM ya Kibweni na kamati imeelezwa kuwa linafanyiwa kazi baina ya Wizara ya Afya na Uongozi wa KMKM. Aidha, tumebaini pia tatizo la upatikanaji wa dawa kwa wakati kwa baadhi ya hospitali na vituo vya afya hali hii huleta usumbufu kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma ambao hulazimika kununuwa dawa hizo. Pia katika baadhi ya vituo vya afya kamati imebaini kuwa dawa muhimu wanazopatiwa ni chache kulingana na mahitajhi yaliyopo kwa wakati ule.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa pamoja na kutolewa kwa huduma mbalimbali katika vituo vya afya na hospitali za jeshi na kumetolewa ushauri kuwa wizara waweke kitengo cha Ustawi wa Jamii katika kuwasaidia wagonjwa wanaofata huduma ambazo zinalipiwa katika Hospitali Binafsi na ambazo pengine hazipatikani katika hospitali za umma, ili wagonjwa wasioweza kulipa waweze kupatiwa nafuu na serikali kupitia Kitengo cha Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, katika Kituo cha Afya Rahaleo, kuna changamoto kubwa ya kuzidiwa na idadi ya watu wanaofuata huduma ambao wanatoka nje ya shehia tatu zinazohudumiwa na kituo hicho. Shehia hizo ni Mitiulaya, Rahaleo na Miembeni. Hali hii inatokana na ukweli kuwa kituo kipo kati kati ya mji na wananchi wengi kutoka maeneo mbalimbali hufuata huduma za afya kituoni hapo. Hatimaye kituo hicho kuzidiwa na idadi ya wagonjwa huku idadi ya wafanyakazi wanaotoa huduma ikiwa ni ndogo.

Mhe. Spika**,** pia hali hiyo inaathiri mgawanyo wa dawa na vifaa kwa kuwa dawa zinazopelekwa kituoni hapo zimelenga kutibu wananchi wa shehia tatu tu zilizokusudiwa kuhudumiwa na kituo hicho. Pia, kamati imebaini kwamba kituo kina ukosefu wa

sehemu ya kutupia taka kwa vile hakina nafasi ya kutosha. Vilevile, kuna tatizo la kujaa kwa maji ya mvua kutokana na kituo kutokuwa na mfumo wa uondoaji wa maji hayo wakati mvua inaponyesha.

Mhe. Spika, vilevile, Kituo cha afya cha Rahaleo kina tatizo la usalama, yapo matukio ya wizi yameripotiwa kutokana na kukosekana kwa ulinzi wa uhakika. Kamati imefahamishwa kuwa walinzi walikuwepo watatu ambao siyo waajiriwa lakini wameondoka na amebakia mmoja tu kutokana na kukata tamaa ya kuajiriwa na wizara. Uongozi wa kituo umeomba kupatiwa walinzi kutoka Idara Maalumu lakini hadi kamati inamaliza ziara kituoni hapo ombi hilo halijatekelezwa.

Mhe. Spika, kamati ilifanya ziara katika Kituo cha Afya cha Tumbatu Gomani ambapo ilibaini changamoto kadhaa kama vile uhaba wa wafanyakazi hasa wataalamu wa maabara, kukosekana kwa uzio katika eneo la kituo hali inayoweza kusababisha uharibifu wa mali za kituo na kukosekana kwa huduma ya maji safi ya uhakika. Katika eneo la kituo kamati imeona kuwa lipo eneo linamilikiwa na Ushirika wa Songambele eneo ambalo tayari limeombwa kuwa kwenye miliki ya kituo kwa vile lipo mkabala na kituo lakini mpaka hivi sasa bado eneo hilo lipo katika milki ya ushirika**.**

Mhe. Spika, lakini tatizo jengine tumelibaini ni la uwekaji sahihi wa takwimu za chanjo, inaonekana kituo kinafanya vizuri katika mwitikio wa chanjo kutoka kwa wanajamii lakini taarifa zilizoko wilayani ni tofauti na zile za kwenye kituo.

Mhe. Spika, kutokana changamoto hizo kamati imetoa maoni yake, ushauri na maagizo ya kufanyiwa kazi na wizara, ili kuzitatuwa changamoto hizo zilizoelezwa kwenye ripoti ya kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza mmepatiwa.

Tumeeleza njia za kutatuwa changamoto hizo kwa mfano suala la kutopatiwa mgao wa dawa kwa Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania Bububu na Hospital za Idara Maalumu za SMZ ingawa hospitali hizo zinatoa huduma kubwa kwa wananchi.

Mhe. Spika, tumeishauri wizara ikae nao na kuona namna hospitali hizo zitapatiwa mgao wa dawa, kwenye changamoto ya uhaba wa wafanyakazi tumeshauri mikakati ya makusudi ifanyike kuongeza ajira kwa wataalamu na vivutio vya ajira. Pia tumeshauri hatua za kuchukuliwa kukisaidia kituo cha Afya cha Rahaleo na Tumbatu Gomani sambamba na changamoto kadhaa zinazokabili vituo vyengine vya afya mfano wa hivyo.

Kazi za Kamati katika Hospitali na Vituo vya Afya kisiwani Pemba

Mhe. Spika, katika kazi zake Kisiwani Pemba Kamati ya Ustawi wa Jamii ilipata fursa ya kukaguwa Hospitali na vituo vya Afya. Hospitali zilizotembelewa ni Abdalla Mzee ya Mkoani, Hospitali ya Chake Chake, Hospitali ya Wete, Kituo cha Afya Kojani na Kituo cha Afya cha Kisiwa Panza.

Katika kazi ya kupitia hospitali na vituo vya afya vilivyotajwa hapo juu, kamati imeona mafanikio yaliyopatikana kutoka na huduma zinazotolewa lakini pia zipo na changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mafanikio:
Mhe. Spika, Katika Hospitali ya Abdalla Mzee tumefahamishwa kwamba ni Hospitali pekee yenye kutoa huduma za '*orthopedic*' kwa upande wa kisiwa cha Pemba. Pia Hospitali ya Abdalla Mzee ina kipimo maalum cha hatua za *DNA, electrolite* na *Chemistry.*

Mhe. Spika, katika Hospitali ya Chake Chake, kamati imeripoti mwaka uliopita kuhusu tatizo ubovu wa paa la hospitali hiyo hivi sasa limeshaingizwa katika mpango wa kulikarabati na hatua za ujenzi zinatarajia kuanza wakati wowote, hii ni hatua nzuri ya kutekeleza maagizo na ushauri wa kamati na sisi tunawapongeza.

Mhe. Spika, katika Hospitali ya Wete imeendelea na utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati katika ziara zake zilizopita ambapo kamati iliridhishwa na hatua mbalimbali za utekelezaji wa maagizo mengi na ushauri uliotolewa na kamati. Kamati ilikuta baadhi ya changamoto ilizozibaini zimetekelezwa na nyengine zinaendelea kuchukuliwa hatua katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018, mfano wa baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na stahiki za wafanyakazi, ukarabati wa baadhi ya miundombinu, upatakinaji wa dawa na vifaa tiba.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo na hatua nzuri ambazo serikali inazichukua kuondoa matatizo na kero mbalimbali zilizopo katika hospitali na vituo hivyo, zipo baadhi ya changamoto bado hazijachukuliwa hatua.

Changamoto katika Hospitali na Vituo vya Afya vilivyopitiwa na Kamati Pemba

Mhe. Spika, kwa ujumla vituo vya afya vilivyotembelewa an Kamati Pemba vimekuwa na Changamoto ya uhaba wa wafanyakazi katika kada mbali mbali jambo hupelekea kuzorota ama kutopatikana kabisa kwa huduma kwa baadhi ya wakati. Vilevile, changamoto ya ubovu wa majengo na miundombinu ya hospitali na vituo vya afya kama vile paa, dari, uzio na kuta kwa vituo vingi vya afya hasa vilivyopo maeneo ya vijijini na tatizo la mashirikiano madogo yaliyopo baina ya jamii na vituo vya afya, kama lilie tulilolibaini katika Kituo cha afya cha Kojani ambapo

Mkuu wa Kituo hana utulivu katika nyumba anayoishi pembezoni mwa kituo.

Mhe. Spika, zipo changamoto mahususi kwa kila eneo ambalo kamati imetembelea kwa mfano katika Hospitali ya Wete tumeona kuna nyumba ndani ya eneo la hospitali ambayo inayomilikiwa na Wizara ya Ardhi, awali nyumba hiyo ilikuwa ikitumika kwa matumizi ya hospitali hiyo lakini baadae uongozi wa hospitali uliarifiwa kuwa nyumba hiyo inamilikiwa na Wizara ya Ardhi ambapo hivi sasa nyumba hiyo haitumiki ipo katika hali mbaya, inaendelea kuharibika na kuleta picha isiyokuwa nzuri kati kati ya eneo la Hospitali ya Wete.

Mhe. Spika, vile vile, kamati imeona kipo kiwanja kitupu mkabala wa nyumba ya Wafanyakazi wanaoishi madaktari wanaotoka nchini Cuba (*Vuga flat*) iliyopo Wete. Hatahivyo, kiwanja hicho hakijaendelezwa na hakijulikani mmiliki wake, kamati imeshauri kwamba wizara wachukuwe hatua ya kukiomba serikalini, ili siku za usoni kiweze kutumika kuweka jengo la nyumba zaidi za madaktari katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kamati imebaini changamoto ya vifaa katika hospitali na vituo vya afya Pemba mfano kuharibika kwa mashine ya kusafishia picha katika Hospitali ya Chake Chake jambo ambalo limekuwa ni kero na usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaohitaji kupatiwa huduma hiyo. Lakini pia, kituo cha Afya Kojani kuna ukosefu wa darubini ya uchunguzi (*microscope*) pamoja na ukosefu wa daktari wa meno ambapo vifaa vya kung'olea meno vipo lakini daktari wa kufanya kazi hiyo hayupo.

Mhe. Spika, katika Hospitali ya Abdalla Mzee, kamati imebaini changamoto kadhaa kama tulivyozisema kwa kirefu katika ripoti mfano tatizo la wafanyakazi wanaoletwa kutoka Unguja kuhama muda mfupi baada ya kuripoti kazi Pemba. Vilevile, hospitali

haina *account* yake ya fedha na kupelekea fedha zinazohitajika kwa huduma za hospitali zipitie mzunguko wa vifungu vya kasma za Wizara kupitia Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Mhe. Spika, Hospitali ya Abdalla Mzee inakabiliwa na tatizo kubwa la kukatika umeme mara kwa mara na kuhatarisha usalama wa vifaa mbalimbali vikiwemo vifaa tiba vilivyofungwa hapo hospitali. Kamati imepata maelezo kwamba Shirika la Umeme limeshafanya ukaguzi lakini hawajaleta mrejesho mpaka hivi sasa na umeme huwa unakatika mara kwa mara. Kamati imeelezwa kwamba hospitali haina mtambo wa gesi (*Oxygen*) na kwa sasa mitungi iliyopo ni 11 tu ambayo haikidhi haja hasa ukizingatia kwamba huduma za upasuaji zinafanyika kila siku.

Mhe. Spika, tumeripoti pia tatizo la kukosekana kwa mfumo wa kuweka takwimu kielektroniki tatizo ambalo kamati imeliona na badala yake uwekaji wa takwimu kwa sasa unafanyika kwa njia za kawaida yaani *manual* na njia zisizo za ufanisi na zinatumia muda mwingi.

Mhe. Spika, kamati imeelezwa tatizo la makaazi ya watendaji wa Hospitali hiyo ya Abdalla Mzee ni changamoto ingawa tumepata maelezo kuwa kiwanja kipya pembezoni mwa Hospitali kimeshapatikana kwa ujenzi mpya wa nyumba za makaazi ya madaktari.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hizo kamati yetu yangu inaishauri serikali kuchukua hatua za haraka za kuliondoa tatizo la ukosefu wa wafanyakazi ambalo kwa kiasi kikubwa hivi sasa limekuwa ni tatizo sugu katika vituo vya afya na hospitali nyingi za Unguja na Pemba. Kamati inapendekeza kwamba Wizara ya Afya ipewe kibali maalum au kipau mbele kwa kada zote afya

hasa vituo vya afya vya vijijini vyenye upungufu mkubwa katika suala zima la uajiri likiweka sheria maalum ya uajiri Serikalini.

Mhe. Spika, kamati inashauri hivyo kutokana na matatizo makubwa ya uhaba wa wafanyakazi iliyoyakuta na mfumo wetu wa uajiri kuwa na urasimu mkubwa, jambo ambalo hupelekea ajira kuchukua muda mrefu na hata kuwafanya vijana waliohitimu masomo kutafuta na kufuata ajira nje ya Zanzibar na kusababisha tatizo la ukosefu wa wafanyakazi kuongeza siku hadi siku, ingawa vijana wenye sifa mitaani wapo kwa wingi. Aidha kamati inaishauri Wizara ya Afya kulifikiria upya suala la usafi wa Hospitali ya Abdalla Mzee kwa kuajiri kampuni ya usafi ambayo itaweza kufanya usafi wa jengo zima kwa muda wote au kuajiri *ordeals* wa kutosha watakakidhi haja.

Mhe. Spika, kamati imeagiza pia changamoto ya ukosefu wa vifaa kama vile mashine ya kisasa ya kusafisha picha ipatiwe ufumbuzi katika Hospitali ya Chake Chake pamoja na Hospitali nyengine zenye upungufu kama huo. Vilevile, kamati imeagiza wizara kufanya utaratibu wa kununua darubini ya uchunguzi (*microscope*) katika kituo cha Afya Kojani.

Mhe. Spika, ripoti yetu tumeshauri Serikali kuchukua hatua za makusudia kwa kuiangalia upya na kuitatulia changamoto za Hospitali ya Abdalla Mzee kwa kuwaongezea vivutio vya kimaslahi *"incentives"* wafanyakazi waliopo, ili waweze kufanyakazi katika mazingira ya Pemba na kuwashawishi wabakia kisiwani humo kutokana na ukweli kwamba wafanyakazi wengi wakihamishiwa Pemba huondoka aidha kwa kuomba uhamisho kurudishwa Unguja, kuolewa kwa upande wa wanawake au kutafuta kazi sehemu nyengine. Aidha, Kamati imeshauri kuangalia upya uwezekano wa kuipatia Hospitali ya Abdalla Mzee *account* yake maalum ya fedha ili kuondoa

usumbufu uliopo hivi sasa wa kusubiri fedha zipitie mzunguko wa vifungu vya kasma za Wizara ya Afya Pemba.

Mhe. Spika, kamati imeshauri wizara kufanywa utaratibu wa kununua vifaa maalum vya umeme ambavyo kamati ilielezwa kuwa maombi ya vifaa hivyo yameshawasilishwa wizarani na uongozi wa Hospitali ya Abdalla Mzee, kwa ajili ya kuondoa tatizo kubwa la kukatika umeme mara kwa mara na kuhatarisha usalama wa *X-ray machine* pamoja na vifaa tiba vyengine. Kamati inashauri kuwa ni vyema wizara ikafanya utaratibu wa kununua mtambo wa gesi (*Oxygen*) kwa hospitali hiyo, ili iweze kusaidia upatikanaji wa *oxygen* hapo hapo Hosipitali.

Mhe. Spika**,** kamati inaishauri serikali kufanya mkakati maalumu wa kuyakarabati baadhi ya majengo ya vituo vya afya ambayo miongoni mwao ni mabovu na mazingira yake hayaridhishi kutoa huduma kwa wagonjwa wanaofika hospitalini hapo. Aidha, kamati inashauri kwamba kutokana na hatua ya serikali ya kuamua kugatua baadhi ya huduma zikiwemo huduma za afya, ni vyema kwa wizara husika kukaa na Halmashauri za Wilaya na Manispaa na Mabaraza ya Miji kuyakarabati majengo yaliyopo katika wilaya zao kwa awamu, ili changamoto ya ubovu wa baadhi ya vituo vya afya na hospitali uweze kuondoka.

AFISI ZA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Mafanikio

Mhe. Spika, kamati ilifanya ziara katika Afisi na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali hapo Maruhubi na kuelezwa kuwa afisi hiyo imepiga hatua kubwa ya maendeleo kwa kupata jengo jipya ambalo ujenzi wake umekamilika. Tunaiopongeza sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikisha ujenzi

na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (*Government Chemist*).

Mhe. Spika, hatua iliyobaki hivi sasa ni ya uwekaji samani na vitendea kazi. Aidha kamati ilielezwa kuwa kutokana na ukubwa wa eneo waliopata Afisi ya Mkemia Mkuu imeongeza wigo wa kufanya kazi kwa kuongeza maabara nyengine afisi itakua na maabara nane ukilinganisha na Maabara tatu zilizokuwepo hapo kabla.

Changamoto

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo, kamati imebaini changamoto kadhaa za msingi zinazoikabili Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo hatua za haraka zinahitajika kuchukuliwa ili kuiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi kwa umakini zaidi. Changamoto zenyewe ni pamoja na uchache wa fedha za ruzuku inayotolewa ambapo katika bajeti hii fedha hizo zimezidi kuwa pungufu na kupelekea kukwama kufanyika kwa baadhi ya kazi za msingi za maabara.

Mhe.Spika, hali hii inaonekana wazi kutokana na kushuka kwa ruzuku ambapo katika bajeti ya mwaka 2014/2015 afisi ilipewa ruzuku ya shilingi milioni 700; 2016/2017 ilipatiwa shilingi milioni 600 na mwaka 2017/2018 ilipatiwa shilingi milioni 500. Malengo ya fedha hizi ni kuendesha kazi mbalimbali za kimaabara na utawala katika Afisi ya Mkemia Mkuu.

Mhe. Spika, kamati pia imegundua changamoto ya kuhama kwa baadhi ya wataalamu wa maabara kutokana na kuwepo kwa tofauti ya maslahi baina ya Afisi ya Mkemia Mkuu na taasisi

nyengine jambo ambalo husababisha baadhi ya wataalamu muhimu na adimu kuhamia kwenye taasisi zenye maslahi mazuri zaidi. Aidha, changamoto ya maslahi madogo pia inahatarisha ufanisi wa kazi kutokana na uwezekano wa kurubuniwa kwa baadhi ya wataalamu na watuhumiwa hasa wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya ambapo yanapokamatwa vipimo vyake hufanya na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, Mkemia Mkuu anakabiliwa na changamoto kubwa nyengine ya kutakiwa kuhudhuria mahakamini katika kesi nyingi zinazohitaji ushahidi kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Mahakamani jambo ambalo kwa kiasi kikubwa hupelekea kesi nyingi kufutwa kutokana na uchache wa wataalamu ambao wangeweza kufika Mahakamani na kuwasilisha vielelezo vinavyohitajika.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkemia Mkuu ina gari moja tu ambayo inatumiwa na viongozi wa taasisi hiyo, kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa kuwafikisha wataalamu hao Mahakamani kunakwamisha utendaji wa Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kamati ilielezwa kwamba changamoto ya wataalamu wa Afisi ya Mkemia Mkuu kupewa*"risk allowance"* ndogo mno ya shilingi 75,000/= tu ukilinganisha na kazi ngumu na nzito wanazozifanya.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hizo kamati inaishauri wizara na serikali kwa ujumla kuiongezea ruzuku Afisi ya Mkemia Mkuu, ili kazi zinazopangwa kufanyika katika afisi hiyo zifanyike kwa wakati uliopangwa chini utaalamu wa hali ya juu ambao upo. Kitendo cha kuipunguzia ruzuku afisi hii kimeisikitisha mno kamati kutokana na uhalisia wa kazi

zinazofanywa na afisi hii pamoja na vifaa vinavyohitaji gharama kubwa.

Mhe. Spika, kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuwaongezea wataalamu wa Afisi ya Mkemia Mkuu maslahi yao, ili changamoto ya kuhama kwa baadhi ya wataalamu wa maabara na kuhamia taasisi zenye maslahi mazuri zaidi iweze kuondoka.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali kushughulikia na kuyafanyiakazi mapendekezo yao ya *"Scheme of Service"* ambayo yameshawasilishwa katika wizara inayoihusika na utumishi zaidi ya mara moja lakini bado hakuna hatua zilizochukuliwa. Hali hii inawakatisha tamaa watendaji wa Afisi ya Mkemia Mkuu na kuwavunja moyo na hatimaye baadhi yao kuondoka kwa ajili ya kufuata maslahi mazuri kwengine. Aidha, kamati inazidi kusisitiza kuongezwa kwa maslahi ya watalamu hao, ili ufanisi wa kazi zao uweze kupatikana *pamoja* na kuepuka vishawishi vya watuhumiwa ambao wanaweza kuwarubuni wataalamu wetu kwa fedha nyingi, ili waharibu ushahidi.

Mhe. Spika, kamati imesikitishwa na taarifa iliyopatiwa na Afisi ya Mkemia Mkuu kwamba baadhi ya wataalamu wake hudhalilishwa na watendaji wa Mahakama wanapokwenda mahakamani kutoa ushahidi wa vielelezo walivyovichunguza, hivyo kamati inaiomba wizara na serikali kwa ujumla kulichunguza suala hilo kwa undani zaidi endapo ni kweli linafanyika, wahusika wa kadhia hiyo wachukuliwe hatua za kinidhamu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kamati inaishauri Wizara ya Afya kukutana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kulizungumza upya suala la wataalamu wa Afisi ya Mkemia Mkuu kuhudhuria Mahakamani katika kila kesi wanazotakiwa kuzitolea ushahidi wa kimaabara kutokana na

ukweli kuwa baadhi ya kesi ndogo ndogo zinahitaji *"certificate"*tu ya uchunguzi tu ili ziweze kuiendelea.

Mhe. Spika, kamati inashauri hivyo kwa kuwa wataalamu waliopo katika Afisi ya Mkemia Mkuu kwa sasa ni wachache na hawatoshelezi katika hitaji hilo na endapo ushauri huu utafanyiwa kazi utapunguza na kuondosha kabisa hali iliyopo hivi sasa katika Mkoa wa Kusini Unguja kesi nyingi kufutwa kutokana na kukosekana kuhudhuria Mahakamani kwa mtaalamu kutoka Afisi ya Mkemia Mkuu. Aidha, kwa kesi ambazo ni kubwa na zina maslahi ya nchi, Kamati haina pingamizi na takwa la sasa la kuwalazimisha au kuwataka wataalamu wa Mkemia Mkuu kuhudhuria katika kesi hizo kutokana na uzito wa kesi zenyewe.

AWAMU YA MWANZO YA UGATUZI WA ELIMU

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi katika kazi zake za kuisimamia serikali imepewa jukumu la kuzisimamia Wizara mbili ambazo ni Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama nilivyosema hapo awali. Kutokana na hali hiyo kamati ilifanya juhudi ya kukutana na taasisi zilizogatuliwa kwa kufanya ziara katika Manispaa na Halmashauri na Wilaya mbali mbali za visiwa vya Unguja na Pemba kuona maendeleo ya afya katika awamu hii ya mpito ya ugatuzi, ili kuondosha uwezekano wa pengo katika utendaji kwa mantiki hiyo hasa sababu za kamati hii kutembelea sehemu ya ugatuzi kwa upande wa elimu na afya.

Tunashukuru kamati wenzetu ya Sheria na Utawala Bora na Idara Maalum nao walifanya kazi kama hii lakini sisi hasa tulikwenda kuona ile *transtion* kutoka wizara mama na uko inakopelekwa ikoje, na mambo yanaendeleaje na kwa kweli tumegundua mengi sana ambapo yatasadia sana sisi tena tukabidhi tusirudi tena katika

ugatuzi. Kwahivyo, tunawakabidhi wao waendelee pale tulipowachia sisi tunawapa kijiti sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa kisiwa cha Unguja, kamati ilifanya ziara katika Halmashauri za Wilaya ya Kaskazini A na Kaskazini B, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini na Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Kwa upande wa Pemba kamati ilifanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Baraza la Mji la Wete, Chake Chake na Mkoani pamoja na kukutana na watendaji wa Wilaya hizo na Madiwani kuzungumzia masuala ya afya ambayo kwa kiwango kikubwa bado yanasimamiwa na Wizara ya Afya.

Mambo yaliyogatuliwa katika Sekta ya Afya

Mhe. Spika, mambo muhimu yaliyogatuliwa kwa Wizara ya Afya ni Uendeshaji wa Vituo vya Afya vya Daraja la kwanza na Daraja la Pili.

Mambo ambayo Hayajagatuliwa

- Uajiri wa wafanyakazi bado unasimamiwa na Wizara ya Afya;
- Mishahara ya watendaji bado inalipwa na Wizara ya Afya;
- Sera, miongozo, mikakati, dawa na vifaa bado vinaendelea kusimamiwa na Wizara ya Afya;
- Kurugenzi yote ya Kinga bado ipo Makao Makuu ya Wizara na Mkurugenzi wake.

MAFANIKIO YA UGATUZI KATIKA SEKTA YA AFYA

Mhe. Spika, pamoja na hatua hii ya awali ya ugatuzi wa baadhi ya huduma za afya kamati imeona kuna mafanikio makubwa yameanza kupatikana kama ifuatavyo:-

a. Halmashauri za Wilaya zote zimeupokea ugatuzi vizuri na mpaka hivi sasa tayari kazi zilizopangwa zimeshaanza na kazi zinafanyika licha ya changamoto kadhaa zinazojitokeza. Tunaiopongeza sana Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa kulipokea vizuri swala la ugatuzi na kutoa elimu ya kutosha katika Wilaya zote.
b. Serikali za Mitaa zimekuwa zinafuatilia kwa karibu huduma za Afya zinazotolewa katika Vituo mbalimbali vya Afya vilivyogatuliwa.
c. Upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (O/C) na upelekaji wa huduma umeanza kuwa wa ufanisi baada ya ugatuzi.
d. Serikali kuu imepunguziwa mzigo na urasimu wa upatikanaji na uendeshaji wa huduma za msingi za afya na huduma hizo kwa sasa zimeanza kuwa za ufanisi na usimamizi mzuri.

CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA KIPINDI CHA MPITO CHA UGATUZI-UNGUJA

Mhe.Spika, Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kamati imebaini changamoto kadhaa katika ugatuzi katika sekta ya afya kama ifuatavyo:-

a) Madiwani wanahitaji kuelimishwa zaidi na kufahamishwa kwa kina sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 na Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira ambazo zimeweka masharti yanayofafanua majukumu ya msingi ya Madiwani, ili Waheshimiwa Madiwani waweze kusimamia ipasavyo majukumu yao mbali mbali.
b) Kuna uhaba mkubwa wa watendaji hasa madaktari na wauguzi, ambapo imeelezwa kwamba moja ya sababu yake ni mfumo wa uajiri unaotumika hivi sasa ambapo uajiri huchukuwa muda mrefu na hauzingatii mahitaji

halisi ya watumishi wanaohitajika katika maeneo ya Wilaya husika.

c) Ushirikiano mdogo kwa baadhi ya Wilaya kutoka kwa baadhi ya viongozi wa Jimbo kama vile Wawakilishi na Madiwani jambo ambalo limepelekea baadhi ya kazi zilizogatuliwa kutofanyika kwa ufanisi.
d) Changamoto ya vitendea kazi hasa usafiri nayo ni miongoni mwa changamoto kubwa iliyojitokeza na kupelekea kuzorota kwa ufuatiliaji wa kazi zilizopangwa.
e) Serikali za Mitaa zinapata changamoto ya bajeti baada ya kuongezwa majukumu ya ugatuzi, ingawa fedha zinapatikana lakini hazitoshi, zipo wilaya wanapata pesa za kuendeshea kazi. Lakini bado kuna wilaya nyengine hawajaziona hipo pesa.
f) Mashirikiano madogo kwa baadhi ya maeneo baina ya Madiwani, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wa Wizara yanazorotesha kazi za ugatuzi na baadhi yao kufanyika pasi kuwashirikisha wahusika hasa Waheshimiwa Madiwani.
g) Madiwani wamekuwa na uwelewa mdogo kuhusu dhamana zao za kusimamia, kuhoji na kupitisha bajeti za Mabaraza na Halmashauri zao wakati fedha za ugatuzi zimeshaanza kufikishwa kwenye uangalizi wao.

CHANGAMOTO ZINAZOKABILI SEKTA YA AFYA KATKA KIPINDI CHA MPTO CHA UGATUZI – PEMBA

Mhe. Spika, Changamoto za kipindi cha mpito cha ugatuzi ambazo zimebainika na kamati katika ziara yake kisiwani Pemba ni hizi zifuatazo:-

a) Kukosekana miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya zilizogatuliwa. Kamati imebaini kuwa baadhi ya kazi zinafanyika kila mtu na mtizamo wake kupelekea kukosekana kwa *“uniformity”*. Hakuna mpango

wa makabidhiano na maelekezo ya namna ya kusimamia huduma zilizogatuliwa kwa afya kutoka zilipokuwepo kwenda Serikali za Mitaa.

b) Kumekosekana ufahamu wa kutosha wa dhana ya ugatuzi kwa baadhi ya watendaji wa Serikali za Mitaa na sekta ya Afya. Kamati imebaini baadhi ya huduma zilizogatuliwa zinapata changamoto kutokana na baadhi ya watendaji wa sekta ya afya kuendelea kuhodhi baadhi ya nyenzo za utendaji kazi, kwa mfano vyombo vya usafiri.

c) Mawasiliano yasiyotosheleza baina ya Watendaji wa Serikali za Mitaa wenyewe kwa wenyewe na watendaji wa Sekta ya Afya. Kamati imebaini baadhi ya wafanyakazi wa Sekta ya Afya wamepewa uhamisho kutoka Pemba kwenda maeneo mengine muda mfupi baada ya kuripoti vituoni mwao. Aidha, baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zimeifahamisha kamati kuwa kumekuwa hakuna vikao vya kuratibu utendaji kazi wa huduma zilizogatuliwa na watendaji wa afya.

d) Kutoshirikishwa na kutambuliwa kwa baadhi ya madiwani katika maeneo ya Serikali za Mitaa ambako huduma za ugatuzi zinahitaji kufuatiliwa na kusimamiwa.

e) Madiwani na baadhi ya watendaji wa Serikali za Mitaa kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira na Sheria za Mfuko wa Jimbo ambazo zinahusiana moja kwa moja na kazi na uwezo wa kufanya majukumu yao ya usimamizi kwa uhakika na kujiamini zaidi.

f) Madiwani hawana nyenzo za kufanyia kazi hasa baaada ya maeneo ya wadi zao kuongezeka sambamba na huduma zilizogatuliwa, mfano wa nyenzo hizo ni vyombo vya usafiri vya kuwawezesha kufatilia majukumu hayo. Tunaipongeza Wizara ya Afya Pemba kwa kuwapatia gari Baraza la Mji Mkoani kusaidia kazi za DHMT.

g) Uhaba mkubwa wa watendaji hasa madaktari na wauguzi katika vituo vya afya.
h) Uratibu hafifu kutoka baadhi ya Ofisi za Wilaya kutokana na uchache wa maafisa na ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi.

MAONI YA UJUMLA YA KAMATI KUHUSIANA NA UGATUZI

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua nafasi hii kuipongeza serikali kwa uamuzi wake makini wa kuamua kugatua baadhi ya maeneo katika sekta ya afya ambazo kamati inazisimamia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya ziara kisiwani Pemba na Unguja na kukutana na madiwani na watendaji wa Serikali za Mitaa, ambako ugatuzi ndiko unakohusika zaidi, kamati inaishauri serikali na wizara zote zinazohusika kuzichukua changamoto hizi zilizoonekana na kamati na kubainishwa ndani ya ripoti na zile ambazo kamati haijaziona ambazo wizara zinazohusika zimezipata.

Mhe. Spika, kamati inatoa maoni haya kutokana na ukweli kwamba ugatuzi kwa hapa kwetu ndio kwanza unaanza na tunapaswa kutoa mashirkiano ya hali ya juu ili tuweze kufanikiwa. Pia kamati inaishauri serikali kuwapa taaluma wahusika wote wa ugatuzi kwa kuwapeleka kwa wenzetu ambao wameanza zamani ugatuzi kwa lengo la kujifunza kama vile kwa nchi jirani za Kenya, Rwanda na Tanzania Bara. Kwa sasa Kamati hii ya Ustawi wa Jamii haitojihusisha tena na masuala yaliyogatuliwa katika afya na elimu na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ambayo mwenyekiti wake ni Mhe. Machano Othman Said tunaikabidhi rasmi. *(Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inatoa pongezi kwa wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya hasa wa vijijini ambao ni wachache, lakini wanafanyakazi kwa bidii zaidi. Pia tunavipongeza vitengo vya *TFDA*, Damu Salama na Kitengo cha Uti wa Mgongo yaani *neurosurgery* kwa ubunifu na uendelezaji mzuri wa majukumu yao. *(Makofi)*

Halikadhalika kazi nzuri inayofanywa na Bodi ya Chakula na Vipodozi inastahiki kupongezwa sana. Ni hivi majuzi tu wamepatiwa Shahada ya Ubora wa Kazi zake yaani *ISO*. *(Makofi)*

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni wizara ya pili inayosimamiwa na Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi katika utekelezaji wa kazi zake mbalimbali. Kamati ya Ustawi ilifanyakazi na Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali katika vipindi tofauti kama vilivyoanishwa katika utangulizi wa ripoti hii.

Mhe. Spika, katika vipindi hivyo Kamati ya Ustawi wa Jamii imefatilia utekelezaji wa Programu kuu na programu ndogo za wizara kwa mujibu wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Katika bajeti hiyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inasimamia programu kuu zifuatazo:-

1. PROGRAMU YAMAANDALIZI NA MSINGI
2. PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI
3. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU
4. PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

5. PROGRAMU YA ELIMU BORA
6. PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA

Mhe. Spika, idara, taasisi na vitengo mbalimbali vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali vinasimamia utekelezaji wa programu hizo kuu ambazo pia zinajumuisha na programu ndogo ndogo kwa mwaka wa fedha 2017/18. Kamati ya Ustawi wa Jamii imeyaweka masuala mbali mbali yaliyofanyiwa kazi kama yalivyotekelezwa kupitia programu kuu za hapo juu kama ifuatavyo:-

1. **PROGRAMU YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

Mhe. Spika, programu hii inahusu utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na moja. Katika kipindi kuanzia mwezi wa Julai, 2017 Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imegatua baadhi ya kazi zinazofanyika chini ya Programu hii na kuzipeleka katika Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 2014. Taarifa hii ya Kamati itafafanuwa utekelezaji wa kazi za ugatuzi, mafanikio na changamoto zake katika sekta ya elimu katika paragrafu zinazofuata hasa ikizingatiwa kwamba hii ni hatua ya mwanzo ya ugatuzi, ambapo wizara mama bado ina dhamana kubwa.

Mafanikio katika Utekelezaji wa Programu

Mhe. Spika, katika kupitia utekelezaji wa Programu hii yapo mafanikio makubwa yaliopatikana kama ifuatavyo:-

a. Kuondolewa kwa michango ya fedha kutoka kwa wazazi ambapo inaakisi sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar elimu bila malipo.

b. Ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi wa maandalizi na msingi baada ya kufutwa michango.
c. Ongezeko la kasi ya uimarishaji wa miundombinu ya kusomea kwa maandalizi na msingi. Yaani ujenzi wa madarasa mapya.
d. Kugatuliwa kwa baadhi ya huduma za elimu ya msingi na maandalizi na kupelekwa kwenye Serikali za Mitaa kama vile gharama za chakula kwa wanafunzi wa Skuli za Maandalizi (posho la uji), malipo ya nauli za walimu wanaosemesha maeneo ya mbali, kuhamasisha kazi za uandikishaji wanafunzi wa maandalizi na msingi, fedha za matengenezo madogo madogo ya Skuli za Maandalizi na Msingi na malipo ya posho za Maafisa wa Elimu wa Wilaya.

Changamoto katika Utekelezaji wa Programu

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo zipo changamoto kadhaa zinajitokeza kwa ujumla katika utekelezaji wa programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi kama ifuatavyo:-

a. Ongezeko kubwa la wanafunzi na uhaba wa madarasa katika skuli mbali mbali za Maandalizi na Msingi kwa Unguja na Pemba. Kamati ya Ustawi wa Jamii imeona baadhi ya skuli zina idadi kubwa ya wanafunzi katika darasa moja, kuanzia wanafunzi 80 mpaka 120. Kwa mfano, skuli ya Sizini, Wilaya ya Micheweni Pemba, na nyengine zikizidi mpaka wanafunzi 290 kwa darasa moja. Kwa mfano, Skuli ya Kinuni Wilaya ya Magharibi Unguja. Aidha, zipo skuli kadhaa zina uhaba au ukosefu wa madarasa ya maandalizi. *(Makofi)*

b. Uhaba wa walimu wa ngazi ya cheti na diploma katika Skuli za Maandalizi na Msingi; kamati imeona pamoja na wingi wa wanafunzi uliopo, walimu wenye uwezo wa

kufinyanga watoto kuanzia maandalizi. Kwa maana ya kufinyanga tunakusudia kuwasomesha ipasavyo watoto, kuanzia maandalizi na darasa la kwanza na kuendelea wapo wachache, walimu hawa ambao hupatiwa mafunzo maalumu ya kuanza kumuandaa mtoto kujuwa kusoma, kuandika na kuhesabu wameadimika.

Sasa moja ya sababu ambayo kamati imejulishwa na wahusika mbali mbali wa sekta ya elimu, ni kuondolewa kwa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti yaliyokuwa yakitolewa zamani na Chuo cha Ualimu Nkurumah, ambacho hivi sasa kimeunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). *(Makofi)*

c. Ukosefu wa vyoo kwa baadhi ya Skuli za Maandalizi na Msingi, kamati imepitia na kuona baadhi ya skuli zinakosa vyoo na watoto wanajisaidia kwenye maeno ya nje (vichakani/pwani). Kwa mfano, Skuli ya Tumbatu Gomani na Mjini Kiuyu Pemba. Aidha zipo na nyengine ambazo vyoo vipo lakini havitoshi na vina uhaba wa maji safi na salama. *(Makofi)*

d. Wingi wa masomo wanayosomeshwa wanafunzi wa ngazi ya msingi; kamati imepata malalamiko kutoka kwa wahusika mbalimbali wa elimu kuwa wanafunzi wa msingi wanasomeshwa masomo mengi wakiwa wadogo. Hivyo, kuna uwezekano wa kutopatikana matokeo mazuri. Hapo zamani mkazo ulikuwa kwenye masomo ya Kingereza, Kiswahili na kuhesabu.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hizo kamati imeelekeza yafuatayo:-

a. Kamati inashauri kurejeshwa ajira za walimu wa cheti makhususi kwa kukidhi upungufu kwenye madarasa ya chini.
b. Kamati inashauri serikali ivirejesha tena Vyuo vya Ualimu kama ilivyo kwa nchi za jirani mfanoTanzania Bara ambapo vyuo hivyo bado vipo na vinasomesha taaluma ya elimu (*profession*) na siyo utaalamu wa elimu (*academic*). Mbali ya kuwepo Vyuo Vikuu kadhaaTanzania Bara. Lakini Vyuo vya Ualimu bado vinaendelea kama Kigurunyembe (Tabora), Chang'ombe (Dar-es-Salaam) na Butimba (Mwanza).
c. Kamati inaishauri wizara kuharakisha kumaliza madarasa yaliyoanzwa kwa nguvu za wananchi, vilevile kuongezwa madarasa ya msingi na ujenzi wa skuli mpya katika maeneo ambayo kuna wanafunzi wengi.
d. Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika ihakikishe inafanya ukaguzi wa Skuli za Maandalizi za kila Wilaya kuhakikisha kuwa huduma za vyoo, maji safi na salama zinakuwepo muda wote.
e. Sera ya Elimu imefika wakati ifanyiwe mapitio kwa kushirikisha wahusika na wataalamu wa ngazi mbali mbali za sekta ya elimu na kuweka mpango wa masomo ambayo mwanafunzi wa maandalizi na msingi anayamudu vizuri.
f. Kamati inaagiza kuwe na mpango wa ufuatiliaji wa karibu wa maendeleo ya elimu ya maandalizi na msingi kuhakikisha wanafunzi wanaoanza waweze kujuwa kusoma, kuandika na kuhesabu kama sera ya elimu inavyoelekeza, wenyewe wanasema *three R. (Makofi*)

2. **PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI**

Mhe. Spika, Programu hii inahusu usimamizi wa elimu ya sekondari kwa vijana wenye umri kati ya miaka 12 hadi 17.

Kamati imepitia na kukaguwa kazi mbalimbali zinazofanyika kupitia programu hii ya elimu ya sekondari.

Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari kamati imeona mafanikio yafuatayo:-

a. Kuimarishwa kwa miundombinu ya majengo ya Skuli za Sekondari katika Wilaya zote za Zanzibar. Tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulifanikisha hili hasa ukitilia maanani ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoingia sekondari kama vile ilivyoagiza sera ya elimu.
b. Walimu wanaendelea kutekeleza wajibu wao wa kusomesha licha changamoto kadhaa zinazowakabili. Kwa hili tunawapongeza sana walimu kwa kufanyakazi kwa bidii ndani ya mazingira magumu. *(Makofi)*

Changamoto za Utekelezaji wa Programu

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo, kamati imebaini changamoto zinazokabili utekelezaji wa programu ya elimu ya sekondari kama ifuatavyo:-

1. Matokeo yasiyoridhisha ya Mitihani ya Kitaifa

Mhe. Spika, hali hii ya matokeo yasiyoridhisha imekuwa ikijitokeza kila mwaka kwa wanafunzi wa kidato cha nne na kidato cha sita. Kamati inatambuwa jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kutatuwa changamoto hii. Katika ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka jana, yaani Febuari 2017, kamati imeeleza kwa urefu changamoto hii na kutoa ushauri kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa za kuitatuwa changamoto hiyo. Hata hivyo, kamati

inaendelea kushauri hatua endelevu za kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto hiyo.

2. Changamoto Maghususi kwa Skuli za Sekondari Zanzibar

Mhe. Spika, zipo changamoto tumezibaini maghususi katika Skuli za Sekondari zilizotembelewa na kamati ambazo ni hizi zifuatazo:-

Mhe. Spika: Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii), kumradhi. Naomba nimpishe Mhe. Mwenyekiti, halafu baadae utaendelea. Mhe. Mwenyekiti, naomba uje.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii) endelea.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii):

2. Changamoto Maghususi kwa Skuli za Sekondari Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, zipo changamoto tumezibaini maghususi katika Skuli za Sekondari zilizotembelewa na kamati ambazo ni hizi zifuatazo:-

i. Uvamizi wa maeneo ya Skuli ya Muanda; kamati imefahamishwa kuwa kuna mwananchi amevamia eneo la Skuli hiyo eneo ambalo ni mali ya Serikali.
ii. Ukosefu wa gesi katika maabara za Skuli ya Muanda, Chasasa na Utaani. Aidha, tatizo hili litazamwe kwa skuli nyengine kadhaa za sekondari ambazo kamati haijazifikia.

Tumejulishwa kuwa gesi katika Skuli ya Muanda ilikuwepo kwa miezi sita ya mwanzo tu baada ya kufunguliwa rasmi skuli hiyo, baadae imetoweka moja kwa moja mpaka hii leo.

iii. Tatizo la uhalifu katika maeneo ya Skuli ya Faraja; kamati imepatiwa taarifa ya vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na baadhi ya vijana wa maeneo ya Skuli ya Faraja vijana hao wanaharibu mazingira ya skuli kwa kuchimba mchanga wakiwa na gari za punda na ng'ombe na wanapozuiliwa hutumia silaha za kienyeji kujihami. Aidha, vijana hao wanawaibia wanafunzi na kuwajeruhi kwa silaha za kienyeji kama mapanga na pauro, yapo matukio ya kushambuliwa wanafunzi yamejitokeza.

iv. Ukosefu wa dakhalia katika skuli za sekondari angalau kwa Kidato cha Tatu, Kidato cha Nne, Kidato cha Tano na Kidato cha Sita.

v. Uhaba wa walimu wa sayansi na hisabati.

vi. Malimbikizo ya madai ya walimu hasa wanaopanda vyeo kutolipwa mishahara mipya wanayostahiki kwa wakati na pale wanapoanza kulipwa basi malimbikizo yao yanachukuwa muda mrefu kumalizwa.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya matokeo yasiyoridhisha ya mitihani ya kitaifa, kamati inapendekeza yafuatayo:-

a. Kuimarishwa elimu ya Maandalizi na Msingi kwa kuweka mazingira mazuri ya wanafunzi kusomeshwa kwa kuwa huko ndiko kwenye matayarisho ya wanafunzi kufanya vizuri baadaye.

b. Kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu katika ngazi zote na kuwawekea walimu mazingira mazuri ya kusomesha.
c. Walimu kutekeleza wajibu wao wa kufundisha na wizara iweke mikakati maalumu na endelevu ya kuhakikisha kuwa walimu wanatekeleza wajibu wao huo kama inavyopasa. Wale ambao hawatimizi wajibu wao basi hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao.
d. Ukaguzi wa walimu uimarishwe kubaini walimu wasiotimiza wajibu wao ipasavyo na hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yao kama nilivyosema.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hatua hizo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaendelea kuishauri serikali kukabiliana na changamoto ya matokeo yasiyoridhisha kwa kuchukuwa hatua zaidi zifuatazo:-

a. Kujenga dakhalia na maabara za kufundishia; kamati imefahamishwa kuwa skuli za nyingi zinazofanya vizuri Tanzania Bara na kwengineko, katika mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne na sita zimewekewa miundombinu mizuri ya kufundishia, kama vile dakhalia ambazo zinawaweka wanafunzi pamoja katika mazingira ya utulivu yasiyokuwa na shinikizo na changamoto za kijamii. Kamati, inatambuwa kuwa jambo hili linawezekana kupitia mipango mbali mbali ya serikali kama vile ilivyowezekana kupitia miradi ya ujenzi wa skuli za mpya katika kila wilaya, kupitia ufadhili wa wahisani wa maendeleo.

b. Kuhakikisha vifaa vya kufundishia kama vile vitabu na vifaa vya maabara vinapatikana kwa wakati. Kamati katika kutembelea baadhi ya skuli imegundua kuwa vifaa hivyo hasa vya maabara hupatikana miezi mitatu tu kabla ya wanafunzi hawajafanya mitihani yao, hali hiyo haiwezi

kuleta mtokeo mazuri kwa vile mwanafunzi hapati muda wa kutosha wa kujifunza kwa vitendo.

c. Mkakati wa kuajiri walimu wa fani mbalimbali uwe endelevu, kwasababu sikuzote wapo walimu wanaostaafu. Walimu kujengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo na mbinu mpya za ufundishaji kupitia vituo vya walimu, aidha kuwawekea mazingira mazuri yasiyokuwa na shinikizo kama vile usafiri au nauli zinazokidhi masafa wanayosafiri.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuandaa mkutano wa kila mwaka wa siku tatu wa mapitio ya wizara yao. Mkutano huo umeanza jana tarehe 19 Februari, 2018 na unaendelea mpaka kesho tarehe 21 Februari, 2018. Kwakweli, mkutano huo ni muhimu na unafanya mapitio ya utendaji wa Sekta ya Elimu. Mkutano huo ulioanza jana unawashirikisha washirika wa maendeleo, sekta binafsi, Wakuu wa Wilaya, wazee pamoja na wanafunzi. Kamati inamshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuialika Kamati ya Ustawi wa Jamii kushiriki kikamilifu katika mkutano huo.

3. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Elimu ya Juu inahusu uratibu wa elimu ya juu, huduma za mikopo ya elimu ya juu, huduma za sayansi na teknolojia na huduma ya elimu ya juu, ushauri na utafiti.

Mafanikio katika Utekelezaji wa Programu

Katika utekelezaji wa programu hii Kamati imeona kuna mafanikio kadhaa muhimu yamepatikana kama ifuatavyo:-

a. Huduma ya utoaji mikopo ya elimu ya juu kwa wanafuzi wapya na wazamani imefanyika, jumla ya wanafunzi wapya 1,461 wamefungishwa mikataba ya mkopo kwa mwaka 2017/18. Aidha wanafunzi 2,582 wanaondelea wamefanyiwa malipo ya muhula wa kwanza wa ada ya mitihani na masomo.
b. Kazi za uratibu wa wanafunzi wanaopatiwa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi zimefanyika.
c. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kinaendelea kutekeleza kazi zake za kutoa elimu ya Juu katika fani mbali mbali hasa baada ya kuunganisha vyuo vya Afya, Fedha na Utalii. Tunakipongeza Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kwa kukamilisha ukumbi mpya wa shughuli za mbali mbali (*multi purpose Hall*), ukumbi huu umepewa jina la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi *Dkt. Ali Mohamed Shein Hall*.
d. Mahafali ya 13 ya *SUZA* yaliyofanyika tarehe 15/02/2018 katika Kampasi ya Tunguu, Mkuu wa Chuo, *Chancellor* Dkt. Ali Mohamed Shein amewatunuku wahitimu saba (7) wa shahada ya Uzamili wa Sayansi ya Kemia (*MSc. Chemistry*), amewatunuku wahitimu watatu (3) wa shahada ya uzamili ya Sayansi ya Mazingira 2016/17 (*Msc. Enviromental Science*), pia amewatunuku wahitimu kumi na moja (11) wa shahada ya Uzamili ya Sanaa ya Kiswahili 2016/17 (*Phd*. Kiswahili).

   Mhe. Mwenyekiti, hakika haya ni mafanikio makubwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) na kwa nchi nzima kwa ujumla. Kwahiyo, tunaupongeza uongozi wa chuo kwa kazi nzuri. *(Makofi)*
e. Maendeleo ya Ujenzi wa Jengo la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (*KIST*) Mbweni ambapo jengo lipo katika hatua nzuri ya kukamilika.

Changamoto za Utekelezaji wa Programu

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo kamati imebaini baadhi ya changamoto zinazokabili utekelezaji wa programu kama ifuatavyo:-

a. *Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu*

i. Kusitishwa Mikopo ya elimu ya juu kwa wafanyakazi wa serikali wanaojiendeleza.

ii. Uchelewaji wa kutumiwa fedha kwa baadhi ya wanafunzi hasa wa vyuo vya nje ya Zanzibar.

iii. Tatizo la ufinyu wa jengo la Ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; Kamati bado inaripoti tena hali hiyo ya ufinyu wa jengo la Ofisi za Bodi ya Mikopo kwa nia ya kuikumbusha Wizara kuchukuwa hatua ya kujenga lao makhususi kwa Bodi ya Mikopo hapo Mazizini nyuma ya Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

b. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(SUZA)*

i. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (*SUZA*) hakipatiwi fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi mbalimbali ya chuo hicho ambayo inasuasua kutokana na ukosefu wa fedha mfano miradi ya uimarishaji wa miundombinu ya majengo.

ii. Kuna tatizo kubwa la uvamizi wa maeneo ya ardhi ya *SUZA* katika kampasi zake mbali mbali Unguja na Pemba, tatizo hili linaelekea kuwa kubwa hivi sasa. Kamati imeona na kuelezwa maeneo ya ardhi yaliyovamiwa katika Kampasi ya Mbweni (Skuli ya Afya), Kampasi ya Nkurumah, Mchangamdogo, Tunguu na Maruhubi (Taasisi ya Utalii). Maeneo hayo yamevamiwa na wananchi kwa kujengwa nyumba za makaazi, shughuli za biashara na kilimo.

iii. Changamoto ya Vyuo vilivyounganishwa na kukosa fedha za Matumizi kwa ajili uendeshaji wa kazi zake mbali mbali, hapo awali kabla ya kuunganishwa vyuo hivyo vilikuwa vikipata fedha hizo kupitia taasisi zao. Vyuo vyenyewe ni Chuo cha Afya Mbweni, Chuo cha Utalii cha Maruhubi na Taasisi ya Uongozi na Usimamizi wa Fedha Chwaka. Hatahivyo, baada ya vyuo hivyo kuunganishwa na *SUZA* fedha hizo hazipatikani tena wala *SUZA* haipatiwi fedha hizo.changamoto hii inaipa mzigo wa bajeti *SUZA* wa kuvihudumia vyuo hivyo wakati mwengine huduma zinachelewa.

iv. Athari za Kimazingira kwa Taasisi ya Utalii ya Maruhubi; Kamati imeona athari ya kimazingira ya kupanda kwa maji ya bahari katika eneo la Taasisi, kamati imefahamishwa kuwa tatizo hilo huenda limetokana na ujenzi wa mradi wa hoteli unaoendelea jirani na Taasisi hiyo, mradi ambao unahusisha kufukiwa kwa sehemu ya bahari mkabala na eneo hilo.

c. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume *(KIST)*

i. Uhaba wa walimu wa masomo ya ufundi hasa wa ngazi ya shahada ya Uzamivu (*PhD*) ambao waliopo wanahitaji kuendelezwa kufikia ngazi hiyo.

ii. Kutopatikana kwa ufumbuzi wa tatizo la matumizi ya umeme wa jua baina ya Taasisi ya Karume na Shirika la Umeme (*ZECO*), licha ya kuchukuliwa hatua kadhaa za kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala hilo bado hatua hizo hazijazaa matunda na mvutano bado unaendelea.

d. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)*

i. Kupanda kwa viwango vya mikato vya Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu ya Tanzania kutoka 8% mpaka 15% ya mshahara, ambayo inaathiri wahitimu wa Zanzibar walioajiriwa. Viwango hivyo haviendani na viwango vya mishahara kwa wanafunzi wanaoajiriwa Upande wa Zanzibar ambao mishahara yao hailingani na wenzao wa Jamhuri ya Muungano.

ii. Kutozingatiwa baadhi ya masomo ya lugha na dini ya kidato cha sita kuwa ni sehemu ya sifa (*credits*) za kumuwezesha mwanafunzi kuendelea na masomo yake elimu ya juu. Changamoto hii inaathiri sana wanafunzi kutoka Zanzibar.

iii. Mabadiliko ya mfumo wa udahili wa wanafunzi kwa njia ya mtandao yameathiri idadi kubwa ya wanafunzi kuchelewa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu kwa vile wengi wao hawakuwa na matayarisho ya mabadiliko hayo.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo Kamati ya Ustawi wa Jamii inaelekeza yafuatayo:-

a) Serikali itafakari tena hatua yake ya kusitisha mikopo kwa wafanyakazi wa serikali. Kamati imeona kuwa zipo kada muhimu za wataalamu ambazo zinahitajika ambazo wafanyakazi wa serikali wanahitaji kujiendeleza na uwezo wa kujisomesha hawana, mfano walimu wa fani za ufundi katika ngazi ya shahada ya uzamivu. Madaktari, wahandisi wa vifaa tiba ambavyo vimeshakuwepo katika hospitali za serikali, wataalamu wa ujenzi, mafuta na gesi asilia na kadhalika. Aidha, kamati inashauri kuwa serikali iweke

kada adimu kwa kasma maalumu ambayo itawezesha wafanyakazi wa serikali kujiendeleza kwa kupatiwa mikopo.

b) Fedha za mikopo zitolewe mapema kwa wanufaika hasa kwa wanafunzi waliopo nje ya Zanzibar ambao wanaathrika sana na ucheleweshaji wa mikopo hiyo.
c) Kamati inashauri serikali kutafuta jengo la kutosha kwa ajili ya ofisi za Bodi ya Mikopo ya Elimu Zanzibar, jengo linalotumika hivi sasa ni finyu na halitoshi kwa kazi za ofisi.
d) Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuisaidia *SUZA* kupata fedha za maendeleo na matumizi mengineyo ili iweze kumudu uendeshaji wa Vyuo na Taasisi zinazoongezwa kwa ufanisi.
e) Kamati inaiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa Waraka maalumu kuhusu uvamizi wa maeneo ya ardhi za *SUZA* na kupeleka Serikalini kwa maamuzi na hatua za haraka za kudhibiti ili hali hiyo isiendelee.
f) Kamati inaishauri Serikali kupitia Idara ya Mazingira kufanya upya tathmini ya athari ya kimazingira katika eneo la Taasisi ya Utalii ya Maruhubi, ili hali ya kupanda kwa maji ya bahari katika eneo la Taasisi hiyo lipatiwe ufumbuzi.
g) Kamati inashauri Serikali kusaidia kusomesha walimu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (*KIST*) katika ngazi ya shahada ya uzamivu ili chuo hicho kiweze kutoa taaluma za ufundi kwa vijana wetu katika ngazi ya shahada.
h) Mvutano baina ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (*KIST*) na Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) kuhusu matumizi ya umeme wa jua upatiwe ufumbuzi na serikali kuu kwa vile mpaka hivi sasa taasisi hizo zenyewe zimeshindwa kupata ufumbuzi wa kudumu.

i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar ifanye mazungumzo na wenzao wa Tanzania bara kuhusu ongezeko la kima cha mikato kwa wanufaika wa Zanzibar kutoka 8% hadi 15% ambacho kimelalamikiwa na waajiriwa hasa katika kada ya ualimu kuwa ni kikubwa na hakikuzingatia viwango vya mishahara ya waajiriwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
j) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ifanye mazungumzo na Kamisheni ya Vyuo Vikuu/*NACTE* kuhusu kuzingatia 'credit' za masomo ya lugha ya kiarabu na dini ambayo kuna baadhi ya fani zinatumia masomo hayo mfano utalii katika fani ya ukarimu *(hospitality)*.
k) Wizara iweke utaratibu utakaowezesha wanafunzi kupata taarifa kwa haraka na kufahamishwa taratibu mpya za udahili ili wasichelewe kufanya maombi ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

4. PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, programu hii muhimu imelenga kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa wanafunzi kulinga na mahitaji ya soko la ajira, kupunguza idadi ya wasiojuwa kusoma na kuandika na kuwawezesha vijana kitaaluma ili waweze kujiajiri.

Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu

a) Kuimarishwa kwa miundombinu ya majengo ya Vyuo vya Amali; ujenzi wa chuo cha amali cha Makunduchi umefikia asilimia 25 na ujenzi wa chuo cha Utalii cha Maruhubi umefikia asilimia 65. Aidha uzio wa senyenge katika dakhalia ya wanawake ya Kituo cha Amali cha Vitongoji unakamilishwa pamoja na ukarabati wa dakhalia za Mkokotoni na Vitongoji.

b) Kazi nyengine mbali mbali za utendaji na uendeshaji zimefanyika kama vile utoaji wa huduma za chakula mara tatu kwa siku kwa wanafunzi wa Kituo cha Mkokotoni na Vitongoji; kuandaa miongozo kwa miradi ya maendeleo ya vyuo binafsi Unguja na Pemba; kufanya mafunzo ya ujasiriamali na stadi za kazi; kuandaa vikao vya Bodi, kuandikisha wanafunzi wa Madarasa ya Elimu Mbadala na vituo vya kujiendeleza.

Changamoto katika Utekelezaji wa Programu

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo kamati imeona changamoto zifuatazo:-

a) Ujenzi wa Chuo cha Amali cha Daya Mtambwe hauridhishi hata kidogo na muda wa ujenzi tayari umemalizika; kamati imeona na kubaini kuwa kuna hali ya kutoelewana baina ya Mjenzi na Mshauri elekezi ambaye hayupo katika eneo la ujenzi na badala yake ameweka Msimamizi wake ambaye hana maamuzi. Maamuzi yanatoka Makao Makuu ya Mshauri huyo yaliyopo Khartoum-Sudan. Hali hiyo imepelekea mjenzi kuanza kazi ya msingi bila maelekezo ya Mshauri elekezi, hatua iliyopelekea msingi huo kuambiwa haufai.
b) Ujenzi wa Chuo cha Amali cha Makunduchi nao ingawa unaendelea lakini hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni asilimia 25 tu huku muda ukiwa unamalizika na Mshauri elekezi ni huyo huyo wa mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Amali Daya Mtambwe.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hayo kamati inaelekeza yafuatayo:-

a) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itazame tena Mkataba wake na Mshauri ekelezi wa Mradi wa chuo cha amali cha Daya Mtambwe na Makunduchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchukuwa hatua stahiki, kwa vile inaonekana Mshauri huyo hafanyi wajibu wake inavyopaswa na kupekelea kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo.
b) Wizara ya Elimu iweke utaratibu wa kuwa karibu na Washauri ekelezi wa miradi yake ya ujenzi na kuhakikisha kuwa wanafanya majukumu yao kwa Maslahi ya Wizara kama ilivyo katika mkataba.

5. PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, programu hii muhimu madhumuni yake ni kuwezesha kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu. Kamati imefuatilia masuala kadhaa yanayohusu utekelezaji wa Programu ya Ubora wa Elimu.

Mafanikio katika Utekelezaji wa Programu

a) Kazi mbalimbali zimefanyika katika utekelezaji wa programu hii kama vile uimarishaji wa miongozo ya kuendesha paneli za kitaifa za mitaala, tathmni ya vitabu na vifaa vya kufundishia, kuchapisha mitihani, kuandaa viwango vya ukaguzi wa elimu, kutoa ushauri katika uanzishaji wa maktaba za skuli na jamii, kuanda mafunzo mbalimbali yanayohusu elimu ya UKIMWI na afya ya uzazi, TEHAMA, elimu mjumuisho, nukta nundu na mafunzo ya walimu wa maandalizi.
b) Kufuatilia na kuchukuwa hatua kuhusu kesi za udhalilishaji, ndoa na ujauzito na kuzitafutia ufumbuzi kwa mujibu wa sheria.

c) Upatikanaji wa fedha katika vituo vya walimu (*TCs*) umeanza, ingawa unahitaji kuendelezwa kwa vituo vyote.

Changamoto zinazokabili utekelezaji wa Programu

a) Kukosekana kwa muongozo wa kisheria kuhusu ukaguzi wa elimu ambao ungeweka masharti ya kisheria pamoja na kanuni.
b) Ukosefu wa Maktaba kwa baadhi ya Skuli sambamba na uhaba wa wakutubi wenye sifa kwa skuli zenye maktaba.
c) Skuli nyingi zina uhaba wa Wataalamu wa Maabara wenye sifa.
d) Uchakavu wa haraka uliobainika katika Skuli ya Faraja, Madungu Sekondari na Muanda n.k

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo kamati inaelekeza yafuatayo:-

a) Sheria ya Ukaguzi wa Elimu inahitajika, ili kuweka miongozo ya kisheria na kikanuni itakayosimamia ukaguzi wa elimu.
b) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikana na Shirika la Huduma za Maktaba ifanye tathmini ya skuli ambazo hazina maktaba ili kufanya mpango wa kufikisha huduma hiyo katika Skuli hizo. Aidha wakutubi wenye sifa waajiriwe, ili kukabiliana na upungufu wa watendaji hao.
c) Wataalamu wa Maabara wenye sifa waajiriwe, ili kukabiliana na uhaba mkubwa wataalamu hao katika Skuli nyingi za Serikali.

6. PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inajumuisha utekelezaji wa kazi za Uongozi, Mipango, Sera na Utafiti na shughuli za uratibu wa elimu kwa upande wa Pemba.

Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu

a) Hatua za Kuifanyia marekebisho sera ya elimu mwaka 2006 zimeanza kuchukuliwa kwa kukusanya maoni ya wahusika mbali mbali katika sekta elimu.
b) Mpango Mkuu wa Elimu (2017/18-2021/22) umewasilishwa kwa wahusika mbalimbali wa sekta ya elimu wakiwemo maafisa wanaoshughulikia maendeleo ya elimu katika Serikali za Mitaa.
c) Posho na stahiki mbali mbali za walimu zimelipwa ingawa kwa kiwango kidogo sana.

Changamoto katika Utekelezaji wa Programu

a) Tatizo kubwa la Uhaba wa Walimu wa fani mbali mbali kuanzia msingi hadi sekondari. Tatizo hili ni kubwa hasa kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi, wimbi kubwa la kustaafu walimu wa zamani na wengine kufariki. Sambamba na hilo kasi ya uajiri haiendani na mahitaji halisi ya idadi ya walimu wa kuziba upungufu huo.
b) Kuna changamoto katika mfumo wa uajiri hasa kwenye sekta ya elimu ambapo mahitaji ni makubwa ya walimu, walimu wenye sifa wapo kwenye soko, mchakato wa ajira unakwenda taratibu na unachukuwa muda mrefu kukamilika kiasi ya kuwafanya walimu wengi kuondoka Zanzibar kwenda kutafuta kazi Tanzania Bara na kwengineko.
c) Sambamba na hilo kuna idadi kubwa ya walimu wa kujitolea hasa upande wa Pemba ambao hawajaajiriwa wengine ni wakaazi wa maeneo wanayofanyia kazi.

Ingawa kujitolea si kigezo cha kuajiriwa lakini lazima serikali izingatie baadhi ya Walimu kama Skuli ya Sekondari ya Utaani kuna mwalimu mmoja wa lugha ya Kiarabu ambae anasomesha kwa kujitolea huu mwaka wa pili.

d) Kuna changamoto ya uhamisho wa mara kwa mara wa walimu ambao unawachanganya wanafunzi, aidha kwa upande wa Pemba wapo walimu wambao wanaomba ajira Pemba na baada ya kuajiriwa wanaomba uhamisho kurudi Unguja kwa visingizio mbali mbali kama vile ndoa na familia.

e) Yapo madai ya walimu kuhusu stahiki zao mbali mbali hayajalipwa kama vile posho za likizo, viwango vidogo vya nauli, masawazisho ya mishahara kwa walimu wapya na wazamani nk. Tumelieleza sana suala hili katika ripoti za nyuma lakina hakuna mafanikio. Kamati inamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kulitolea agizo suala hili karibuni katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama Cha Walimu. (*Makofi*)

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Mhe. Spika, Kutokana na changamoto hizo Kamati inaelekeza kama iafuatavyo:-

a) Kamati inaishauri serikali kuona umuhimu wa kuwa na Tume ya Utumishi ya Walimu kwa kushughulikia masuala yote walimu ikiwemo tatizo kubwa la ajira ya walimu, matatizo ya kiutumishi ya walimu kwa upekee na wingi wake, mahitaji halisi ya upungufu na ujazaji wa nafasi zilizo wazi.

   Kamati inasisitiza umuhimu wa Tume ya Utumishi ya Walimu kwa kuwa ni mfumo ambao unatumika katika nchi nyingi za Afrika Mashariki na duniani na unasaidia kutatuwa changamoto nyingi za kiutumishi na ajira za

walimu ambazo kwa Tume ya Utumishi ya Serikali peke yake hazimudu kwa ufanisi unaotakiwa hasa kasi ya kutatua matatizo ya maslahi ya walimu.

b) Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kuwa uhamisho wa walimu unafanyika kwa mpango bila kuleta athari katika maendeleo ya masomo ya wanafunzi.

UGATUZI KATIKA SEKTA YA ELIMU

Hili tumelizungumza kama utangulizi na pia kwa upande wa afya tumezungumza kwa undani zaidi lakini nataka kusema kwa ufupi tu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ugatuzi uliofanyika ulikuwa katika gharama za chakula kwa wanafunzi wa skuli za maandalizi, yaani posho la uji.

Malipo ya Nauli za Walimu Wanaosomesha Maeneo ya Mbali

Mhe. Spika, mnamo mwezi Julai mwaka 2016 serikali ilianza rasmi kutekeleza sera ya ugatuzi wa huduma za elimu ya Maandalizi na Msingi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kamati ya Ustawi wa Jamii imepata fursa ya kupitia shughuli za elimu utekelezaji huo katika hatua za awali kwa kutembelea Serikali za Mitaa Unguja na Pemba ambazo zimepelekewa utekelezaji wa huduma hizo. Lengo kubwa kuona maendeleo ya elimu baada ya hatua za awali za ugatuzi.

Mhe. Mwenyekiti, huduma zilizogatuliwa ni elimu ya Maandalizi na Msingi katika maeneo yafuatayo:-

- Gharama za chakula kwa wanafunzi wa Skuli za Maandalizi (posho la uji)
- Malipo ya nauli za walimu wanaosemesha maeneo ya mbali.

- Kuhamasisha kazi za uandikishaji wanafunzi wa maandalizi na msingi.
- Fedha za matengenezo madogo madogo ya Skuli za Maandalizi na Msingi.
- Malipo ya posho za Maafisa wa Elimu wa Wilaya.
-

Mambo ambayo Hayajagatuliwa na Inafaa Kuzingatiwa kwa Makini:-

- Uajiri wa wafanyakazi bado unasimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
- Mishahara ya watendaji bado inalipwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
- Sera, miongozo, mikakati, vifaa vya kufundishia bado vinaendelea kusimamiwa na Wizara.
- Kurugenzi ya Elimu ya Maandalizi na Msingi bado ipo Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Mkurugenzi wake.

Mafanikio yaliyoanza kifikiwa katika muda huo mfupi

Kamati imeona mafaniko ya hatua ya Serikali kugatuwa huduma za elimu za Maandalizi na Msingi kwa Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

a. Utekelezaji umeanza licha ya changamoto zinazoikabili.
b. Changamoto za huduma za msingi za elimu zimeanza kushughulikiwa kwa haraka kupitia Serikali za Mitaa.
c. Urasimu wa upatikanaji wa huduma na fedha umeanza kupungua kwavile matumizi ya fedha hizo yanakwenda moja kwa moja kwenye Serikali za Mitaa.
d. Serikali kuu imeanza kupunguza mzigo wa majukumu ya ngazi ya msingi kupitia Serikali za Mitaa.

Changamoto za Ugatuzi kwa Sekta ye Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, changamoto zilizobainika na kamati katika utekelezaji ni hizi zifuatazo:-

a. Kumekosekana miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za elimu zilizogatuliwa; kamati imebaini kuwa baadhi ya kazi zinafanyika kila mtu na upande wake na matokeo yake hakuna *"uniformity"*. Vilevile, hakuna mpango wa makabidhiano na maelekezo ya namna ya kusimamia huduma zilizogatuliwa kutoka zilipokuwepo kwenda Serikali za Mitaa.
b. Kumekosekana ufahamu wa kutosha wa dhana ya ugatuzi kwa baadhi ya watendaji wa Serikali za Mitaa na Sekta ya Elimu; Kamati imebaini baadhi ya huduma zilizogatuliwa zinapata changamoto kutokana na baadhi ya watendaji wa Sekta ya Elimu kuendelea kuhodhi baadhi ya nyenzo za utendaji kazi kwa mfano vyombo vya usafiri na mafaili ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, sababu zipo mpaka h lakini pia Waheshimiwa Wajumbe wanaweza kuzisoma katika ripoti zeo.

c. Mawasiliano yasiyotosheleza baina ya Watendaji wa Serikali za Mitaa wenyewe kwa wenyewe na Watendaji wa Sekta ya Elimu. Kamati imebaini baadhi ya Walimu wamepewa uhamisho kutoka Pemba kwenda maeneo mengine muda mfupi baada ya kuripoti vituoni mwao. Aidha, baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zimeifahamisha Kamati kuwa kumekuwa hakuna vikao vya kuratibu utendaji kazi wa huduma zilizogatuliwa na Watendaji wa Wizara ya Elimu.
d. Kutoshirikishwa na kutambuliwa kwa baadhi ya Madiwani katika maeneo ya Serikali za Mitaa ambako huduma za ugatuzi zinahitaji kufuatiliwa na kusimamiwa.

e. Madiwani na baadhi ya Watendaji wa Serikali za Mitaa kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Elimu ya Jamii na Mazingira na Sheria za Mfuko wa Jimbo ambazo zinahusiana moja kwa moja na kazi na uwezo wa kufanya majukumu yao, yakiwemo ya ugatuzi, kwa uhakika na kujiamini zaidi.
f. Madiwani hawana nyenzo za kufanyia kazi hasa baaada ya maeneo ya Wadi zao kuongezeka sambamba na huduma zilizogatuliwa, mfano wa nyenzo hizo ni vyombo vya usafiri kuwawezesha kufatilia majukumu hayo.
g. Uhaba wa nafasi za kufanyakazi kwa baadhi ya Ofisi za Wilaya ambako masuala ya Ugatuzi yanaratibiwa, mfano Ofisi ya Wilaya ya Wete haina nafasi ya kutosha kwa kazi za Ugatuzi.
h. Changamoto ya kuzigawa kwenye ugatuzi baadhi ya Skuli za Maandalizi na Msingi zinazojumuishwa pamoja na Skuli za Maandalizi, Msingi na Kati mfano Skuli ya Kidagoni ya Kaskazini Unguja na nyengine kadhaa mfano wa Skuli hiyo.

MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto hizo kamati ineleza yafuatayo:-

a) Serikali ikamilishe miongozo ya utekelezaji wa ugatuzi ili kuondoa changamoto zinazokabili hivi sasa kutokana na kukosekana kwa miongozo hiyo. Kamati, imefahamishwa kuwa Kamati Maalumu imeundwa na serikali kutayarisha miongozo hiyo, hivyo Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri Miongozo hiyo ikamilishwe haraka, ili ianze hatua ya utekelezaji kwa ufanisi.
b) Changamoto ya kuzigawa za Skuli za Maandalizi, Msingi na Kati, ambazo zinakuwa pamoja, Kamati inashauri kuwa wizara ishirikiane na Serikali za Mitaa husika kuona

namna ya kutekeleza kazi za ugatuzi katika skuli za aina hiyo.

c) Elimu kuhusu dhana ya ugatuzi, madhumuni yake na matarajio ya Serikali iendelee kutolewa kwa wahusika mbali mbali kwa sekta zote zilizogatuliwa hasa ya Elimu.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti. katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na sheria nyenginezo, kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya serikali kupitia Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa taratibu yanapewa kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti**.** kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na kamati kwa wizara hizo yatazingatiwa na kufanyiwa kazi kwa lengo la kutoa huduma nzuri kwa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwanza kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia kamati katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti. kamati imefanyakazi zake kwa mashirikiano makubwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya, kuanzia Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Naibu Waziri wote wawili, Matibu Wkuu na Manaibu Makatibu Wakuu

wote, Maafisa Wadhamini, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Vitengo, Maafisa na Watendaji wa ngazi zote walitoa ushirikiano kwa Kamati kwa lengo la kusaidia kufanikisha utekelezaji wa huduma za afya na elimu kwa wananchi. Kamati inawashukuru wote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, shukurani za pekee kabisa kwa wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Makatibu wa Kamati ambao majina yao nimetangulia kuyataja awali, kwa kazi kubwa ya kufika kila panapowezekana Unguja na Pemba kufanyakazi za kusaidiana na wizara zinazosimamiwa na kamati, na kwa upekee kabisa kamati itoa shukurani kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Divisheni ya Taarifa Rasmi za Baraza kwa kusaidia matayarisho na hatimaye kuchapishwa kwa ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti**,** nakushukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini kabisa ahsanteni sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Asante Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii). Sasa Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tuendelea na taratibu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nasimama kwa kutumia Kanuni ya 42 pia na kuikazia Kanuni ya 27. Mhe. Mwenyekiti, jana baada ya kipindi cha maswali na majibu Mhe. Mohammed Said Mohammed alileta hoja hapa kuhusiana na uhaba wa mafuta unaoendelea ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Mhe. Waziri mwenye dhamana alikiri na alisema

kuwa hana tarifa za kutosha na atatujuilisha chombo hichi, ambacho rasmi cha wananchi tupate taarifa rasmi.

Mhe. Mweyekiti, yameshapita masaa zaidi ya 24 kipindi cha maswali na majibu yamepita tunaendele sasa kuchangia hoja hii lakini hadi hivi sasa serikali haijaleta majibu rasmi juu ya masuala ya mafuta. Je, uhaba huu utaendelea au upo au unakwenda kwa kiwango gani sasa tunataka kuelewa. Kwahiyo, je serikali inahitaji masaa, siku, wiki au muda gani ili na sisi pia tuwe na majibu rasmi kwa wananchi wetu Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Mhe. Mjumbe nimekusikia na serikali ipo imesikia na ikiwa tayari itaweza kutoa majibu ambayo kuwa yanastahiki haiwezi ikakurupuka lazima ifanye utafiti. Tunaendelea, Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi katika michangio yetu mjumbe wetu wa mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, una lolote la kusema kuhusu hoja.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, nitaiwasilisha na taarifa ya Spika itatolewa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Mhe. Waziri tunaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo katika kamati hii atakuwa ni Mhe. Bihindi Hamad Khamis, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleima Ali, na mwengine atakuwa ni Mhe. Ali Khamis Bakari *(Doholo).*

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya mwanzo leo hii kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunijaalia leo hii ikaweza kusimama kwenye Baraza hili la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Wanawake na

Ustawi wa Jamii, pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi mbili Waziri wa Elimu na Naibu Waziri pamoja na Waziri wa Afya na Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niaze kwanza kwa utangulizi wangu nianze kwa kulaani kitendo cha udhalilishaji. Mwenyezi Mungu anasema mdhalilishaji yoyote yule Mwenyezi Mungu atakwenda kumhukumu ndani ya haki, pia nitoe pole kwa mzazi mama na baba kwamtoto wao aliyedhalilishwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye mchango wangu kwa kamati hii niimpongeze Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza kuwasilisha ripoti hii kwa ufanisi na ufasaha na utulivu nasema hongera. Niendelee kwenye Wizara ya Afya najua kwamba wajumbe wa kamati walitembelea kwenye Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu lakini nikianza Wizara ya Afya kwenye vituo vya afya ambavyo walitembelea Unguja na Pemba, kuna changamoto mbalimbali ambazo wamezieleza.

Mhe. Mwenyekiti, niende Hospitali ya Wete, kuna changamoto nyingi ambazo wamezieleza na faida zake. Lakini pia Hospitali ya Wete kuna changamoto kubwa ambayo kwa upande wa nyuma wa Hospitali ya Wete kuna makaro ambayo yamefurika vinyesi. Namuomba Mhe. Waziri alifuatilie suala hili kwasababu ni eneo ambalo lina mzungumko kwenye upande wa wanawake aweze kulifuatilia, ili aweze kulitafutia ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee Hospitali ya Micheweni walieleza kuwa wametembela vituo vyote vya Unguja na Pemba, Hospitali ya Micheweni ni hospitali ambayo ni ya Wilaya, lakini pia nayo kwenye uzio wake uzio ushakuwa wa zamani. Pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majibu anieleze ni sababu gani

ambazo zimezuia kuweza kufanyiwa utekelezaji wa uzio ule ili uweze kuzuia maeneo ambayo ni ya hospitali ile.

Pia niende upande wa changamoto ambazo zimo kwenye hotapitali yetu hiyo hiyo ya Micheweni, tukiangalia hospitali ya Micheweni kuna eneo ambalo kwenye wodi za watoto, wodi ya wanawake na wodi ya wanaume hospitali ile rangi yake tanu hospitali ilipoanza kuhamiwa, rangi ipo ile ile haijabadilika na maeneo yale ambayo wanatumia wananchi kwa kulazwa na huduma nyengine kwa kweli ni chafu. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hiyo siku ya kutoa majibu ni sababu gani ambazo zimepelekea hospitali ile ikawa ina hali ile ambayo hairidhishi.

Vilevile, katika Hospitali ya Micheweni tunajua kwamba tuna ambulance ambayo inawachukua wagonywa kama wamepata rufaa ya Wete ukosefu wa mafuta, Mhe. Waziri wa Afya ukosefu wa mafuta kwa kweli ni changamoto kubwa sana tunajua kama *OC* ni ndigo lakini ukosefu wa mafuta upo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele Hospitali ya Wingwi kama tunavyojua tunajua kwamba sasa hivi kuna ugatuzi wa madaraka lakini Hospitali ya Wingwi imekabiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, pana nyumba ya daktari, pana kituo chenyewe lakini pia pale eneo lile linaingia maji. Je, Mhe. Waziri ni lini ataweza kufuatilia pamoja na kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, ili kuliondosha tatizo lile.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, kwenye changamoto na kwenye Hospitali iliiyoko Kojani kwakweli Mhe. Mwenyekiti, ameeleza changamoto hii ya kuhusu huyu mfanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni la muda mrefu tangu miaka mitano iliyopita kila mara tunabadilisha mfanyakazi lakini bado wananchi wa Kojani hawawapokei madaktari wae au

wafanyakazi ili kuwapa mashirikiano. Naiomba Wizara iweze kutoa taaluma kwa wananchi wa Kojani, ili waweze kuwapokea wafanyakazi na kuendeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, niende Hospitali ya Chake Chake kama alivyoeleza changamoto kama kuna kaa ambalo linataka kutengenezwa lakini pia tukirudi nyuma Hospitali ya Chake, kwakweli kuna dharau kubwa sana Mhe. Waziri, nakuomba sana uweze kuzungumza na wafanyakazi kwa sababu sisi wananchi wa Pemba tunatoka tunakwenda hospite ya Wete kufuata huduma. Lakini ukifika pale dharau kwakweli ipo kama walivyoeleza kipindi cha nyuma Waheshimiwa Wajumbe hapa kwenye michangio yao na maswali kwakweli hospitali zetu tukiangalia ni kweli zina dharau na hususan upande wa wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende kwenye Wizara ya Elimu niimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote lakini nielekee kwenye changamoto ambazo amezieleza Mwenyekiti wa Kamati wakati wa ripoti yake ni kweli, wajumbe wa kamati huwa wanatemboea lakini wakati mwengine huwa hawafi changamoto ni nyingi tunazozijua ni sisi tunaoishi kwenye maeneo yale.

Sasa naelekea Chuo cha Kiislam Micheweni, Chuo cha Kiislam pale palikuwa na gari ambalo walikuwa wanatumia tangu skuli ile ilipofunguliwa mwaka 1981. Kwakweli, skuli ile pale palikuwa na gari, gari lile limeuzwa najua kwamba ufuatiliaji wa Wizara ya Fedha kweli gari lile limeuzwa lakini wamepatiwa gari ndogo ambayo haitoshelezi kwa Chuo kile cha Kiislam Micheweni. Gari ile inatakiwa ikachukue kuni ikachukua na vifaa vya skuli kwa huduma ya wanafunzi Wizara ya elimu kwa kweli wafuatilie, ili waweze kuwanunulia gari angalau linaloweza kutoa huduma nzuri wa Chuo kile cha Kiislam.

Mhe. Mwenyekiti, nikirudi nyuma niendelee Skuli ya Micheweni, kwakweli skuli hii ina kilio kikubwa wakati wa mvua za masika, kama atunavyojua tuna watoto wetu ambao ni wadogo dogo sana na wanaweza kuchezea maji na huwa yanaingia mpaka maeneo ya skuli ndani kule. Sasa naiomba wizara kwasababu ndio wanaingia kwenye ugatuzi washirikiane na wizara nyengine ili kuweza kuwatilia fusi na kutengeneza miundombinu ya skuli ile.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nende kwenye maeneo ambayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, niipongeze na niitakie kheri njema na iweze kufanya kazi vizuri pamoja na viongozi, mawaziri na watendaji wote. Mhe. Mwenyekiti narudia tena nyuma wananchi wa Mkoa wa Kaskani Pemba hususan wanawake wanakilaani kitendo hiki cha udhalilishaji, kimetusikitisha na kweli kinatutoa machozi tukiwa wazazi suala hili ni baya sana, na kama tunavyojua mtu yeyote yule kama ni mwanawe kwakweli hakubali kufanyiwa kitendo kama hicho. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nampongeza Mwenyekiti wa Kamati naunga mkono ripoti hii ya kamati asilimia mia moja ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa mchango wako sasa namuita Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) akifuatiliwa na Mhe. Ali Khamis Bakar.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na mimi kutoa mchango katika ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa dhati Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wote wa

Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya na kutuletea ripoti nzuri ambayo takriban Mhe. Mwenyekiti, kachukua karibu masaa mawili kuisoma, ni jambo ambalo alikaa na kufikiria mengi ambayo kayagundua ayatoe moja kwa moja na sisi tunapata urahisi wa kuchangia. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara mbili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi pamoja na madaktari wetu kwa upande wa Wizara ya Afya na wasaidizi wao. Lakini pia na walimu wetu wakuu na walimu wa kawaida katika skuli zetu kwa shughuli zao nzuri ambazo wanaendelea nazo kuzifanya ili kuleta mambo haya muhimu juu ya afya na elimu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba huwezi kuwa daktari au muuguzi bila ya kusoma kwa hivyo elimu ni jambo la mwanzo utaalam ni jambo la pili. Kwa hivyo vyovyote utakavyokwenda mwalimu wako umuheshimu kwa njia moja au nyengine. Kwa kweli nawaheshimu walimu wote na nawaombea sana changamoto zilizowekwa hapa wapatiwe msaada mbali mbali juu ya maisha yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naanzia na Wizara ya Afya, kwanza niwapongeze madaktari wetu na wauguzi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika sehemu mbalimbali ya nchi yetu. Lakini pili nizipongeze hospitali zetu za Jeshi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Idara Maalum kwa kazi zao nzuri wanazozifanya na wao katika kuhakikisha kwamba wanawasaidia jamii kila inapohitajika na kusaidia changamoto zinazojitokeza katika hospitali zetu za serikali.

Vilevile, nivipoteze vituo vyetu vya afya mbalimbali katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, kwakuwa nipo Jimbo la Kijitoupele,

nasema tu kwamba tuna hospitali moja ya Fuoni ambayo kwa njia moja au nyengine yaani kituo cha Afya hichi kimezidiwa sana na wananchi wetu. Kituo cha Fuoni cha Afya wadau wake wakubwa yaani wagonjwa au wajawazito, wanatoka sehemu mbali mbali, Tunguu kwa bahati nzuri wanatoka huko siku nyengine. Lakini Pangawe, Fuoni, Kwarara, Kijitoupele, mpaka Mwanakwerekwe na kwengineko watu wanakuja huko kupata huduma hii kwa ajili ya kusaidia huduma za lazima.

Mhe. Mwenyekiti, naishauri wizara na nampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi yake ya kwenda mbio kwa kila sehemu. Lakini tunakituo chetu ambacho hiki ni kipya, narudia tena katika kikao hichi. Kituo hichi cha Magirisi maarufu sana katika Wizara ya Afya, Mhe. Waziri, sijamuona Katibu Mkuu tu katika kituo kile lakini kama ni kazi zake asibakie ofisini umefika wakati sasa hivi Mawaziri na Makatibu Wakuu na wengineo watembee katika maeneo mbalimbali, ili kuona changamoto za watu wetu wakati wa huduma zinapotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kituo cha Magirisi kitasaidia watu wengi sana, kikimalizwa, mama wajawazito, na watu wengine wote wagonjwa. Kituo hichi kilianzishwa na Waheshimiwa Wajumbe waliotangulia, kulikuwa na Mbunge wetu wakati huwo alikuwa Mhe. Sereweji na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha wakati huwo alikuwa Mwakilishi ambaye sasa hivi ni Mbunge wa jimbo hilo walikianzisha kituo hicho.

Kwakuwa, nimekikuta kituo hichi, wenzetu wamekiweka vizuri wameshakiezeka, kimeshajengwa vizuri kilichobakia bado plasta, madirisha, milango, tupate jipsam juu pamoja na tarazo chini kianze kazi. Kwa bahati nzuri Waheshimiwa wetu wametumia pesa nyingi sana karibu milioni 64, walitumia wao na mimi nikasema kwa kuwa nimelipata jimbo jipya nitahakikisha katika utawala wangu mimi sitokubali hata siku moja kushindwa kituo

hichi kifanye kazi kwa manufaa ya watu wetu hawa. Nimejitahidi katika mfuko wangu wa jimbo na nyenginezo nimejitahidi kupiga, nimepiga vizuri, madirisha tayari na milango ya mbele na nyuma bado milango ya ndani.

Mhe. Waziri tumekabidhiana kwa maelezo na mambo mengineyo, lakini kaniahidi kwamba kinafanyiwa kazi na kitamaliza. Namuomba hichi kiangaliwe ili kunusuru au kusaidia sana katika jamii katika maeneo yafuatayo. Kikimalizwa kituo hichi kitawasaidia sana watu wa Magirisi, Melinne/Uzi, Melinne/Tomondo, Kijotoupele, Kwarara, Pangawe na kadhalika, watatumia zaidi ya watu 40,000 katika kituo hichi hapa, kwasababu kituo cha Fuoni kwa Mhe. Yussuf Hassan Iddi, wenzetu wanashida sana na yeye Mheshimiwa shahidi anajua hali halisi ya huko. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja afanye bidii ili kituo kimalize haraka kipate kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja Hospilita ya Mnazimmoja, hospitali hii ni kimbilio la wananchi wetu wanyonge na hospitali nyengine zozote za serikali. Lakini bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti hushangaa na napatwa na masikitiko baadhi ya wakati wananchi wetu wanapata shida wapo kwenye vipimo. Wananchi wetu wanapata shida sana kwenye kutaka huduma hiyo hawaipati kirahisi, pamoja na uchakavu, sijui kuna uchakavu wa aina gani lakini mara kwa mara unaambiwa *CT-Scan* haifanyi kazi, *X-Ray* sijui imeharibika kitu gani, ukenda hospitali za kawaida unakuta huduma zile zinaendelea siku hadi siku, hakuna kuharibika chombo kile, pana nini hapa. Namuomba sana Mhe. Waziri na kamati katika taarifa yao nzuri tumeshuhudia kwamba lazima tukae pamoja tuangalie usalama wa vitu vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema wananchi wanasema kauli zao tofauti mimi siziungi mkono lakini kwakuwa wamesema na mimi

chombo hichi nitawasemea wanasema labda kuna kitu unakuja pale unataka kipimo cha *CT- Scan* hamna pale, unaambiwa kipo, lakini kiboru. Anaweza akaja mwengine mwenye uwezo wa pesa zake akafanyiwa pale pale. Hichi ni kitu kinaleta changamoto inataka ifanyiwe kazi na lazima iangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine *X-Ray* haifanyi kazi. Tunakuomba nenda zako TASAKHTA (*Global Hospital*) pale hili ni tatizo. Tunaomba sana jamani katika kazi zetu tuwe madhubuti kusimamia huduma hizi kwa maslahi ya wananchi wetu. Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mwenyezi Mungu ampe maisha mazuri zaidi marefu, ni mtu mkarimu, ni mtu ambaye anaumia sana katika taasisi ya afya kwasababu ndiyo alikotokea na ndiyo maisha yake yote mpala leo ukaona kwamba jitihada zake nyingi anazipeleka katika huduma ya afya na afya bora kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo suala la hospitali za Wanajeshi, hospitali hizi ukenda Bububu na Kibweni unakuta mazingira tofauti sana na hospitali zetu za serikali. Mhe. Mwenyekiti, unajua mwanajeshi anakula kiapo cha uaminifu japo sio kwa msahafu lakini kikatiba, kisheria lazima ule kiapo, lakini na madaktari nao ni lazima unakula kiapo cha uaminifu. Kwahivyo, lazima turudi, mwananchi anaridhika kwenda hospitali ya jeshi ikiwa Bububu ama Kibweni anasema kule napokewa vizuru na napata maneno mazuri au maliwazo mazuri. Turudi kwa Mwenyezi Mungu katika vituo vyetu mbalimbali vya afya vya serikali tuwe waadilifu, lakini kwanza tumuelekee Mwenyezi Mungu yeye ndiye anaetupa na anatuelekeza, tunachokipata tukifanyie kazi kwa moyo wetu, ili kunusuru jamii zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala moja kwa ufupi sana, Wizara ya Afya katika hospitali zetu lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja Kituo cha Mkono kwa Mkono. Kituo hichi ambacho

kinaitwa cha kutoa huduma pindi yanapotokezea matatizo ya udhalilishaji. Kwahiyo, nawaomba sana madaktari wetu na wataalamu kwanza tuelekeze imani kwa Mwenyezi Mungu, tuwape haki zao watoto wetu wanaoathirika au wanaodhalilishwa wakienda pale wapokewe, wafanyiwe uchunguzi na jibu lipatikane la ukweli kuliko kutumia mkono wa pembeni kurudisha chuki kwa mwenye mtoto yule kitendo kafanyiwa majibu hayapatikani. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti hili nawaomba madaktari wetu wazuri wanafanya kazi vizuri, lakini tuwaangalie sana watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara ya Elimu nitazungumzia machache na hiyo kwanza niwapongeze walimu kama nilivyowapongeza mapema, lakini niipongeze wizara kwa jumla kwa kazi zao nzuri. Tumesema tu kwamba katika changamoto zilizokuwemo katika mitihani yetu iliyopita mwaka huu kunakasoro zilijitokeza tukaambiwa skuli kama saba au tiza za mwisho kidogo sio suala zuri, japo watoto wengi wamefaulu lakini shule zetu nyingi zimeanguka natoa ushauri kama ufuatao.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 30 na 31 kamati ilitoa maoni ya ushauri na maagizo naomba kwa ruhusa yako Mheshimiwa ninukuu namalizia. Ushauri wa maagizo ya Kamati ukurasa wa 30 kutoka changamoto hizo kama inaeleza yafuatayo:

a) “Kamati inaishauri serikali kuona ulazima wa kuona Tume ya Utumishi ya Walimu kwa kushughulikia tatizo kubwa la ajira ya walimu. Matatizo ya kiutumishi ya walimu kwa upekee na wingi wake mahitaji halisi ya upungufu na ujazaji wa nafasi zilizowazi. Kamati inasisitiza umuhimu wa Tume ya Utumishi ya Walimu kwa kuwa ni mfumo ambao unatumika katika nchi nyingi za Afrika Mashariki na duniani na unasaidia kutatua changamoto nyingi za

kiutumishi na ajira za walimu ambazo kwa Tume ya Utumishi ya Serikali peke yake hazimudu kwa ufanisi."

Naomba Mheshimiwa hili liangaliwe, Tume ya Utumishi ya Walimu itatusaidia sana.

b) "Stahiki za walimu zifanyiwe kazi ili kuondosha malalamiko ya walimu ambao baadhi yao muda mrefu hawajalipwa stahiki hizo." Na hili liangaliwe.

c) "Kama inaagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ishirikiane na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kushughulikia na kuvipitia upya viwango vya nauli za walimu katika gari za abiria. Viwango hivyo vinawekwa na Idara ya Usafirishaji na Leseni ndivyo vinavyotumika na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..."

Kwa hivyo, naomba na hili liangaliwe ili nauli zao ziende sambamba.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha kuwa uhamisho wa walimu unafanyika kwa mpango bila ya kuleta athari katika maendeleo ya masomo ya wanafunzi.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hii Kamati imefanya kazi vizuri nimpongeze mwenyekiti na watendaji wake wote, kwasababu bila ya kuwepo mahitaji haya tutakuwa nyuma katika kuwafanikishia wanafunzi wetu. Niseme tu kwamba mimi nina ushauri mwengine wa kuwapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, kweli tukubali kidogo tumeanguka kwa kipindi hiki, japo wanafunzi watakuwa wengi, lakini kielimu skuli zetu zimeanguka sana ukilinganisha kwa Tanzania nzima. Ombi langu na ushauri, mwalimu kahitimu soko la Kiingereza au *Geography* au Hesabu, kama kahitimu soko la Kiingereza anaambiwa wewe pale kasomeshe Kiswahili anapangiwa somo la *Geography*, mwalimu kweli ana fani mbali mbali lakini unamuharibu akili yake.

Kwahivyo, naomba kutoa ushauri walimu waangaliwe kila fani ya somo lake alilofaulu bora apangiwe katika somo lile, hapo itatusaidia sana kukuza elimu. Lakini usimlazimishe mwalimu kahitimu somo la *Geography* ukamwambia akasomeshe somo la hesabu, ni wajibu wake aingie huku na huku, lakini kwanza watafutwe walimu kwa kipaumbele wa masomo waliyofaulu, basi hapo elimu yetu itakuwa vizuri na nahakikisha kwamba haya yaliyotokea hayatatokea tena.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho niseme tu kwamba naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, nawapongeza walimu wote, naipongeza Wizara ya Afya na nawapongeza madaktari wetu. Tunaomba wizara zetu mbili hizi sisi ndio walengwa wa mwanzo, bila ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kusimamia walimu wetu na wanafunzi wetu vizuri basi hatutopata madaktari wazuri na wengineo. Madaktari wetu wanapopata kufanya kazi zao vizuri kwanza wakumbuke walikuwa walimu walipata shida kuwapa wao na wao wawatumikie wananchi kwa kadiri ya uwezo wao.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa heshima kabisa naiunga mkono ripoti hii ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa taarifa nzuri na naiunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). Sasa namuita Mhe. Ali Khamis Bakar, akifuatiwa na Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi).

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ambayo iko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nimpongeze tu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa kazi kubwa ambayo ameifanya yeye na wajumbe wake. Vilevile, nizipongeze wizara mbili hizi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Afya, kwa kushirikiana vyema pamoja na kamati hii na kuibua changamoto na mafanikio ambayo yalipatikana katika kipindi hiki kifupi, ambacho kamati ilikwenda katika wizara hizi, ili kujua yale ambayo yanatekelezwa, lakini vile vile yale ambayo kwa kipindi hiki yameibuka kama kuwa ni changamoto.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa upande wa Wizara ya Afya kisiwani Pemba. Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuipongeza kamati kwa kazi kubwa ambayo wamefanya, nimeona hapa kwamba miongoni mwa ziara yao katika sehemu ya afya, walitembelea katika hospitali tatu hizo walizozitaja hapa ikiwemo ya Abdalla Mzee, Chake Chake, Wete na Kojani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nianze kwa changamoto ambayo ilianza kwa upande wa Hospitali ya Abdalla Mzee kule Kisiwani Pemba. Walisema hapa kamati imebaini changamoto ya kuharibika kwa mashine ya kusafishia picha katika hospitali ya Chake Chake, jambo ambalo limekuwa ni kero na usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaohitaji kupatiwa huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba changamoto hiyo waliyoieleza ni kubwa na kama tunavyojua Hospitali yetu ya

Chake Chake pale sisi ndio kiyoo, takriban Wapemba sote pale ndiko tunakokwenda kwa ajili ya kupata matibabu. Lakini jambo la kusikitisha kwamba kifaa hiki sijui kina gharama kiasi gani, jambo ambalo linaweza kutekelezeka kwa haraka, ili kuondosha usumbufu huu.

Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara iangalie suala hili, sielewi ni wino gani au ni mashine gani hii na gharama yake, wao ndio wanatambua hiki kilio. Lakini waangalie tu kwamba tatizo hili kama lina muda mrefu na sisi ndio ambao tunalihitaji kwa wananchi wa kule kisiwani Pemba, ukiwacha kwenda Abdalla Mzee ambako ni mbali basi Chake Chake ndio *center*. Ningependekeza wizara ilione hili ni changamoto kubwa ambalo linasababisha kuzoroteka kwa baadhi ya mahitaji ya wananchi wetu. Naishauri wizara waangalie ni kiasi gani cha fedha, vile vile liharakishwe ili wananchi hawa waweze kupata ile huduma ambayo inastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika changamoto kumetajwa changamoto nyengine ya ukosefu wa vipande, yaani zile *ID card* kwa wafanyakazi hususan katika Kituo cha Kojani. Mhe. Mwenyekiti, suala kama hili ukilisikia kusema kweli nalo pia halipendezi. Mimi nataka niulize kwa upande wa wizara, sijui *ID* hiyo inahitaji gharama kiasi gani kuweza kuwa mpaka leo labda wafanyakazi hawa wameshindwa kupatiwa hizo *ID card*, ili kuweza kufanya kazi zao vizuri ili na wale wananchi wanaokwenda pale kuwezakuwatambua kwamba hawa ndiyo wafanyakazi wetu. Vilevile, na wao kama wafanyakazi kuweza kujua kwamba mimi wajibu wangu ni upi katika masuala yangu ya kazi.

Vilevile, naishauri wizara kuona kwamba jambo hili kama ni kero ndiyo maana likatajwa hapa katika kamati liweze kufanyiwa kazi. Nikiendelea katika changamoto ya hii nyumba ambayo imetajwa

katika sehemu hii ya Hospitali ya Kojani ambayo imeelezwa hapa kwamba kuna nyumba ambayo anatumia huyu muuguzi kwa ajili ya kutoa huduma. Hapa mimi niseme pamoja na Wizara lakini kunajitihada kubwa ambazo zinatakikana zichukuliwe kwanza aanze sheha, pili aendelee Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kuweza kuwapa taaluma hawa wananchi juu ya umuhimu wa hili jengo ambalo limejengwa pale kuweza kutokumfanyia bugudha ya yule mtu ambaye amekabidhiwa kwa ajili ya kuweza kutoa huduma. Kwahiyo, naiomba serikali, wizara husika pamoja na Mkuu wa Mkoa kwamba aende akaweke mkutano pale kuwaeleza wale wananchi juu ya matumizi halisi ya hii nyumba waache kumbugudhi ili aendelee kubakia na kuweza kutoa huduma.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika *bullet* ya (f) changamoto ya Hospitali ya Abdalla Mzee ambayo kumetajwa kwamba hospitali pia haina haina mtambo wa gesi kwa sasa, mitungi iliopo ni 11. Hii ni changamoto kubwa katika hospitali hii kubwa ya Abdalla Mzee sisi ndiyo tunayoitegemea kwa upande wa Pemba. Vilevile, hata wenzetu ambao wapo kisiwa cha pili cha Unguja tunaona kwamba baadhi ya matibabu basi wanahamishiwa au wanaondoka au wanachukua safari ya kuja kule kisiwani Pemba na kuweza kupata matibabu. Sasa leo hapa unambiwa hospitali kubwa kama ile haina masuala ya gesi au haina gesi kuna mitungi kumi na moja.

Mhe. Mwenyekiti, naona siku hizi kina *Mihan gas*, sijui kuna nini *gas* kwa kusema ukweli mimi hata hayo majina ya *gas* siyajui na tukiangalia hii mitungi kuna mpaka ya bei nafuu kuna kumi na tano, kumi na sita, sijui laki tatu, sijui elfu sitini, elfu hamsini.

Mhe. Mwenyekiti, kusema ukweli hapa nilikuwa tu naiomba wizara na Mhe. Waziri wa Afya natumai ananisikia mitungi hii kumi na moja ni kidogo alau hospitali kubwa kama ile ni wakupata angalau mitungu sitini kwa siku, kwasababu wamesema

hapa kamati imekwenda na ikaona kwamba huduma hii ya upasuaji ni ya kila siku. Kwahiyo, ina maana mitungi kumi na moja hii inawezekana pengine kwa siku moja ikamaliza hata mitatu. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti hili ni suala analo ni vizuri kufanyiwa haraka iwezekanavyo, ili kuweza kuonekana kwamba huduma hii inapatikana kwa ukaribu zaidi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti hapa nadhani Mhe. Waziri wa Afya ananisikia vya kutosha, naomba nimuulize swali langu katika Jimbo langu la Tumbe kuna jengo la mama na mtoto tumefikia hatua ya uwezekaji na jengo lile limekwama. Kwahivyo, naomba wizara au kitengo kinachohusika kuweza kutusaidia watu wa Tumbe, ili kupunguza mrundikano wa wananchi wanaokwenda Micheweni kwa ajili ya kujifungua jengo lile. Hivyo, ni lini Wizara ya Afya itatusaidia kuona kwamba changamoto ile inaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende upande wa masuala ya Ugatuzi Elimu ya Msingi na Maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali na wizara kwa ujuma kuona kwamba jambo hili sasa hivi limegatuliwa kutoka katika wizara husika na likapelekwa hapa licha ya mafanikio yaliopo lakini bado kuna changamoto, ambazo changamoto hizi kwa kusema ukweli Mhe. Mwenyekiti mimi nikiwa mjumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum na sisi vile vile tumeliona ingawa huku wenzetu wa Kamati ya Ustawi wa Jamii wamelieleza kwa wale ambao wameyaona kwa juu.

Lakini na sisi kwa upande wetu tumeangalia kuna mambo mengi. Kwa mfano, moja kati ya nililoligundua ni ukosefu mkubwa ambao wa elimu kwa wananchi pamoja na kwa hizi wizara ambazo zimegatuliwa kwa kipindi hiki kifupi kuweza kujua wajibu wao, kwasababu wakati mwengine unaweza ukenda pale Mhe. Mwenyekiti ikiwa hata wale watendaji hawajui kama jambo

hili linastahiki kiupande wao kama ni la huku huku liliko gatuliwa kwenye halmashauri ama linahusu wizara moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, bado kungali na changamoto lakini vile vile kuona kwamba jambo hili limekuwa ni tatizo, hivyo naomba kwanza nimuulize Mhe. Waziri wa Elimu hapa yupo kuna usemi ambao baadhi ya skuli zilizoko vijijini, lakini sijafanya uchunguzi kwamba bado kuna matatizo ya walimu ambao kuna wanafunzi ambao wanatoleshwa ada. Kwahiyo, hili mulifuatie mujue kwamba kweli hizi ada za wanafunzi ni wapi wanaostahiki kutoleshwa hizi ada je kwasababu kuna wanafunzi tumeona hapa wanapasi wengine darasa la nne, darasa la sita, saba na la kumi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba mtakapokuja japo kama kwenye majumuisho sio leo tumeambiwa kwenye bajeti lakini najue na nyie mtapewa nafasi ya kuweza kuzungumza hapa, hivyo mtuambie ni sehemu gani na gani wanafunzi wanahitaji kulipa na sehemu gani na gani wanafunzi hawahitaji kulipa, ili wale wananchi wetu wanotuuliza kule tuje tuna jambo gani au jawabu gani yakuweza kuwajibu, niwambie kwamba bado kuna tatizo hilo.

Vilevile, kwa upande wa afya ni hali kadhalika tunaweza tukaenda katika vituo vyetu ambavyo vimegatuliwa bado upatikanaji wa dawa kama wenzetu walivyoeleza humu unakuwa ni wakusuasua, hujui kama wewe hospitali ile ipate dawa kupitia halmshauri au ipate dawa kupitia wizara bado kuna changamoto. Hivyo, ni vyema wizara zishirikiane na halmashauri zilizopo kwanza zifanye ziara, pia ziandae mikutano juu ya wananchi kuwapa elimu ya kutosha juu ya hili jambo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika ukurasa 29 sehemu ya changamoto ambazo zimetajwa katika masuala mazima ya Elimu Mbadala. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze

tena kamati kwa kazi kubwa ambayo wamefanya ya kuweza kuona haya mambo ambayo walipitia katika kamati na kuweza kuyaeleza humu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kwanza na hapa nauomba Mhe. Waziri wa Elimu anisikilize vya kutosha juu ya hili jambo ambalo nataka kulieleza.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imejitahidi kuweze kujenga skuli hizi kwa ajili ya vijana wetu waliotoroka skuli, lakini hata wale ambao wanaendelea skuli kuweze kujiunga katika skuli hizi za Elimu Mbadala au Mafunzo ya Amali kuweza kupata taaluma. Katika Jimbo la Wingwi ambalo ndio jimbo langu ninalokaa, lakini Jimbo langu la Tumbe lile ninakaa nimeenda katika kituo kilichopo pale cha Elimu Mbadala kilichopo Wingwi na nashukuru kwamba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Issa Haji Ussi Gavu) siku ile alikuwa mgeni rasmi nilibahatika kualikwa pale nikaenda kuona jinsi gani ya kile kituo. *(Makofi)*

Kwanza nimpongeze Mwalimu Mkuu ambaye kakibidhiwa kile kituo yuko vizuri na ile skuli wanosoma nawashukuru sana wale vijana wetu bado ile skuli hawaijafua lakini cha kushangaza Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa skuli hii imeambiwa ni ya mbadala kuweza kupata taaluma vijana ambao wamekwenda kujiunga pale lakini hadi leo skuli hii tena nakwambia tunaweza tukaja tukapata maiti hapa, haraka haraka skuli ile haina umeme, sijui kama ni mwalimu ama ni vijana waliopo katika shule ile kuona lile jambo wanalihitaji lakini kwa haraka haraka halipo wamechukua waya za baskeli maana yake mimi lazima niseme hivyo, waya za baskeli kuweza kuinganisha umeme kutoka kwenye skuli nyengine iliyopo jirani ya msingi kuweza kuingiza ndani ya kituo kile au skuli ile kwa ajili ya kuweza kupata huduma yao.

Kwahiyo, kumeunganishwa umeme jambo ambalo ni hasara waya zenyewe hazikupitishwa ambazo ni zile anazozisema Makombora kwenye michezo ni zile waya feki wameunga tu wenyewe wanavyojua wenyewe wameziunga wakaweza kupata, kwasababu pale wanahitaji ule umeme uwake kwa ajili ya mafunzo la mwanzo kuweza kupata kujiendeleza katika shughuli zao za masuala ya umme yaani kupata mafunzo, vile vile kuweza kutumia kwa ajili ya vyarahani pamoja na kuweza kutumia kwa ajili ya kompyuta ziliopo.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine hizi kompyuta ambazo zipo pale nne, madarasa nimekwenda nikayangalia mimi mwenyewe vijana waliopo pale karibuni madarasa matano vijana waliokwenda kujiunga. Kwahiyo, kampyuta zilizopo ni nne na hizo nne mwalimu anayefundishwa bado hajaajiriwa ni kijana anayetoka Konde anajitolea tu katika kipindi chote hiki shule ile ilipofunguliwa mwalimu huyo yupo lakini yeye bado anajitolea. Kwahiyo, naiomba sana wizara kwanza ifanye jitihada za makusudi kwenda kuiangalia ile skuli kufanya upelelezi, kwanza kuwaondolea hili tatizo la umeme, lakini kuwaondolea tatizo kubwa la huyu mwalimu wa masuala ya kompyuta.

Lakini vile vile kwenye masuala ya vyarahani ambavyo vipo pale vyarahani havikishi haja mimi nashukuru tu kwamba wamejitahidi vyarahani vilivyopo vinafika vinane lakini bado havitoshi kwasababu manafunzi mmoja akikaa hata akishakata sindano mbili anamsubiri mwenzake zaidi ya watu wanasubiri charahani hiki kimoja. Kwa hiyo niwaombe tu wizara na hili waliangalie waende wakaangalie pale ili kujua changamoto zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza hapo niende katika jimbo langu Mhe. Mwenyekiti, hivyo kwanza nishukuru serikali vile vile niishukuru Halmshauri yangu Mkurugenzi wangu, vilevile na

Wizara ya Elimu nimshukuru dada yangu Mhe. Waziri Riziki Pembe Juma kwa kuchukua jitihada za makusudi kuja katika skuli yangu akanitembelea na tukaweza kuweka mawe ya msingi katika skuli ile, lakini hapa nina masikitiko kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, skuli nimetumia fedha za Mfuko wa Jimbo na nyengine ninazojua mwenyewe pakuzipata, nashukuru tumeshirikiana katika hatua ambayo ndiyo kubwa, lakini imebakia ndogo na sisi siku zote tunaambiwa kwamba tujitahidi ili suala la elimu liboreke. Sisi wanafunzi wanaotoka Chimba, Pobwe, Shumbaviamboni hawa wengine maana ile Shumbaviamboni viko mbili kuna hapa wanapopita Uwondwe washirikiana na wale wa Shumbaviamboni Miondoni kujia upande wa Chimba. Chimba skuli iko mbali tumeamua kuweka shule ile ili kupunguza wale watoto masafa lakini vile vile kuhatarisha hatarishi zinazoweza kutokezaa barabarani, shule ile imebakia jambo dogo tu Mhe. Mwenyekiti jambo lenyewe lililobakia ni masuala ya vyoo kuweza kujegwa na huduma ya maji kwasababu maji kama tunavyojua ni muhimu sana kwa binadamu, kwa hiyo waweze kupata vitenda kazi vilivyobakia.

Kwahiyo, naomba Waheshimiwa Mawaziri wangu kwamba suala hili la vyoo lini tutashirikiana kwa pamoja kwa ajili ya kuondoa kero hii ya vyoo pamoja na yale maji, ili wanafunzi wale skuli ile katika mwaka huu 2018 iweze kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ni hayo. Nakushukuru sana pamoja na kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) kwa kutetea sana jimbo lako liweze kupata huduma ahsante sana. Mhe. Simai Mohammed Said atafuatia Mhe. Mussa Foum Mussa ajitayarishe. Mhe. Simai karibu sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, samahani nilifikiria mtu ameomba utaratibu alipogonga ndio maana nikasita.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwa wizara hizi mbili ambazo ni mama mtambuka. Lakini pia nichukuwe nafasi hii pia kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayoifanya kuendeleza Zanzibar hasa katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Vilevile, nichukuwe nafasi ya kipekee kuipongeza Kamati hii ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2017/2018 na pongezi ziende kwa kamati hii pamoja na Mwenyekiti Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, naweza kuthubutu nikasema kwamba *this is the fantastic report, it is one of the best*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo mimi pia ni mjumbe wa Kamati ya Bajeti na ripoti yetu itakuja lakini nasema hivi kwasababu kupitia hii kama umeipitia hii ripoti kwa kweli naweza kusema kwamba hii ripoti inatoa mwanga mzuri juu ya changamoto na ushauri na wajumbe wa kamati hii kwakweli walikaa kwa pamoja ukiangalia lina kurasa chache, lakini naweza kusema mpaka hivi sasa basi ripoti hii ndio itakayokuwa inaongoza kuangalia kwa uandishi wake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu kwa ukaribu wao, ukarimu wao na kuniamini meseji zao nazipokea, simu zao wanatumia na nitaendelea kadiri ya uwezo wangu kuweza kunishauri na kuichangia ripoti hii kitaifa. Kwahiyo, naomba pia kwa ruhusa yako niweze pia kutoa ushauri juu ya Jimbo langu la Tunguu, ambalo mimi naliwakilisha, ili nao wananchi nao kwa njia moja au nyengine wapate mawili matatu ya kwao.

Jambo la kwanza nikimwambia Mhe. Waziri wa Afya *inshaallah* Mwenyezi Mungu akijaalia baada ya Baraza hili basi tufanye rasmi ziara ya Jimbo letu la Tunguu kwenda kuangalia kasi ya maendeleo inavyokuja hasa katika Sekta ya Afya na mahitaji ya wananchi na pia ikiwezekana tufike mpaka Kisiwa cha Uzi, ambapo ni moja katika maeneo ya watu ambao naweza kusema kwamba ni maskini au wana hali duni kwa upande wa Zanzibar, ili tuangalie njia gani tutaweza kuwasaidia wananchi wetu.

Lakini nataka nizungumze pia suala la asubuhi leo kuhusu bima juu ya masuala ya magari. Mhe. Waziri wa Afya wakati nauliza suala lile la nyongeza aliniambia nitoke nje nikaangalie gari, Mhe. Mwenyekiti nilikwenda nje kuangalia magari ya mawaziri, magari ya mawaziri wote vioo vyao ni vyeupe havita stika vyengine havina hata *road license* hakuna gari hata moja yenye bima isipokuwa ya taarifa niliyofanya utafiti gari ya Mhe. Waziri wa Fedha ndio gari pekee niliyoambiwa ina bima ndiyo nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha. Hivyo, inawezekana mawaziri wengine washakata bima yao lakini hawajabandika kwenye magari, basi itakuwa vizuri na wao wazibandike. Ikiwa mwananchi anakata bima juu ya magari yao basi na utaratribu huo uendelee na kama bima zao wanazo basi wazilete tuzione, lakini gari ya Mhe. Waziri wa Afya haina bima ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka niongelee juu ya changamoto zilizokuwepo juu ya Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, naomba unilinde naona kuna watu wananong'onea sana watu wanazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hospitali yetu ya Mnazi mmoja pamoja na hospitali nyengine zote za Pemba naomba ifahamike kwamba vitu viwili ambavyo vinasumbua sana hospitali hizi mbali ya vifaa waliokuwa navyo na mahitaji.

Naomba kutoa ushauri katika suala zima hasa la watendaji wetu ambao wanasimamia katika nafasi kubwa mpaka chini lazima katika *management* na *supervision* ya watendaji wafate zile *code of conduct.* Wafanyakazi wa chini na wafanyakazi ambao wako juu ni ma *senior* ukaribu wao lazima wazingatie sana kujenga umoja wao, na kuamini kuwa kwmba huduma wanazotoa hasa katika hii Sekta ya Afya na hospitali hizi ni muhimu, na ikiwa watendaji wakuu pamoja na wa chini hawatabalika mawazo yao, fikra zao, basi ripoti hii juu ya changamoto walizotoa lakini pia na ushauri wanaotowa itakuwa ni vigumu kuutekeleza.

Kutokana na hali hiyo namuomba sana Mhe. Waziri wa Afya aendelee kutumia lugha kukaa nao na viongozi ambao wanahusika, ili kuhakikisha kwamba lugha na utendaji wao unabalika katika utendaji na mawazo yao.

Vilevile, nataka nizungumze juu ya maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, huwezi ukambadilisha mtu mawazo yake ikiwa haki zake naye pia hazipati Mhe. Mwenyekiti ukienda Hospitali ya Mnazi Mmoja ukiangalia masuala ya *outfit allowance* pamoja na *night allowance* ukiangalia kwa ujumla maslahi ni madogo nayo pia ya watendaji wetu yanachangia pia, hasa safari ni hatua. Kwahiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Afya katika bajeti hii atakapokuja mwaka huu aanze na kianzio, ambacho angalau hawa watendaji anaowasimamia unaweka huo utaratibu wa kuweza kupata maslahi yao, ili mtu yeyote afanye hakuna binadamu yeyote atafanya kazi bure, atafika pahala atajitolea kwa uzalendo wake, lakini atafika pahala atashindwa. Kwakweli, usiku kuwepo kwa huduma zinazostahiki kwa Mnazi Mmoja ni muhimu hivyo maslahi yao yanahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana wakati nachangia ripoti hii nilizungumzia la *reagents* kwa juu ya suala zima la maabara namshukuru Mwenyezi Mungu kuwa sasa *reagents* sasa

zinapatikana vizuri, lakini kuna tatizo kubwa kwenye maabara ni suala la *service*. Kwa mfano, tukiangalia mashine kama ya *chemistry* ambayo inatumika kwa ajili ya figo, maini mashine ya *electrolytes* ambayo inahitajika kupimia chumvi zimelala na hizi zinahitajika kwa ajili ya watu wa *ICU* zimeharibika zimelala kwasababu hakuna mafundi wa kutosha.

Lakini hadi leo ukiangalia Hospitali ya Mnazi Mmoja ina *Biomedical Engineer* mmoja. Sasa tusomeshe watu ambao wanahitaji katika fani hizi, ili waje kusimamia masuala haya, leo kila ikitoa tatizo mafundi kutoka Dar es Salaam. Tunahitaji at *least* tuwe na *Biomedical Engineer* wasiopunguwa watano katika ile Hospitali ya Mnazi Mmoja peke yake.

Tukienda katika suala la kwenye mambo ya *X-Ray* uhaba wa wafanyakazi *rediographer* tunao wachache tuwasomeshe zaidi, ili ambazo hizi huduma ambazo wananchi wanahitji kila siku hasa wale vijana wa bodaboda, waziri mmoja anawapenda sana huku mbele wanapotaka kuja wanapelekwa na miguu yao ishavunjika washapata maajali. Kwahiyo, *rediographer* tunahitaji wa kutosha, ili huduma zifike kwa wananchi wetu na hasa hao wanaotoka maeneo ya mbali kuja zao mjini kwa matumaini kwamba wanapofika mjini watapata huduma inayosthiki.

Wale wananchi wanaotoka Makunduchi jimboni kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman wanotoka kule Kaskazini kwa Mheshimiwa rafiki yangu Mhe. Ame Haji Ali kule Nungwi, wanapokuja mjini wanahitaji hizi huduma, sasa naomba kwamba suala la *biographer* haya tusiyarudie kila siku, tuwaongeze tunao wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, pia suala la madawa na bohari yetu usimamizi mzima je tunakwenda sambamba na fedha ambazo serikali inayotumia. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kamati katika mwaka unaokuja wa bajeti wangalie sana suala la bohari na madawa

fedha zinazotumika juu ya masuala ya madawa na hii Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini nimuombe yeye mwenyewe akiwa ni kiongozi maana yake yeye ni *senior* humu ndani. Bohari hii ambayo fedha zinatumika za madawa je zinakwenda kwa stahiki maeneo yote Unguja na Pemba, maana yake serikali inasema pesa inatumia ni nyingi na bajeti kila mwaka inaongezwa, je huduma inakwenda sambamba na fedha inayokwenda, kwasababu hata leo binadamu unapotoka wewe kwenda kutaka kula chakula, ukitaka kwenda kula mbatata za urojo utakwenda mitaani, ukita chakula kizuri utakwenda Serena kule kwa Mhe. Nadiri anapenda sana kwenda, anakaa kule anafanya vikao vyake.

Sasa unapoangalia huduma unayolipia zaidi utapata huduma bora zaidi. Kwahiyo, hizi fedha ambazo kila siku Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Makamu wa Pili pamoja na Mhe. Waziri wa Afya wanzungumza juu ya bajeti, je wafanyakazi zinakwenda sawasawa kwanini wafanyakazi wetu au wananchi wakifika mahospitalini wanaambiwa kitu fulani hakuna, baada ya akiingia kiongozi mkubwa pale hospitali panapotokezea ajali unasikia vile vifaa vinaanza kutolewa.

Ndio maana nilikuwa namsikilizi Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) kwa umakini sana alokuwa anasema leo anayazungumza kitu kwa hisia anasema mambo yote yeye pamoja na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini suala la bohari walifuatilie kwa undani kamati yao na baadaye watuletee ripoti inayostahiki hasa hizi pesa, na ikiwa fedha hazitoshi basi bajeti hii tuongeze zaidi kwenye Sekta ya Afya kwasababu serikali tayari inaongeza mapato tusiwe wao wanaongeza safari za nje kwenye sekta ya Afya tunarudi nyuma kama bajeti fedha zinaongezeka kwenye kukusanya mapato basi na huduma za wananchi pia ziongezeke kuwa bora zaidi na huo ndio ushindi wa Chama cha Mapinduzi kuelekea 2020. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nigusie kidogo suala la elimu na ajira. Mhe. Mwenyekiti, hapa juzi watu walizungumza kwa hisia sana juu ya suala la ajira kwamba Wazanzibari wapatiwe kazi na kila kitu. Kwakweli, naunga mkono na yote na naamini katika sekta tofauti ya ujenzi, sekta ya utalii, sekta ya kilimo watu wanaajiri watu tofauti na Wazanzibari wanapata kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna changamoto bado tukiri tuliyokuwa tunayo. Hapa mjini nimepita sehemu tafauti kidogo maana yake naweza nikasema hasa nina uelewa mzuri kwa mitaani hapa na nina ukaribu na wawekezaji wengi tumepata kujua juu ya mambo mengi. Lazima tukiri kwamba suala la Wazanzibari changamoto bado tunayo kwenye suala la kuzungumza lugha ya Kiingereza na lugha nyengine, lakini pia kuzungumza kwa ufasaha pamoja na kuzungumza kwa *confidence* uwe unazungumza kwa umahiri na kujiamini. Watu wanaajiriwa wanakwenda maeneo wanapatiwa kazi lakini sasa unapokuja sehemu wakati mwengine una elimu ndogo au una elimu *size* unakuwa zile *principle* na *ethics* za ile kazi huzifuati.

Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kusema pamoja na Waheshimiwa Wajumbe mnanisikia hakuna mwekezaji atakayekuja Zanzibar akataka kuajiri mtu ambaye yeye yuko nje ya Zanzibar au anatoka Tanzania Bara au mbali huko ataangalia watu waliokuwa karibu ili awachukue. Sasa katika mkazo huu ambao tunakwenda kwenye suala la elimu tuzungumze katika elimu ambayo inakwenda sambamba na ajira zilizokuwepo mitaani. Mimezungumza mwaka wa kwanza hapa 2016 kwenye bajeti, nikazungumza kwamba ili ajira ziende vizuri moyo wa Zanzibar kwenye suala la ajira moja ni Chuo cha Karume (*Karume Institute of Science and Technology - KIST*) jirani yetu hapa. Na ukiangalia chuo hiki ni chuo ambacho kinastahiki kipatiwe kila nyenzo na nikazungumzia kuhusu masuala ya *mechanical engineers*, *electrical engineers*, masuala

ya *refrigeration* tuwasomeshe, ili katika sekta hizi ndio watakapoingia na kuweza kujiajiri.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukiangalia vifaa ambavyo vilivyopo hapa Zanzibar vinatumika ni vya zamani lazima tutulie mkazo katika maeneo haya, ili mtu akienda humu katika hizi ule uwezo wao uwe unakwenda sambamba na yale ambayo wanaweza kuyafanya. Sasa kama elimu tunayozungumza sisi ni elimu ipi na hiyo katika suala la *job creation* tunawaunganisha vipi. Leo unamsomesha mtu katika masuala ya *astronomy* aende zake kwenye mwezi kwani sisi malengo yetu Zanzibar ni kwenda kwenye mwezi? Tuangalie ajira iliyokuwepo kule na tuwasomeshe kwa kuwaunganisha.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar juzi katika hotuba yake alizungumza masuala ya *environmental science*, anaangali mabadiliko ya tabianchi na mazingira ambayo tunayoyahitaji. Sasa lazima mawaziri wenye sekta hizi waangalie hizo tunazohitaji pia huko nje na tutilie mkazo isiwe Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anapokwenda kwenye *cabinet* anaunga mkono mawazo yetu ambayo wajumbe tunabeba hapa wengine mawaziri mkaja mkayapiga na chini. Muyachukue haya kwa pamoja wote ili tukayafanyie kazi, kwasababu mawazo yanayotoka hapa ndio tunayoyaleta sisi ndio katika sekta hii…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

Mhe. Simai Mohammed Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Kwahiyo, naendelea kutilia mkazo kwenye suala la elimu na ajira lazima ziende sambamba, na ajira hizi ambazo zilizokuwepo huko mitaani tunazozizungumza sisi hata katika mahoteli unapoanza ujue kuangalia *hotel manager*, ukiaangalia kwenye *department* za *FMB*, ukiangalia kwenye *maintenance housekeeping*, ukenda

kwenye suala la *landscape***,** ukiangalia kwenye masuala ya *laundry* kote humo ndani kuna utaalamu. Mhe. Mwenyekiti, huwezi ukafika mpaka katika hoteli kubwa ukawa *hotel manager* kama hujapitia *department* zote hizi, kwenye hizi *department* unaweza ukafanya kazi masaa 15, kwasababu kazi hizi za mahoteli ni *labor intensive* unahitaji muda mwingi na utumie nguvu nyingi na maarifa na lazima uwe na lugha nzuri.

Sas, haiwezekani unapopelekwa pahala unamjibu kiongozi wako *supervisor* lugha mbovu, kazi ya masaa manane unataka uifanye kwa masaa matano uondoke. Kwahiyo, inakuwa hii ndio changamoto yetu hivyo lazima tujitilie mkazo tujali hizi kazi na tusibague. Mhe. Mwenyekiti, nilisema mwaka jana kwamba katika wilaya zetu zote Mhe. Naibu Waziri anayesimamia masuala ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma alikiri na nikamtaka kuanzisha *job centres*, ili kuwajua wananchi wetu kuwaorodhesha wote wanahitaji kazi zipi ile elimu waliokuwa nayo tuwaunganishe na soko la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu elimu na soko la ajira kwasababu hili ni kero tulilokuwa tunalo, unaweza ukazungumzia elimu ukamaliza kusoma kama ajira kule nje haipo inakuwa tena ni changamoto. Kwahiyo, elimu yoyote tunayoizungumza Zanzibar tuangalie elimu na soko la ajira lile tunalolitaka, na mawaziri wote katika suala hili wakiliweka pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, najua umenipa dakika mbili umeniangalia sana, basi nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya na Mwenyekiti wa Kamati, lakini pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mhe. Waziri kwa kupokea changamoto hasa katika skuli ya Tunguu pamoja na Kikungwi juu ya mahitaji ya wananchi, naamini Mhe. Naibu Waziri utalifanyia kazi vizuri ili wananchi wetu wa Kikungwi na Tunguu wale 55 wa Tunguu na 43 wa Kikungwi tuweze kulitatua tatizo lao na kwa

faida ya wananchi wetu. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana, nawashukuru sana wajumbe wa Baraza lako hili la Wawakilishi kwa kunisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Mussa Foum Mussa, akifuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajitayarishe.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa ruhusa hii ya kupata kuchangia kidogo au nikaweza kutoa mawazo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa ripoti yao nzuri na yenye mwelekeo kwa serikali yetu. Vilevile, niwapongeze mawaziri wote wa wizara mbili pamoja na manaibu waziri pamoja na watendaji wao wote kwa jitihada zao kubwa na nzito. Mhe. Mwenyekiti, kwasababu wizara mbili hizi ni wizara ambazo zina kazi nzito, kwasababu zote zinahusiana na kazi za kijamii, na kazi za kijamii zote ni nzito. Kwahivyo, ni pahala pao kwamba tunawapongeze kwa kazi hiyo wanayoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo kwanza nianze mchango wangu kwenye Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, nitaanza kuchangia ukurasa wa 11 unaozungumzia Hospitali ya Abdalla Mzee, Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tumeelezwa kwamba nadhani nikinukuu hiki kifungu cha (f).

> “Katika Hospitali ya Abdalla Mzee kamati imepata taarifa ya wafanyakazi wanaoletwa kutoka Unguja kuhama muda mfupi baada ya kuripoti”.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili kama lilivyoelezwa lipo na Hospitali yetu ya Abdalla Mzee kwanza nimpongeze Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutujengea hospitali nzuri kwa Pemba nzima. Lakini kama tulivyoelezwa hapa Mhe. Mwenyekiti hii hospitali nayo ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi, na mambo kama yalivyoelezwa hapa mengi. Kwahivyo, tunamuomba Mhe. Waziri ajitahidi hawa wafanyakazi wanaopelekwa Hospitali ya Abdalla Mzee wakaomba kurudi nadhani ni vyema wakajengewa miundombinu mizuri wakaendelea kubaki, kwasababu watu wanapata shida upungufu ni mkubwa wa wafanyakazi pale.

Mhe. Mwenyekiti, pia imeelezwa kwamba bado kuna tatizo la makaazi, makaazi bado ya hawa wafanyakazi hayajakuwepo vizuri. Sasa na hili nalo liangaliwe vizuri kwa sababu mfanyakazi kumuweka Chake-Chake aje afanye kazi Mkoani kwa mujibu wa mazingira yetu si hali nzuri. Kwahiyo, nadhani ni vyema yakatafutwa makaazi kule kule Mkoani ili kuona kwamba madaktari wetu wanabaki katika hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile nilielezee hili tatizo la wafanyakazi zaidi limeelezwa katika vituo vyetu vilivyomo katika shehia zetu. Kwakweli, hali ni mbaya, hali si nzuri ya wafanyakazi, upungufu ni mkubwa. Kwa mfano, kama nielezee mimi katika Jimbo langu la Kiwani tuna vituo vitano. Tuna kituo cha Mtangani, Kendwa, Tasini, Mwambe na Shamiani. Kwa mfano, kituo cha afya Mtangani kina wafanyakazi watatu, kituo cha Kendwa kina wafanyakazi wawili na huyo mmoja kipindi hiki kapata maradhi kenda operesheni, kwa hiyo kuna mfanyakazi mmoja akiumwa hapana muhudumu wa aina yoyote, pale hata *orderly* hayupoa, sasa nadhani hii hali sio nzuri.

Kwa upande wa kituo cha Tasini kuna wafanyakazi wawili mmoja daktari na mmoja ni *orderly*, ina maana daktari pengine anapoumwa au anapopata dharura yoyote ina maana anayekiendeleza pale ni *orderly*. Sasa hiyo kazi sijui kuna utaratibu gani wa *orderly* kutibu ikija ikitokea tatizo nani atakayekuja kulaumiwa. Mhe. Mwenyekiti, nadhani lile lile suala la upungufu wa wafanyakazi hapa linajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, pia Shamiani ni kisiwa nako pia kuna wafanyakazi wawili, mmoja ni daktari na daktari huyo huyo kapangiwa hospitali nyengine pamoja na *orderly* ndio wanaofanyakazi wawili tu. Kwahiyo, anapokuwa hakwenda daktari ina maana atakayetibu kule ni *orderly*. Mhe. Mwenyekiti, hii kazi ni kubwa, nzito kwasababu kwa mujibu wa utaratibu wenu wa afya *orderly* haruhusiwi kutibu litakapotokea tatizo sijui nani atakayejibu hayo masuala. Sasa Mhe. Mwenyekiti, niseme vijana waliomaliza *diploma* ya afya tunao wengi, katika jimbo langu mimi hawapungui kumi.

Kwahiyo, kuna tatizo gani kutokuajiriwa watu na watu wapo wamesomeshwa na serikali hii hii, tatizo ni nini? Ikiwa ni tatizo kama kumeelezwa huku. Kutokana na hali hiyo, naomba serikali itoe kibali na mimi nasema kwamba itoe kibali maalum kwa Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, kwasababu huu utaratibu uliopo hivi sasa unachukua muda mkubwa. Kwahivyo, nadhani wizara mbili hizi basi wapewe kibali maalum cha ajiri kwa mfano kama kipindi hiki tuna tatizo kubwa la ajira kwa Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali basi wapewe hiyo ruhusa mpaka hili tatizo liondoke, likesha kuondoka hiyo shughuli itabaki huko huko inakohusika. Lakini kwa kipindi hiki jamani hatari vijana tunao, wamemaliza Diploma ya afya wapo mitaani wamebakia tu huku tunalia na wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili suala serikali inatusikia kilio chetu.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile hawa madaktari wanaofanya kazi pamoja na hawa ma-*orderly* wanapokwenda kwenye likizo basi posho zao za likizo hawapewi, huo si utaratibu. Serikali imepanga utaratibu wake mzuri wafanyakazi kuna haki zao wapewe, basi wanapokwenda kwenye likizo hizo haki zao wapewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile nadhani kwenye Wizara ya Afya sasa nitoke kidogo niende Wizara ya Elimu nichangie muda wangu usije malizika.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia ukurasa wa 30 hapa naomba ninukuu changamoto katika utekelezaji wa programu, nitanukuu baadae nitachangia.

Kifungu (a) kumezungumzwa tatizo kubwa la uhaba wa walimu wa fani mbali mbali kuanzia msingi mpaka sekondari. Pia kunaelezwa hapa kuna changamoto katika mfumo wa ajira hasa kwenye sekta ya elimu ambapo mahitaji ni makubwa ya walimu, walimu wenye sifa wapo kwenye soko lakini ajira bado hawaajiriwi.

Mhe. Mwenyekiti, kiukweli kamati imeeleza vizuri kwa sababu nadhani wamepitia, mimi nataka nitoe mfano tu Kamati ya Ustawi wa Jamii imeenda katika skuli ya Mwambe wameona tatizo lililopo pale Mwambe uhaba wa walimu. Nataka niseme kwamba mwaka jana tuliandikisha watoto 611 lakini pale mwaka jana palikuwa na upungufu usiopungua walimu 30, mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri naomba hapa anisikilize vizuri. Mwaka huu tumeandikisha watoto 985 hii hali ni nzito, pale wanafunzi wanakwenda mikondo mitatu katika hizo skuli tisa zilizofanya vibaya darasa la nne na Mwambe imo kwasababu hii ya walimu, mikondo ni mitatu. Mkondo wa kwanza unaanza saa moja na nusu mpaka saa nne, saa nne mpaka saa saba, saa saba mpaka, hivi

kweli hapa patakuwa na usomeshaji. Mhe. Mwenyekiti, vijana waliomaliza cheti tunao wengi, waliomaliza *diploma* tunao wengi, waliomaliza *degree* tunao wengi tatizo liko wapi?

Mhe. Mwenyekiti, hii hali ni ngumu ya walimu upungufu umekuwa mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri mimi nasema kwanza niipongeze wizara kwasababu watu wa kale wanasema pangokapo jino hukaa pengo. Sasa naipongeza wizara kwamba alau wametuletea walimu tisa, si haba. Lakini bado upungufu upo kwa sababu wanafunzi wameongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba hiyo ajira ikiwa ipo basi wale vijana wetu wanaojitolea lile jicho lianze pale kwasababu wale vijana ndio watakapopata moyo. Nasema tena kwamba si vyema kwa vile vijana wapo pale kutoka sehemu nyengine zaidi hakuna ubaya kuwaajiri, lakini na wale pale basi wapewe *priority* mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema wakiajiriwa ni sawa, wasipoajiriwa basi liangaliwe lile pengo tupunguze ule ukubwa wa upungufu wa walimu pale, walimu 30 kuwa hawapo wengi mara hii hali mbaya zaidi, ikiwa mwaka jana tu tulikuwa hali mbaya kidogo mara hii kama mgonjwa husema tena anatiliwa maji maana hali mbaya zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo namuomba Mhe. Waziri ajitahidi na hiyo hali niliyoizungumza, ili tuone kwamba hali inapungua kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwamba tumeelezwa hapa kuna skuli ambazo zina dakhalia na kuna skuli ambazo hazina mpaka yale matokeo yake basi yanajionesha kwamba zile skuli ambazo zina dakhalia basi matokeo ni mazuri. Kwahivyo, tunaiomba serikali irudishe ule mfumo wa kizamani zilizokuwa

zijengwa *boarding*, ili wale watoto wakae pamoja tuone kwamba yale matokeo yanakuwa mazuri kwasababu tumeshaona mfano kwamba wale wanaokaa dakhalia na wale wasiokaa matokeo mazuri yanajitokeza wapi? Kwahivyo, nadhani Mhe. Mwenyekiti hilo ni suala ambalo wizara wachukue jitihada kupitia serikali, ili waone kwamba wanarudisha huo mfumo na kupata vijana wetu kupasi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba nifikie hapo na naiunga mkono Ripoti hii ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Machano Othman Said akifuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa ufasaha wake wa kutoa ripoti kwa muda wa masaa kama mawili. Tulikuwa tukijiuliza jumla ya hii ripoti ina kurasa 34 lakini kumbe muhtasari una kurasa 50, kwa hivyo ripoti ni ndogo kuliko muhtasari wenyewe. Lakini nafikiri ilitokana na kwamba baada ya ripoti kama mwenyekiti kuona kuna mambo ya msingi yanatakiwa kujulikana na wajumbe ndio maana ikawa hivyo. Tunamshukuru na tunampongeza sana. *(Makofi)*

Aidha, nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote wa kamati na niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri akiwemo Waziri wa Afya na Naibu Waziri wake na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu na Naibu Waziri wake. Wanajitahidi kuchapa kazi lakini nafikiri wizara hizi mbili zinachukua karibu *one-third*

au zaidi ya wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au nusu ya wafanyakazi.

Sasa hapa lazima tuone kwamba hawa wana kazi kubwa na ngumu na niungane na wale watu au Waheshimiwa Wajumbe waliopendekeza, ingawa kuna ugatuzi kwamba kuwe na Tume ya Utumishi wa kada hizi na wenzetu wa Tanzania Bara wanayo kule kwenye TAMISEMI. Kwahivyo, bahati nzuri hawa wafanyakazi wa msingi wa afya, wa simgi wa elimu sasa wote wanakwenda kwenye Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla pia wafanyakazi wengi wa wizara hizi mbili wanakaribia kustaafu katika miaka miwili mitatu ijayo, kada ya kati na wataalamu wa kati hawa wengi wao ni wale ambao waliajiriwa miaka ya 1980. Kwahivyo, na muda wao wa utumishi serikalini unakaribia kwisha. Sasa hofu yangu tunaweza tukachelewa kuajiri wafanyakazi wa afya, walimu baadae wakistaafu hawa kutakuwa na pengo la walimu wazoefu na wataalamu na wafanyakazi wa kada ya afya wataalamu. Kwasababu katika afya kuna madaktari, wauguzi, kila watu lakini wote lazima nao wawe na uzoefu wa kufanya kazi.

Kwahivyo, tuiombe serikali na ikiwezekana kwa kupitia sasa wangelifanya labda sensa maalumu ya kuwatambua wafanyakazi wao lini watastaafu kwa sababu wengine bado wako makazini. Lakini sasa hivi ukikutana nao wanakwamba mimi tena kwa umri wangu huu hata kazi siwezi kuifanya. Mimi nimeshakutana nao katika jimbo langu tulitembelea vituo vya afya wengine wanasema, 'baba mimi tena kuchukua mtoto nikamzalisha siwezi', yaani lakini bado umri wake wa kubaki kazini upo. Kwa hivyo, hawa ukisema kituo kina wafanyakazi wanne maana yake kituo kina wafanyakazi watatu. Kwa hivyo, lazima hili nalo liangaliwe kwa kina.

Jengine ni dawa. Tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba dawa sasa afadhali, hazijatosheleza lakini afadhali lazima tuseme ukipata lazima ushukuru. Na sisi tunasema dawa zinapatikana kwa kiwango hicho. Lakini kuna jambo ilikuwa nataka Wizara ya Afya itusaidie. Katika mpango huu wa matibabu Tanzania Bara wameupunguza sasa wamekuwa na vikwazo vile wamevipunguza. Kwa mfano, kituo cha afya cha Chuini wanatakiwa watoe panadol pengine na dawa nyengine moja tu kwamba za chini zile. Sasa hivi kweli hatufiki wakati baada ya miaka mingi hatuwezi na sisi tukabadilisha ule mfumo wetu kwamba na vituo vya afya vya kijijini vikapewa fursa na wao kutoa dawa za aina ngapi zikaongezwa zikapandishwa kidogo kutoa dawa au kutibu wagonjwa.

Kwasababu vituo vile sasa hivi vinatakiwa kama akienda mgonjwa wa kisukari mgonjwa wa maradhi mengine wanavyotakiwa hasa usiwatibu wawaondoe tu, wawapeleke katika maeneo mengine. Sasa na wagonjwa hao ni wengi sasa katika maeneo hayo. Je, tunachukua hatua gani kuona kwamba vituo vile vinatoa huduma na vinapata dawa, kwasababu bila ya kuwaadhibu wale wanaohusika na kule kutoa huduma katika maeneo yetu. Hili tumeona ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kama tulivyozungumza juzi wakati wa Kamati ya Tawala za Mikoa Mhe. Waziri na watendaji wake tunahisi wakati umefika kwa vituo vya SMZ za vikosi kupatiwa mgao wa dawa. Kibweni pale wanahudumia watu wengi wana kazi kubwa wanafanya, lakini ukiangalia hata JKU Saateni muda mfupi ujao watakuwa na mambo mengi. Sasa hivi wanang'oa meno lakini watafanya na operesheni. Kwahivyo, watakuwa wanazalisha pale itakuwa kituo kikubwa zaidi kwa hivyo watu wasaidiwe katika upatikanaji wa dawa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nizungumzie donda ndugu letu Hospitali ya Mbuzini. Mheshimiwa donda ndugu ni mwaka wa 14 sasa tangu kimeanza kujengwa kituo kile kwa matumaini ya kuwa Hospitali ya Wilaya ya Magharibi wakati ule ilikuwa Magharibi moja mpaka sasa imekuwa ni Magharibi 'A'. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na timu yake na pamoja na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii hili walipigie chapuo na yeye anatoka Magharibi, lipigiwe chapuo kituo kile kimalizike. Eneo liko kubwa, zuri, panafikika kwa njia zote, kwa nini hakiwezi kumalizika kituo kile, wakati vituo vipya vinaanza kujengwa vinamaliza kile kiko vile vile kwa nini kiko katika hatua ile.

Kwakweli, kama sababu kwamba wanataka waanze upya mimi naona sio tatizo kama wanaweza, sisi watujengee hata ghorofa sawa tu, lakini kile kituo kiwe Hospitali ya Wilaya kijengwe tumalizane na ile kadhia, itakuwa sio vizuri kwamba Mhe. Rais kaahidi tangu mwaka 2009 sijui na 2007 mpaka leo na amalize muda wake itakuwa bado sio jambo jema hakutendewa haki. Mhe. Waziri nafikiri kabla ya kuanza ujenzi wa Binguni basi kituo cha Mbuzini kiweze kujengwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna tatizo la walinzi kwenye vituo vya afya vyote vya Unguja na Pemba na hili liko katika Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio hizi wizara mbili. Hawaajiri walinzi, walinzi wanaonekana kama sio mfanyakazi wa serikali, lakini maofisini kwao wameajiri walinzi na wanalipwa, sasa wale wanatarajia nini? Wale kule kwenye vituo vyetu kunafanyika wizi kwa sababu hakuna walinzi, wanaweza kuleta kifaa cha gharama cha shilingi milioni tano au kumi siku ya pili kikaibiwa kikenda kuuzwa kwa shilingi laki moja. Kwahivyo, nahisi hili litiliwe mkazo.

Nije Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, napo hapa nampongeza Mhe. Waziri wa Elimu anajitahidi sana. Namshukuru aliona wingi wa wanafunzi wa Skuli ya Kihinani walikuwa wanasoma mpaka nje, tulivyojenga na Mhe. Mbunge Mhe. Waziri na timu yake walikuja kuimalizia ile skuli tunawashukuru sana. Tunaomba waendelee na mioyo ile kwa skuli zote ambazo tayari zimefikia kiwango cha kumalizia basi wazimalize. *(Makofi)*

Pia nimuombe Mhe. Waziri liko jengo la skuli moja la muda mrefu sana tena la ghorofa, hebu Mhe. Waziri aimalize ile skuli ya Donge. Jengo lile la Skuli ya Donge la muda mrefu sana na kwa Wilaya ya Kaskazini 'B' hakuna skuli ya ghorofa. Kwahivyo, ile wilaya nzima wanategemea jicho lao pale. Naomba iangaliwe sana afanye maafira yake limalizike lile jengo.

Nizungumzie miradi ya Wizara ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, tuna mashaka sana na mkandarasi au wakandarasi wanaochukua miradi ile hawamalizi vizuri. Serikali inajitahidi kuwapa kazi sasa hivi tunaona pale Bububu tayari wameshaanza nafikiri wakati wowote wanaanza kujenga, lakini hofu tu kwamba wasije wakatufanyia kazi ikawa sio kazi nzuri ya maana. Kwasababu fedha ni nyingi na pale pia ni eneo lenye wanafunzi wengi kwa hivyo ni pale kama walivyozungumza watu wengine kama Daya na kwengineko hata pale Maruhubi papigiwe chapuo, wanakwenda lakini Maruhubi pale Chuo cha Utalii wanatakiwa wasimamiwe kwa umakini waweze kumaliza lile jengo japo si kwa wakati lakini kwa ubora. Maana yake ukisema kwa wakati tu hawahewi lakini angalau kwa ubora unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara ya Elimu sikutaka kuchangia sana kubwa kuwapa shukurani zangu na kuwaomba kwamba huko majimboni tunajitahidi kuwasaidia kwa kujenga angalau msingi na mambo mengine, lakini watusaidie tumalizie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho katika wizara hii nalo mawili kama nilivyosema Wizara ya Afya. Kutarajia walimu wengi kustaafu kwa mpigo na kutokupata fursa ya kuajiri walimu wapya kwa mpigo. Wanapewa fursa za kuajiri lakini wanakuwa 100 au 200, lakini pengine wanatoka 1,000. Kwahivyo, hili Mhe. Waziri akae na timu yake waangalie katika miaka mitatu au minne ijayo mnatarajia walimu wangapi kustaafu na mpako kazi wa kuwaajiri utakuwaje. Lakini sekta ya elimu ni kuja na afya ni muhimu kuwa na tume ya uajiri yao wenyewe ili kuweza kuangalia. Katika jambo la ugatuzi kwa wizara zote mbili niwaombe la mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, yako malalamiko kwamba wale wafanyakazi wazuri wote wanabakishwa kule maeneo ambayo hayako ugatuzi. Wafanyakazi manunda wote ndio wanapelekewa kwenye ugatuzi zaidi wa Wizara ya Afya. Sijapata kwa Wizara ya Elimu ukweli niseme lakini zaidi kwa Wizara ya Afya. Wale maafisa wa afya wa wilaya wanasema hatuna mamlaka ya kuhamisha wala nini wizarani huko wanatuletea wale walioshinda wizarani ndio wanatuletea sisi huku, wengine wamegoma tumekwenda Pemba, wengine sijui wakaambiwa waende wapi hawataki kwenda, yaani inakuwa shida halafu kituo kinakuwa hakina mfanyakazi. Hebu na hili liangaliwe linafanyika vipi.

Mhe. Mwenyekiti, baaa ya hayo niunge mkono ripoti ya Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nikushukuru sana, sasa namwita Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na akifuatiwa na Mwenyekiti wa Baraza, Mhe. Mwanaasha Khamis.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu kufika hapa katika hali ya uzima, lakini nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa

Jamii ya Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa niwapongeze sana kwanza mawaziri wote wawili, lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya, nimpongeze Mhe. Waziri wa Elimu, hizi sekta ni muhihu sana katika jamii yetu. Naamini sitaki nimpongeze sana Mheshimiwa mawaziri wetu wanafanya kazi nzuri na wanajitahidi sana, lakini niwapongeze na watendaji wao wote wa Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya.

Vilevile, niipongeze sana serikali nianzie kwenye Wizara ya Elimu. Niipongeze sana serikali kwa juhudi zake kubwa sana iliyofanya kujenga skuli ya kisasa pale Bugugu ile skuli kuivunja kujenga skuli ya kileo. Kwahivyo, kilio kile kilikuwa cha siku nyingi na maombi yale niliomba tangu kipindi kile Mhe. Ali Juma Shamuhuna mzee wetu alikuwepo, lakini kwa sasa hivi utekelezaji umeanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kujenga skuli hii itasaidia sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye ukurasa wa 19 wa ripoti hii. Kwakweli, niseme katika programu hii elimu ya maandalizi ya msingi ni muhimu sana, lakini hapa tunaona katika programu hii katika ukurasa huu wa 19 programu hii inahusu utoaji wa elimu, maandalizi ya msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na moja.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni kubwa sana kwasababu miaka minne kwa wanafunzi ndio wanaanza kupata zile akili za kujua mila, utamaduni wetu husika na akili yake inaanza kibaolojia hasa pale mtoto ndio anaanza kukamata mambo yote, ukimkosa pale kuanzia miaka minne mtoto utakuwa huna mtoto wa taifa la kesho wala kumjenga akawa mwanafunzi mzuri kama ukimkosa hapa kuanzia miaka minne. Hii sasa hivi wamepewa wenzetu hawa wa Serikali za Mitaa ni ugatuzi huu. Kwahivyo, wana kazi kubwa na tuangalie sana. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ajitahidi sana kuwasaidia hawa wenzetu ili waweze kufanya kazi zao vizuri sana

katika huu ugatuzi hasa kuanzia skuli za msingi hizi kuanzia miaka minne.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 4 kwa ripoti yetu ya kamati na imeeleza. Namshukuru sana Mwenyekiti kwa ripoti yake nzuri sana na kaeleza mambo mengi katika ripoti yake hii.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 20 unasema kuongezeka kwa wanafunzi, madarasa katika skuli mbali mbali za maandalizi. Kwa mfano, tukitizama hapa ripoti ya kamati inasema madarasa watoto wanasoma 120, 200 mpaka 90, 80 ndio kidogo. Hili suala ni kubwa sana katika taifa letu na ukiangalia hata mimi Mhe. Mwenyekiti tukiangalia jimboni kwangu, sasa hivi Skuli ya Bububu inajengwa kwa hivyo wanafunzi wengi wamekuwa hamna skuli, lakini kuna skuli moja hii ya maandalizi iko kule Kibweni ni skuli ndogo sana lakini ukienda kutembelea skuli ile utaona huruma watoto wanavyokaa, watoto wanakaa chini halafu wanajibana sana darasa moja tu watoto 200. Kwakweli, hii inakuwa shida hata watoto hawa kusoma basi sidhani kama watakuwa na uelewa mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia tatizo hili la Skuli ya Kibweni Mwalimu Mkuu nampongeza sana mama yangu Bi Time anajitahidi sana, hata kupasisha watoto pia anajitahidi, lakini kazi kubwa nayo. Hata ukitizama uhaba wa walimu pia wanao, utakuta mwalimu mmoja anasomesha masomo mengi karibu yote mwalimu mmoja tu, uhaba wa wanafunzi tunao. Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti tuangalie sana suala la madarasa, hasa hii skuli ya msingi tuweke kipaumbele kweli kweli ili kujenga madarasa mengine haraka haraka, ili kuweza kuwasaidia hasa watoto hawa wadogo kuanzia miaka minne kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, pia ukiangalia ukosefu wa vyoo. Hili jambo ni aibu sana, tuangalie skuli zetu nyingi ukosefu wa vyoo upo hasa

ukiangalia maradhi, mara nyingi watoto hawa wanapata maradhi ya kipindupindu au maradhi ya kuambukiza. Kwahivyo, tuangalie sana tulipe kipaumbele suala hili la madarasa na vyoo ni kitu muhimu sana kwenye taifa letu kuwajengea mazingira mazuri watoto wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 22 nije kwenye hali hii ya matokeo yasioridhisha inayojitokeza yaani siku baada ya siku. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesikitika kuwa Zanzibar skuli nyingi zimekuwa na matokeo sio mazuri. Lakini niipongeze serikali sana kwa jitihada zake kubwa sana kwa kujitahidi kuwasaidia wanafunzi wetu hawa. Mhe. Mwenyekiti, huwezi kuilaumu serikali peke yake, hapa ukiangalia wanafunzi hawa watoto kuwahudumia kuna majukumu mengi, kuanzia mzazi mwenyewe anashiriki ukiangalia pia hususan jamii yenyewe, pia ukiangalia na hali ya kipato cha yule mzazi mwenyewe.

Kutokana na hali hiyo, utamkuta mzazi wakati mwengine anataka kumshughulikia mtoto wake vizuri, lakini kipato chake ni kidogo, ajira yeke ndogo, mtoto yule *automatically* anakuwa hata skuli hawezi kwenda kwa ajili ya mazingira ya nyumbani. Kwahivyo, hili suala tuangalie sote wazee na serikali pia na jukumu lake na jamii yote tusaidiane kwa pamoja. Ukiangalia suala hili la watoto, mtoto akitoka nyumbani sasa hivi kutoka kama Jimbo langu la Mtoni, kutoka kule kuja mjini inakuwa shida hasa usafiri Mhe. Mwenyekiti sida sana utawaonea huruma hawa watoto. Hivyo, ndio maana nimeanzisha usafiri huu mwaka wa sita au saba unaingia huduma hii naifanya na Mwenyezi Mungu ananisaidia sana nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwasababu ukiangalia yule mtoto atoke nyumbani aje skuli, kwanza anatakiwa nauli, hujui yule mzee fedha anazo au vipi, anampa mtoto wake nauli au hampi, mtoto anakwenda njiani kutafuta gari wakati mwengine pesa hana, sasa

inakuwa shida ndio maana yanakuja mambo mengi mpaka udhalilishaji unakuja hapa kwa ajili ya wanafunzi hao. Lakini wakipata usafiri watoto hawa kidogo...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, minong'ono imekuwa mikubwa, Mjumbe hasikilikani tunawapa shida wenzetu. Ahsante, endelea.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Kwahivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala hili la wanafunzi hawa ukiangalia ni lazima liangaliwe kwa ujumla na serikali pia iliangalie sana, ukitizama pia usafiri na mambo mengine changamoto ni kubwa. Kwahivyo, wazee nawaomba sana tushirikiane na serikali yetu kwa asilimia mia kwa mia, ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanakuwa salama na wanaendelea kwenda skuli kila siku kwa kushirikiana na serikali yetu kwa vizuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wa 30 huu, changamoto katika ripoti ya kamati tatizo kubwa ni uhaba wa walimu Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema fani mbalimbali. Sasa hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka sisi tuliposoma walimu walikuwa kidogo, lakini kuna walimu wanakuja ambao wanajitolea, lakini wanafunzi au wanafunzi walikuwa wanajitolea kutoka sehemu nyengine na kuja kutusomesha pale. Sasa hili liendelea kwasababu tukiwaangalia walimu tukiwaajiri wote serikali haiwezi, lakini tuanze kuwasaidia hawa wanafunzi ambao wanaojitolea kuwasomesha wanafunzi wengine.

Hili litaweza kusaidia kwasababu utakuta hapo uhaba wa walimu na kama walimu watakuwa hawapo skuli hawa watoto hata kusoma watakuwa hawaweze. Kwahivyo, tuiangalie sana idadi hii

kubwa sana ya walimu sasa hivi iliyokuwa hatuwezi kuwaajiri lakini na wanafunzi wengine wanakosa walimu.

Kwahivyo, naomba sana tutafute walimu wa kujitolea basi kwa muda, ili mpaka serikali iwaajiri walimu wengine, na walimu hapo kuna walimu wameshasomesha hawa ajira hawajaajiriwa, basi wajitolee kwanza kwa muda ili baadae waweze kupata ajira hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ripoti ya kamati pia hili tatizo la uhamisho katika ukurasa wa 30 kifungu namba (d). Tatizo la uhamisho Mhe. Mwenyekiti, leo mwalimu anapelekwa huku kesho anatolewa anapelekwa huku. Mimi naomba Wizara ya Elimu iangalie kwasababu ukimpeleka mwalimu kama Pemba familia yake iko hapa ni mwanzo wa kuivuruga familia yake, utakuta mama yuko kule, baba watoto wako huku.

Kwahivyo, naomba sana tuangalie kama huyu mwalimu anaishi Zanzibar basi apewe ajira yake hapa Zanzibar na kama kuna mwalimu anatoka Pemba apewe ajira yake kule kule kwasababu ikiwa hivyo itasaidia hata kukaa na familia zao, kuweka maadili na sehemu ile ambayo wanayoishi wazee itawasaidia kwa wanafunzi wao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Elimu iangalie kiundani kabisa haya mambo ya kuweza kuwawezesha walimu wetu wasipate kuhamishwa kila siku kwenda huku na huku. Lakini pia ukiangalia hawa walimu wetu ukiangalia kuhusu stahiki zao mbalimbali hawajalipwa posho zao hawajalipwa, nauli hawapewi zinazostahiki, mishahara yao ya zamani.

Kwahivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, hawa walimu nao watu muhimu kama walivyokuwa madaktari muhimu basi na hawa walimu muhimu tuwaangalieni kama hizi nauli zao angalau

wapate hizi nauli pia na hii mishahara yao pia iangaliwe kwa sasa kwa sababu wakiwa kama hawajapa mishahara mizuri hata kusomesha kwao kutakuwa kudogo sana kutakuwa hakuna muelewa mzuri na watakuwa hawana imani zaidi. Hivyo, naomba serikali aingalie sana suala hili la nauli na stahiki zao.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 31 huu Ugatuzi wa Sekta ya Elimu. Maeneo yaliyogatuliwa katika Sekta ya Elimu ukiangalia hapa gharama za chakula kwa wanafunzi skuli za maandalizi, lakini malipo kwa nauli walimu wanaosomesha maeneo ya mbali. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti tatizo kubwa tuliangalie kwa undani kama nilivyosema bila ya kuangalia hii changamoto ya nauli hawa walimu wetu usafikiri itakuwa shida hata kufika skuli hata kurudi itakuwa ngumu. Kwahivyo, naomba sana katika Ugatuzi huu na sasa hivi Serikali za Mitaa wamepewa majuku haya waangalie zaidi ya hawa walimu wawatizame usafiri wao wa kwenda na kurudi.

Lakini pia ukiangalia fedha za matengenezo madogo madogo za Skuli ya Maandalizi Mhe. Mwenyekiti. Skuli zipo nyingi lakini sasa kuna baadhi ya skuli bado hazijatengezwa wanafunzi wanataka kusoma. Lakini naomba sana Serikali za Mitaa hasa kwa Mkoa wangu wa Mjini Magharibi namuomba sana Mkuu wa Mkoa angalie sana hili suala ni lake la Ugatuzi. Kwahivyo, hizi skuli zilizokuwa hazijesha naomba zijengwe kwa haraka, ili wananchi wetu waweze kuzitumia vizuri waweze kufaidika na matunda ya nchi yao na mapinduzi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie kwenye Wizara ya Afya kidogo nimalizie haraka haraka katika ukurasa huu wa 9. Nije kwenye changamoto ya vituo vya afya viliopo. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia changamoto kubwa katika Wizara hii ya Afya ukiangalia kwanza madaktari kidogo, ukiangalia sana wauguzi pia kidogo sana. Lakini niiopongeze sana serikali wanajitahidi sana

kama nilivyosema mwazo. Nimpongeze sana Waziri wa Afya kwa juhidi zake kubwa na anajitahidi na Naibu Waziri anajitahidi sana niwapongeze sana kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia wauguzi kidogo tunao hiyo ni kweli hata ukienda Mnazi Mmoja ukifanya *survey* pale wauguzi tunao kidogo na wengine wanafanyakazi vizuri sana wanajituma usiku na mchana. Lakini wengine wanaharibu kwa makusudi wanafanya *sabotage* katika huduma hii, ili mambo yasiende tu sijui wana chuki zao za kisiasa au za mambo mengine. Lakini utakuta mambo yanakwenda vizuri lakini wao wanayaharibu kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Wakuu, Watendaji muangalie kama kuna watu wanatuharibia, kwasababu sisi tunakwenda kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumechaguliwa na wananchi kwa kura nyingi. Sasa wananchi wanataka maendeleo sasa kama kuna watu wanatuharibia Mhe. Mwenyekiti, tunaomba waondishwe au wasimamishe au wafukuzwe kazi kabisa. Kwahivyo, naomba uchunguzi uendelee ndani kwa ndani kwasababu sekta ya afya ni sekta muhimu sana na tukiharibu hapa Mhe. Mwenyekiti si serikali yetu mpaka chama chetu pia kitakuwa kimeharibu. *(Makofi)*

Kwahivyo, naomba sana tujitahidi sana katika suala hili zima la watendaji wetu kama wanafanya *sabotage* katika wizara au katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ama katika vituo vya afya vyote, basi naomba hawa wahudumu waondoshwe au wapumzishwe kabisa kwasababu hawana nia njema ya kutumikia wananchi wao katika taifa letu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 2 Serikali za Mitaa. Changamoto zilizojitokeza katika ukaguzi ndani ya sekta za afya.

Ukiangalia karipoti ya kamati inasema sasa hivi katika ugatuzi huu Madiwani wanahitaji kuelimishwa sana ripoti ya kamati imesema Mhe. Mwenyekiti. Madiwani bado hawajui nafasi zao hawajui nini wanafanya tunakuwa tunasukumana Mwakilishi atasema hivi, Mbunge atasema hivi, Diwani atasema hivi. Lakini wao kama Diwani hawajajua.

Kwahivyo, naomba sana Mhe. Waziri hawa Madiwani wapate elimu ya kutosha kwenye ugatuzi huo kwa kutumia Serikali za Mitaa, ili tuweze kufanya kazi vizuri. Lakini pia kuna uhaba mkubwa wa watendaji na madaktari na wauguzi kama nilivyosema changamoto ipo kuanzia chini kwenye vituo vya afya pia shida hii ipo. Mhe. Waziri naomba sana tuanze kuwasaidia hawa wenzetu wapate madaktari na wauguzi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme suala la madaktari .....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, bado dakika moja.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namalizia. Suala hili la madaktari Mhe. Mwenyekiti, shida kubwa ya madaktari tunayo sisi Zanzibar. Lakini naomba sana hawa madaktari kwa nini wasikopeshwe fedha wakanunua nyumba na gari yao, maana utamuona daktari hana hata usafiri, daktari anakuja pale anaokoa roho ya mtu lakini yeye usafiri hana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba wakopeshwe na Benki *PBZ* wanunue hata nyumba wakopeshwe ili mshahara wao kidogo kidogo waweze kukatwa halafu hawa madaktari wakikopeshwa hawawezi hata kukimbia kwenda nje ya nchi kufanyakazi sehemu nyengine watatumikia kwasababu wana deni hawawezi kuondoka.

Kwahiyo, naomba sana Mhe. Waziri aangalie sana suala hili la daktari wetu wapate kupewa kipaumbele cha kukupeshwa fedha. Lakini pia niseme ushirikiano mdogo baina ya Madawani na Wawakilishi kwenye majimbo hiyo kweli wapewe elimu hawa Madiwani wetu waweze kushirikiana vizuri na Wabunge na Wawakilishi kuisaidia sekta hii ya afya pia.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia changamoto kubwa hata fedha wanazopewa hii Serikali za Mitaa pia kidogo .....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemaliza.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia kwa mia wizara zote mbili kwa kazi yao nzuri kabisa nawapongeza sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana namwita mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ambaye atakuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa muhula huu.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache kwa sababu ni Mjumbe katika kamati hii nitakuwa sina mengi ya kuchangia labda ni kukumbusha tu katika wizara zetu hizi mbili ambazo tunazisimamia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi, changamoto nyingi zimetajwa katika ripoti yetu hii. Kwanza kabisa nimpongeze Mwenyekiti wetu wa Kamati ambaye kwa umahiri wake ameileta vizuri ripoti yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, mie nije moja kwa moja naipongeza Wizara ya Afya tumefanya nao kazi vizuri nachangamoto tulizoziona najua watazifanyia kazi.

Lakini, nije moja kwa moja katika Wizara ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara ya Elimu amelizungumzia Mhe. Machano Othman Said suala la majengo ya skuli zetu na kuhusiana na hizi kampuni zinazopewa tenda za ujenzi. Mhe. Mwenyekiti, katika kamati tuliliona hilo lakini mimi nilitaka niwakumbushe tu Wizara ya Elimu kwa mfano katika ubuvu wa skuli ile ya Madungu hii kampuni iliyojenga skuli ile imekubali kuwa itaifanyia ukarabati.

Kwahiyo, nilikuwa naomba wizara waifatilie kwa wepesi au kwa uharaka kabisa ili tuone ule ukarabati umefanyika kabla ya mvua za masika zinazokuja, ili kuwaondoshea usumbufu wanafunzi waliokuwepo katika Skuli ile ya Madungu. Naiomba sana wizara ifatilie huyu Mkandarasi kwa vile mwenyewe amekubali kuifanyia ukarabati.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima katika hilo hilo suala la skuli zetu. Kuna skuli za Wilaya zile za Sekondari ambazo zilidhaminiwa kwa mkopo wa *World Bank*, tatizo pia tulilibaini uvujaji wa mapaa mfano Skuli ya Utaani, Muwanda, Chasasa na nyenginezo. Skuli hizi pia nazo zinavuja lakini pia wakandarasi walisema kuwa wamepata maelekezo ya mshau elekezi ndio wakajenga vile.

Kwahiyo, nilikuwa naomba tu kuikumbusha wizara kuwa iangalie pale wanapopewa mapendekezo au michoro kabla ya kupewa yule mjenzi, basi wizara iangalie kwa umakini michoro ile kama wakiona haitafaa basi wafanye juhudi za makusudi kuona kwamba ile michoro haifai na wao wapendekeze michoro ambayo wanahisi inafaa, ili kuondosha ule usumbufu unaojitokeza katika majengo haya na kuona kuwa zile pesa za serikali zinakuwa zinafanyakazi vizuri na ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja katika suala zima la maslahi ya walimu. Mhe. Mwenyekiti, ili tupate mafanikio, pamoja na elimu bora lazima na walimu waangaliwe. Mhe. Mwenyekiti, niseme walimu waangaliwe katika Mkutano Mkuu wa tatu wa Chama cha Walimu hata Mhe. Rais wa Zanzibar aliliona hili na alilipendekeza kwa makusudi mazima kuhusiana na madai ya walimu kuhusiana na maposho pamoja na mishahara na mambo mengineyo yapatikane kwa walimu walimu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, walimu wana kazi ngumu tena wana kazi ngumu sana, serikali kama haijaangalia kwa jicho la upana wake basi kila siku tutaona kuwa tunapata matokeo mabovu kwa wanafunzi ni kwasababu tu mwalimu ana mazingira magumu. Lakini katika utendaji wake wa kazi anahitaji aangaliwe aonekane kama na yeye ni mwalimu katika ile fani anayosomesha. Kwahiyo, maslahi yao yakiboreshwa nafikiria walimu watakuwa vizuri katika ufundishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika uhaba wa walimu, katika ripoti imesema kuwa iundwe Tume Maalum. Kwahiyo, naomba serikali walione hili kama tulivyoshauri ile tume iundwe *especially* iwe kwa walimu tu, kwasababu nakumbuka tuko nilipoingia katika kipindi hichi suala la uhaba wa walimu unasemewa kila siku. Kwahiyo, naomba sana serikali ilione hili na walifatilie kwa umakini na ikiwezekana hiyo Tume ya Utumishi iundwe iwepo, ili wizara ione mahitaji yao ni kwa kiasi gani. Mahitaji ni mengi na mahitaji ni makubwa kuhusiana na suala zima la walimu.

Kwahiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali mimi sitakuwa na mchango mwingi ila nilikuwa nikumbushe wizara wayaone haya na wayafatilie kwa ukaribu zaidi, ili tufanikishe kuna msemo unaosema kuwa "Elimu Bora Kwanza" mara nyingi anazungumza Mhe. Waziri kwa hiyo iwe

elimu bora ya kweli kwa maslahi ya walimu lakini hata majengo na mazingira yanayozunguka katika upatikanaji wa elimu bora.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana mimi nilitaka niseme hayo machache. Lakini pia nawapongeza Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kwa mashirikiano makubwa waliyotupa pamoja na serikali kwa jumla na matumaini yangu katika ripoti hii zile changamoto ambazo tumezibaini watazifanyia kazi na majawabu yake itakapofika Septemba basi *insha-Allah* kila kitu watatuletea majibu sahihi na yale ya ufanisi zaidi. Nakushukuru sana Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe, kwakweli niwashukuru sana katika kutimiza wajibu wenu kuona kwamba ripoti yetu hii tumeichangia sana na bado tunaendelea. Wachangiaji bado wapo hapa mbele yangu ninayo orodha hapa.

Lakini, naomba niwataje ambao wataanza jioni wajitayarishe akiwemo Mhe. Suleiman Said Sarahan, Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Nadir- Abdul-latif Yussuf. Hao wataanza kuchangia lakini na wengine wako wanafuatia. Nawataja hao, ili waweze kujitayarisha na baadae watafuatia wengine.

Waheshimiwa Wajumbe, hadi hapa naomba nichukuwe fursa hii kuendelea kuwashukuru tena. Naakhirisha kikao hichi hadi hapo saaa 11:00 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 6: 55 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(*Saa 11 jioni Baraza lilirudia)*

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa majadiliano yanaendelea, mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia machache ripoti hii Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze Kamati hii ya Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika muda wote wa kazi zao. Mhe. Naibu Spika, kamati hii kama inavyojieleza hapa kwamba ni Kamati ya Ustawi wa Jamii, ambayo imezungumzia masuala mazima ya afya pamoja na elimu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze Wizara ya Elimu kwa kazi zao ambazo wanazozifanya pamoja na watendaji wake wote lakini pia niipongeze Wizara ya Afya pamoja na watendaji wake wote. Mhe. Naibu Spika, mimi nitaichangia hii ripoti kwa jumla. Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye vituo vyetu vya afya katika maeneo ya vijijini na mjini, vituo hivi vina changamoto nyingi na kamati hii imeweza kutembelea baadhi ya maeneo ya vituo hivi vya afya lakini pia wameweza kuyakuta mambo ambayo hayaridhishi katika maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya vituo haviridhishi lakini pia kuna changamoto kubwa ya dawa, vituo vingi vya vijijini dawa ni usumbufu au ni tatizo kwa jamii zetu inafika pahala wananchi wetu wanatulalamikia sisi viongozi wao wanasema kwamba, wanapofika katika vituo vya afya hivi kila wanapokwenda wanaambiwa dawa wakanunue. Kwa hivyo, naomba sana Wizara ya afya kupitia ripoti hizi basi waone kwamba hili ni tatizo na waone kwamba jamii yetu inapata tabu sana na ukitazama jamii yetu ni ya kinyonge.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile katika vituo vyetu vya afya kuna changamoto kubwa ya huduma umeme, Wizara ya afya huwa tunasikia kwamba kuna huduma ambayo wanachangia kwa kila mwezi lakini katika kituo changu cha afya cha Kitope huduma hii ya afya wanaipata shilingi 50,000/- kila mwezi. Lakini kwa kweli kituo kile kinafanya kazi usiku na mchana ni kituo ambacho kwa sasa kinatoa huduma ya

uzalishaji. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana inafika pahala sisi viongozi sasa tutowe huduma ile ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu waweze kuhudumiwa naomba sana wizara husika iwafikirie basi vile vituo vyote ambavyo vinatoa huduma masaa 24 waweze kuwaongezea posho la huduma ya umeme.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kuna suala zima la ulinzi katika vituo vya afya, Mhe. Naibu Spika, suala hili ni changamoto kubwa sana na wenzangu baadhi wameizungumzia changamoto hii na tuone kwamba wizara itambue imepata tabu sana na serekali kwa jumla imegharamika kununua vifaa ambayo vipo katika vituo vile, lakini cha kusikitisha vituo hivi havina walinzi. Nikisema tena kwamba katika kituo cha afya Kitope, kupitia uongozi wetu sisi mimi na Mhe. Mbunge tumejitahidi sana na tunahakikisha kwamba kila mwezi tunamlipa mlinzi. Tunaomba sana katika vituo vya afya vyote basi vipatiwe walinzi waajiriwe kama kawaida. (*Makofi*)

Lakini pia kuna kitua cha afya ambacho kituo kizuri tu kimejengwa katika kijiji cha Mgonjoni ambacho kwa sasa hakina mlinzi, naomba sana wizara husika kikitazame sana kituo hichi cha afya cha Mgonjoni na wao waweze kupatiwa mlinzi kwani kijiji kile kiko katika maeneo hatarishi.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Wizara ya Elimu niipongeze sana Wizara ya Elimu kwa kweli wanajitahidi sana kufanya kazi na tuone kwamba elimu ni ufunguo wa maisha na tunatakiwa watoto wetu waweze kupata elimu bora. Lakini kuna changamoto mbali mbali ambazo wameziona wanakamati na wameweza kutuwasilishia katika ripoti hii na tunasubiri majibu mwezi wa tisa basi wizara ije ituletee majibu.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwa jumla kwamba katika Wizara ya elimu au katika elimu kwa jumla kuna changamoto na changamoto hizi mimi nitazizungumzia baadhi tu ya changamoto. Mhe.Naibu Spika, ili tukikataka mafanikio katika *program* ya elimu basi tujipange na kutafuta mikakati ambayo itaweza kutekelezeka kwa *program* hii.

Mhe. Naibu Spika, tutazame kwamba changamoto ya wototo wetu ambao ni watoto ongezeko la wanafunzi na uhaba wa madarasa. Mhe.

Naibu Spika, ili suala ni kwamba tunalifahamu sote kwamba kila mwaka wanafunzi wanaandikishwa lakini na waliopo madarasani ni wengi na madarasa ni kidogo. Naomba sana Wizara ya Elimu kupitia ripoti hii tunaomba sana yale madarasa ambayo wananchi wenyewe wamejitolea kuyajenga basi tunaomba sana kupitia bajeti ya mwaka 2017/2018 itakapomalizika basi tuone kwamba majengo yale yamemalizika ili wanafunzi wetu waweze kusoma.

Mhe. Naibu Spika, kuna mkakati mwengine ambao napendekeza kwa wizara kwamba tatizo kubwa la walimu, kwa kweli katika maeneo yetu mengi hususan Mkoa wa Kaskazini tuna walimu wachache sana na changamoto hii inapelekea wanafunzi wetu kufeli. Utakuta skuli nzima ina walimu watano na watano hao inawezekana wawili wako masomoni watatu wamebaki katika skuli hiyo. Kwa kweli suala hili ni changamoto kubwa sana Mhe. Naibu Spika, naomba sana wizara husika ifikirie na itafute ifanye utafiti katika maeneo ya skuli zote na iangalie kwamba kila skuli ina changamoto ya walimu wa aina gani tuone kwamba basi kama kuna skuli zimeongezeka walimu wapunguzwe wapelekwe katika maeneo mengine na kama haiwezekani basi waajiriwe walimu wengine ili waweze kuziba mapengo yale.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niseme kwamba kuna changamoto katika baadhi ya maeneo ya skuli nyengine changamoto ya vyoo, katika skuli ya Mgambo Jimbo la Kiwengwa kwa muda mrefu wana kilio kikubwa sana cha siku nyingi ambacho cha vyoo, vyoo mwanzo vilikuwa havitoshi lakini na pia kwa sasa haviwezi kutumika tena kwa kweli na tunakokwendea sasa hivi ni kipindi cha mvua naomba sana tushirikiane pamoja kupitia sisi viongozi wa jimbo pamoja na wizara husika ili tuhakikishe suala hili linatekekelezeka.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba lakini pia tuone mazingira, mazingira ya watoto wetu katika maeneo mengi ya skuli zetu za Unguja na Pemba tutazame maeneo yalivyo mazingira na wanafunzi maeneo wanayotoka na maeneo ambayo wanakwenda kutafuta elimu. Mhe. Naibu Spika, hii ni changamoto sana, naomba sana Wizara ya Elimu ipite katika maeneo ya skuli na iangalie basi maeneo hususan wanafunzi wanaotoka sehemu mbali mbali.

Kuna wanafunzi wanatoka katika kijiji cha Kipandoni wanakwenda aidha waende skuli ya Kiwengwa au skuli ya Upenja ukitizama vitoto viko vidogo na masafa ni marefu kwa kweli naomba sana Wizara husika ya elimu ilitizame suala hili na pia liweze kutolewa ufafanuzi au litazamwe kwa kina na wao waweze kupata elimu bora ya elimu hii.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa niseme kwamba naunga mkono Ripoti hii ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa asilimia mia moja na pia niungane mkono na wajumbe wenzangu walionitangulia nikushukuru sana. Ahasante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa sasa basi nimpishe Mhe. Suleiman Sarahan Said atafuatia Mhe. Nadir Abdul-latif.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia machache ili kuweza kukamulisha taarifa za kamati yetu hii ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nianze na sehemu ya pili katika Wizara ya Afya. Mheshimiwa Wizara ya Afya kwa mujibu wa jaduweli hili tulilolipata ina progamu nne ina programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Programu ya Tiba, Programu ya Usimamizi wa Sera ya Afya na Utawala. Lakini ina pia programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa muundo huu ina idara zisizopungua nane kwa tisa ina-

1) Idara ya Mipango Sera na Utafiti
2) Mipango Endeshaji na Utumishi
3) Idara ya Kinga na Elimu ya Afya
4) Idara ya Huduma za Hospitali
5) Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja
6) Idara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
7) Idara ya Mfamasia Mkuu wa Serikali
8) Idara ya Bohari Kuu wa Dawa
9) Ofisi ya Afisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba

Pia ina-

1) Maabara ya Afya ya Jamii Pemba

2) Bodi ya Chakula na Dawa na Vipodozi
3) Baraza la Wauguzi wa Wakunga
4) Bodi ya Ushauri wa Huduma za Hospitali Binafsi

Mhe. Naibu Spika, hapo zamani palikuwa na Wizara ya Afya na mambo yote yalikuwa yakienda vizuri sana katika sekta mbali mbali ambazo zilikuwa zikiunganisha mpaka maeneo tuliyokuwa tukiita kwa bahati mbaya lakini ndio tuseme matopasi wote walikuwa katika wizara na usafi wa miji na ustaarabu wa miji ulikuwepo. Usafi na ubora wa chakula ulikuwepo na mambo mengine ya tiba yalikuwepo.

Mhe. Naibu Spika, tumeunda idara nyingi sana lakini kila mmoja wao huyu angekuwa amechukuwa wajibu wake wa utekelezaji wake basi serikali wala isingekuwa na tatizo kubwa sana. Lakini idara ya nyingi mambo ni mengi na utekelezaji wake ni mdogo sana, hapa ndio tunapokuwa tunatupiana paka wa uso kila mmoja anamtupia mwenzake pale si kwangu hapa ni kwangu.

Sasa idara zote hizi zilizopo kama zinaonekana bado nazo hazijaweza kufanyakazi basi zipunguzwe tufanye ugatuzi ili zile nyengine zifanye kazi zaidi. Maana yake inaonekana zikiwa nyingi ndio kabisa. Mhe. Naibu Spika, nitoe mfano tu peleleza wachezaji wa kawaida wa mpira wa miguu wanakuwa kumi na moja kwa kumi na moja sasa mmoja atolewe kwenye timu nyengine waangalie wale kumi wanavyofanya kazi na ile timu nyengine ikafungwa kwa wale kumi. Sasa inaonekana idara zinapokuwa nyingi na vyombo vinapokuwa vinaingiliana kila mmoja anamtupia mwenzake paka wa uso na matokeo yake maharibiko yanapatikana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeziona sana hizi idara zikafanya wajibu wao ili kuweza kuwatumikia wananchi kama serikali ilivyokusudia. Hilo Mheshimiwa nilikuwa nianze nalo.

Mhe. Naibu Spika, nimesoma katika jadala hii ukosefu wa wafanyakazi katika maeneo mengi ambayo Mhe. Naibu Spika, sehemu ya afya si sehemu ya kuifanyia masihara ya kwamba daktari hayupo. Ile ni sehemu ambayo Izrail yuko karibu na wewe hata kama huku nje yuko lakini kule ndio anakotembelea zaidi. Mtu anapopelekwa hospitali anakuwa

katika mazingira ya saa zote uso wake hautanabahi mpaka anapoambiwa atoke leo ende zake hata kama anatoka akiwa bado hali mbaya lakini anaona kama amepata nafuu. Sehemu ya Hospitali si sehemu ya kuchezea Mhe. Naibu Spika.

Leo nataka nizungumzie Abdalla Mzee Hospitali kwa ripoti iliyomo humu si maneno yangu. Abdalla Mzee Hospitali tumeijenga kwa sifa nyingi sana kwa gharama nyingi sana ni hospitali ya kupigiwa mfano. Ni tafauti na maneno tuliokuwa tukiambiwa na maneno yalipo hivi sasa, Abdalla Mzee unakwenda uaambiwa madaktari hawapo unaambiwa wengine wamefika pale wamekuja tu kuzunguka *round about* wameondoka, wengine wanasema mazingira yale hawawezi kuishi yale mazingira ya Mkoani hali ilivyo, maana ikifika jioni tena wewe ni ndani tu hakuna pahala pa kutembea. Lakini huu ndio mtindo wetu wa kisasa ikifika saa kumi na mbili ulale. Sasa wafanyakazi wengine ndio matatizo yamekuwa kama hayo.

Lakini cha zaida kamati imesema imewaona wafanyakazi watatu tu wa usafi. Hivi jengo kama lile lina wafanyakazi watatu kwa maneno ya kamati litakuwa kweli na usafi utapatikana na kuna maeneo mengine wamesema hayasafishwi kabisa.

Ningeiomba sana serikali ikafanya jitihada zote kutokana na umahiri wa hospitali ile, ukubwa wa hospitali ile, upya wa hospitali ile ama ikatafutwa kampuni ambayo inaweza ikasafisha hospitali ile hata kikianguka kisheti ukaweza kukichukuwa na kukila. Ile hospitali kwa kweli Mheshimiwa sifikirii kuja kujenga tena karibuni. Sasa si kitu cha kuchezea sana. Ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, ikatizamwa kwa jicho la huruma sana ile hospitali mambo yaliopo. Kwa hivyo, naiomba wizara ikaitizame hospitali.

Lakini hospitali ile Mheshimiwa kwa kweli ukiachia masuala mengi ambayo tunategemea na vifaa vilivyopo mimi sikutegemea tena kama kutakuwa na wagonjwa ambao wataondoka Pemba kwenda Dae- es Salam au kuja Unguja kwa matibabu. Sijui madhumuni ya ile hospitali na malengo tuliyopewa hospitali ile kwamba sasa watu walioko Pemba hata akiondoka pale anakwenda India labda. Lakini kwa maeneo ya nchi hii alikuwa hana hapala pa kwenda. Lakini siku zote wagonjwa

wanasafiri kutokana na hospitali haijatimia viwango vyake vilivyokusudiwa. Ningeomba sana serikali ikalitizama hilo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo niangalie tena kwenye uwajibikaji wa familia katika kutekeleza sheria za mzazi. Mhe. Naibu Spika, matatizo makubwa yanayotupata katika sehemu nyingi sana ukitizama za afya na kila kiti ni mama na mtoto. Mhe. Naibu Spika, serikali bado haijakamata kisawasawa katika suala la wanaume inawaachia wanawake wenyewe katika masuala yao matokeo yake watoto wote wanawaangukia wanawake na dhahama zinaanza hapo mama hajui mkumpeleka hospitali mtoto, mama hajui mtoto alimelee vipi, Ustawi wa Jamii hapo unapotea hapo inakuwa ni kashehe mama kumuacha mwanawe hawezi, kumlea hawezi matokeo yake sasa tunatengeneza matatizo chungu nzima ya watoto.

Mhe. Naibu Spika, serikali ningeishauri sana matunzo ya mtoto ni fedha, matunzo ya mtoto si lazima baba awepo kama akeshakuwa hataki basi. Lakini ningeomba kwa Wizara hii ya Ustawi wa Jamii kwa kupitia Ustawi wa Jamii, wazazi wote waliokuwa na watoto waliokuwa hawashughulikii na wengine ni wafanyabiashara wengine ni wafanyakazi wa serikali, sheria ikatumia mkondo wake, fedha zikachukuliwa wakapelekwa wale watu wa watoto ambao wamewatupa kule kwenye maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, kama suala hili tutaliwacha tutangeneza watoto waliokuwa hawana desturi nzuri, hawana heshima na wazazi wao wamewakosa kabisa na pia kuna wengine wanakufa kati kati kwa sababu hawana uwezo wa kwenda kutibia baba hana habari hata ukimwambia mtoto anaumwa matokeo yake mama anashindwa kufanya kila kitu. Tunawakosa watoto kutokana na sababu nyingi za kutokuwa na uwajibikaji katika kulea watoto.

Mhe. Naibu Spika, niende kidogo kwenye wazee sasa. Mhe. Naibu Spika, sisi kama watoto tunalelewa na tukifika pahala katika mambo yetu tunafika mzee nae anataka kulelewa. Mhe. Naibu Spika, katika jumla ya mambo ambayo huko mitaani yapo pia watoto wanawatupa wazazi wao hawawalei, hawawasaidii na bado serikali haijachukua hatua yoyote kwa wazazi hao, hata wale tunaowapeleka katika maeneo

ya kusema wanakwenda kuwekwa wazee katika sehemu zile, watoto wao ambao wamewazaa wao hawalazimishwi kwenda kuwaangalia wala kuwasaidia. Kwa sababu serikali inapiga kelele kuhusu mzazi amshughulikie mtoto, lakini kwa nini mtoto asimshughulikie mzazi wakati hajiwezi tena na bado sheria nyengine zipo, lakini serikali bado haijakazania sheria hizo zikaweza kuwakamata kabisa wale ambao wanakwenda kinyume na maadili ingawa hawajifahamu, wakiachia mambo kwamba sio tu kwamba ni mambo ya serikali, lakini hata Mwenyezi Mungu hatowaacha. Kwa sababu mzazi ni mtu mkubwa sana katika dini, lakini pia anakua kutokana na hulka zake anakua hapati usaidizi wa mtoto na mtoto hajui kama pale kutakuwa kuna pepo yake, lakini kuna radhi zake na wengine inakuwa maadili yamewatoka. Kwa hivyo, serikali sio vibaya ikachukua hatua za kuwafahamisha kwa nguvu au ikiwezekana kwa hiyari, lakini suala lile likawezekana.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende tena kwenye elimu. Mfumo tunaoutumia kwenye elimu mimi unanipa tabu kwenye kichwa. Sisi tumezungumza hapa kwamba elimu ya lazima iwe darasa la kumi na mbili, ndio mfumo ambao nilikuwa nausikia. Lakini sasa kuna mfumo ambao umeshika kasi wa darasa la saba na darasa la kumi ambapo mtoto wa darasa la saba aki-*fail* anakwenda *out*, mtoto wa darasa la kumi aki-*fail* anakwenda *out* huyu mtoto huku nyumbani anakwenda kufanya nini.

Mhe. Naibu Spika, sisi zamani tulipokuwa tukisoma mitihani ilikuwepo, lakini humtoi mtoto unamrudisha tu au unambakisha darasa ili mwakani aendelee kujiendeleza, akifika darasa la kumi na mbili mtoto atakuwa ameshajikamata angalau anaweza kuangusha nazi, unaweza ukamtuma dukani. Mtoto wa darasa la saba au darasa la kumi hafai hata kumwambia nenda hapo nyuma kanichukulie jembe hajui lolote. Leo yule unamrudisha nyumbani na wala hakuna misingi mizuri tunayomjengea kama mtoto yule akiondoka pale atakwenda wapi. Kwa hivyo, ningeomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikalitizama hili, ni watoto wangapi ambao tunawatengeneza wa darasa la saba na darasa la kumi ambao hawana pakwenda. Sisi tulisema msingi wa elimu ya lazima iwe darasa la kumi na mbili, sasa hivi elimu ya lazima darasa la saba, elimu ya lazima darasa la kumi. Kwa hivyo, ningeomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na yote nitaendelea tu. Hawa watoto tunawapeleka wapi. Kwa hivyo, ningeiomba sana wizara ikalitizama hili, leo mtoto anaambiwa hupati kurudia mitihani imeshatoka, huu sio msahafu, hii ni *system* na mipango ambayo tunaweza tukaitizama watoto hawa tutawapeleka wapi. Mhe. Naibu Spika, wewe ukiondoka nyumbani unataka mtoto wa darasa la kumi na mbili unampeleka pahala angalau ana akili timamu ameshatimia miaka 15 au 12 anakwenda, lakini mtoto wa miaka 10 au 12, hata elimu yake na hicho kichwa chake bado. Hata humu kwenye sheria zetu tumeandika mtoto wa miaka 12 bado hajakuwa timilifu, lakini leo tunamgeuza huku huku kwamba huyu ka-*fail* mitihani abakishwe nyumbani.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana hii wizara ikatizama kwa jicho la huruma sana watoto ambao wa darasa la saba na darasa la kumi, mitindo mingine Mhe. Naibu Spika, tusiifuate kama haina faida na sisi. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan, mchangiaji anayefuata sasa hivi ni Mhe. Nadir Abdul-latif, ajitayarishe Mhe. Khadija Omar Kibano.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahman Rahiym.* Mhe. Naibu Spika, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa wazima sote, lakini nikupongeze na wewe kwa kunipatia nafasi hii kuwa mtu wa tatu leo kuchangia. Kwa kuwa wizara hizi mbili ni nzito na nyeti, na wizara hizi zote zinagusa wananchi wote kwa jumla ndani ya Unguja na Pemba. Kwa hivyo, ningeomba kuwapongeza mawaziri wote wa wizara hii, Manaibu Waziri, watendaji wao na wafanyakazi wote kwa jumla kwa jitihada zao wanazozichukua. Lakini bila ya kusahau kwamba tumpongeze sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake zote anazohakikisha kuziimarisha wizara mbili hizi, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wizara hizi hata nikipewa mimi zinaweza zikanishinda kwa sababu ni wizara nzito na zina majukumu makubwa katika nchi. Lakini nikisema hivyo sio kwamba tena tuanze kulewa au tuanze kujisahau, tunatakiwa tujitahidi tufanye kazi kwa jitihada, watendaji wote wenye majukumu yao wafanyekazi kwa uweledi wajuwe kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali halafu niingie Wizara ya Afya. Kama nilivyosema kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanajitahidi sana na Mhe. Rais anajitahidi sana kwa kupitia Mhe. Makamu wa Rais wetu kutekeleza miradi mingi ya kujenga mashule na kufanya vitu vyengine vya kuleta elimu nzuri katika nchi yetu. Ninachoomba zaidi ni kwamba wajitahidi sana kwenye kuboresha mazingira ya mashule yote vijijini na mijini, kwa sababu shule sehemu hasa za maeneo ya shamba ziko taabani sana.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, tunafahamu jitihada zake na hasa Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wanajitahidi sana. Kwanza jambo moja kwenye ajira, tungeomba wawafikirie wale wote ambao walijitolea bila ya malipo kufanyakazi kwa muda mrefu kwenye ualimu, wakawapa kipaumbele wale kuwachukua wakati inapotoka ajira, halafu wawafikirie wepi ambao wame- *apply* kwa njia nyengine.

Mhe. Naibu Spika, la pili, mashule mengi yanavuja tunaomba mjitahidi sana ikiwa kwa njia ya maombi au njia yoyote, ilimradi shule zitiwe mabati, mtowe vifaa vya *equipment* za mambo ya *chemistry*, mambo ya *laboratory* na vifaa vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki kuzungumza sana kwenye mambo ya elimu kwa sababu mimi sio fani yangu, lakini nitazungumzia kwa ujumla kwamba wahakikishe kwamba mazingira haya yako vizuri, wanafunzi wanapata masomo vizuri na hasa kwenye *syllabus* vitabu ambavyo wanavitumia wahakikishe nchini vinakuwepo na visiwe pungufu au viwe havipo.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningehimiza zaidi pia kwa upande wa jimbo langu katika shule zangu ambazo hazijamaliza kama shule ya Kandwi, Pwanimchangani na shule nyengine ambazo hazina hali sio nzuri, ningemuomba Mhe. Waziri katika bajeti yao inayokuja safari hii basi waweze kulifikiria jimbo langu kuja kuimarisha, kwa sababu wananchi wangu wamejitolea sana katika kujenga na kujitolea katika hali nzuri, ili mje muwasaidie.

Mhe. Naibu Spika, mimi natoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, nakwenda Wizara ya Afya. Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya. Kama nilivyosema wizara hizi nzito na kawaida anapoharibu Mhe. Waziri, anakuwa kaharibu Mhe. Waziri, anapoharibu Naibu Waziri anakuwa kaharibu Naibu Waziri, lakini tusiwe na fikra mbaya, au tusiwe na *vision* mbaya au kutaka kumsingizia mtu kitu ambacho hajawahi kufanya au sio nafasi yake. Hatuwezi Mhe. Waziri wa Afya kafanya manyago halafu tukamlaumu Mhe. Rais au Mhe. Makamu wa Rais, tutamlaumu Mhe. Waziri. Lakini tufahamu katika utendaji mzima wa masuala ya afya wanaoharibu ni watendaji hawa ambao wenye majukumu yao, sio Mhe. Waziri au Naibu Waziri, sio Katibu Mkuu wala sio wakurugenzi kila mmoja na majukumu yake Wizara kama zile zenye wafanyakazi zaidi ya 30,000 au 40,000 huwezi kumrushia mpira mtu mmoja au wawili kwenye wizara, huwezi kumlaumu Mhe. Rais wakati yeye kazi yake ni kutoa fedha, kusimamia, kutoa ushauri na vitu vyote anavifanya. Sasa kama linatokea jambo ambalo sio zuri basi wakulaumiwa ni watu wa chini.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri, mbona Zanzibar hatuoni mtu kutumbuliwa manyago yanayofanyika, hasa kwenye wizara yako kila siku naona unakuja kulaumiwa hapa hatuoni *action* yoyote mnayochukua, hebu anzeni kutumbua hawa watu wakorofi wanaofanya mazingira mabovu. Juzi mmeona kakatwa mtoto mkono, siku za nyuma huko nasikia watu wanapigwa sindano pengine ya malaria anakwenda kupigwa ya pumu, ni vitu ambavyo havina maana hivi, anzeni kufanyakazi mawaziri kwenye *department* zenu, kwenye *ministry* zenu tumbuweni tujuwe nani anafanyakazi na nani hafanyikazi, aliyekuwa hataki kufanyakazi basi mtoweni, anayefanyakazi mwacheni aendelee na kazi kuna wananchi tele nje wanataka kazi ajira ngumu hawapewi. Sasa hivi imefika wakati wa kuona *action* inakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningempongeza sana, wizara hii ina daktari yule aliyetoa ripoti za mtoto aliyelawitiwa. Huyu aliyelawiti ni Hassan Aboud Talib maarufu, Kiringo ningewapongeza sana wizara hii kwa ukweli wao wa ripoti ile kwamba hawajajali huyu mtu nani, kama anafanyakazi wapi ana jamaa yake mkubwa nani hajajali kabisa. Wizara ningeomba muendelee na uweledi wenu, fanyeni kazi huyu mtu atashikiliwa na sisi Baraza la Wawakilishi tuko pamoja na kamanda wa polisi na viongozi wenzake wote wa chini waliosimamia suala hili. Mhe. Naibu Spika, bila ya Wizara ya Afya kama hawajawa wakweli basi ushahidi ule na suala hili lingekuwa jepesi sana. Tunamshukuru Kamanda Hassan Nassir kwa kupitia Wizara ya Afya na hasa daktari aliyetoa ripoti kakubali ni kweli limefanyika, na huyu mtu ni maarufu. Nitahakikisha tutakula sote sahani moja, hatuwezi tukamuona mtu kwamba yuko serikalini labda mtu ana watu viongozi kwamba aachiliwe, hatuwezi kuona hivyo kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi hata aje afanye ndugu yangu baba mmoja, mama mmoja kwenye suala kama hili, basi sitokwenda kuchukua dhamana wala sitomfuata mtu yeyote kuomba. Lakini nashangaa leo yanatokezea mambo kama haya basi unayakuta magari ya mawaziri ndani ya Kituo cha Polisi. Magari ya Mawaziri kazi yao kufanyakazi za wizara sio kwenda kuwachukulia watu dhamana au kwenda kutetea mambo ya uhalifu, ya ulawiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Rais suala hili alisimamie na sisi wawakilishi tuko macho, kiongozi yeyote atakayejaribu kwenda kufutisha kesi ile ambayo itakuwa ina ukweli wake baadae utatangazwa kama ulivyowekwa hapa, kwamba inaendelea kufuatiliwa zaidi, basi tutakuja kumtaja kwa majina mmoja mmoja. Tunachotaka kuona Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto tunawapongeza na wao wamefuatilia hili suala kwa ukaribu, lakini pia Wizara ya Afya kwa upande wao, Polisi kwa upande wao na watu wengine. Kwa hivyo, hatuwezi kuona sasa hivi tunapitisha sheria tu halafu watu wanazidharau. Mhe. Waziri wa Afya endelea hivyo hivyo, akiletwa mdogo wake labda kama katokezea katika upande wa familia ya Nadir Abdul-latif kafanya manyago mtajeni, upande wako wewe atajwe, ikiwa wa kiongozi yeyote ndani ya nchi hii atajwe. Hatuwezi

kuwaona wananchi wanyonge watoto wao wanalawitiwa halafu tukakaa kimya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tumesikia huko kwamba Kamanda Hassan Nassir kafika kutukanwa, kafika kuambiwa anajifanya Mungu mtu kashambuliwa kwa kutishwa kwa maneno kwa ajili ya kumtoa mtu yule. Lakini mimi ninachosema hapa mbele na Mwenyezi Mungu ananisikia, hatotoka kama kafanya kosa hili hata ende nani. Hatuwezi tukachukuliana nambo haya kwa wepesi watoto wanaharibiwa. Mtoto wa miaka 13 hii taarifa kwenye gazeti. Mtoto wa miaka 13 anaingiliwa na mtu mzima, huyu mtu ana *record* mbaya tokea miaka hiyo sisi wadogo, ameshafika mpaka kuowa wanaume wawili nani asiyejua hapa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana nchi nzima kwa ujumla, hili liwe ni fundisho na yeyote atakayekuja kufanya hatutomuachilia. Hata mimi Mwenyezi Mungu aniepushe, lakini nikija kufanya jambo lolote nisiachiliwe na wala asionekane mtu yeyote kwenda kunichukulia dhamana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningeomba wizara hizi zote zifanye kazi na hasa watendaji wa chini, kwa sababu mawaziri wapo juu, Manaibu Mawaziri wapo juu, Makatibu Wakuu wapo juu. Kwa hivyo, tungeomba fuatilieni hakikisheni kila anayefanya makosa mnamtumbua anachukuliwa adhabu na hatutakikuwaona watu ambao wanawadhulumu watu, wanalipwa mishahara kwa nini wasifanye kazi na kama ni hivyo wapo wananchi tele wapeni kazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi naendelea tena kusema kwamba naunga mkono ripoti hii na nimesahau sana kumpongeza mwenyekiti wangu, kwa sababu leo nimeingia na mambo mengine. Nampongeza mwenyekiti sana na kamati nzima, ripoti hii kaisoma karibu saa nzima ili watu wapate wafahamu nini ukweli uliopo humu ndani na ni vizuri zaidi kwamba azungumze ukweli usifichike. Tunakupongeza sana Mhe. Mwinyihaji Makame, pamoja na hao wenzako wote mliofanyakazi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini ningeomba Hospitali ya Mnazi Mmoja *CT Scan* na zile mashine ambazo hazifanyi kazi, Mhe. Waziri wa Afya ni aibu kuja kuona Hospitali ya Mnazi Mmoja haina wakati Al Rahma inayo na Global inayo. Hivi kweli watu binafsi watashirikiana na serikali, wananchi ni masikini hawawezi kwenda kulipa shilingi 200,000 *CT Scan*. Kwa hivyo tungeomba mashine zile kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Hospitali yetu angalau ziwepo mashine mbili mbili, ikiharibika moja basi moja inafanyakazi, wanaokwenda pale ni masikini. Leo tunaambiwa sisi wawakilishi wa majimbo, sawa tutachangia. Je, kama wameumwa watu 10 au 20 fedha hizo tutazitoa wapi, mfuko wa jimbo mpaka leo hatujapewa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango sijui atatupa lini, pesa sijui tuzitolee wapi mambo yako taabani.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakushukuru, tumuombe Mwenyezi Mungu nchi yetu iende kwa salama. Lakini nimefurahi sana kwamba safari hii tumeanza kuona kwamba sheria inafuata mkondo wake, hakuna mkubwa wala hakuna mdogo. Tutasimama kidete hapa na sote tuko macho tunafuatilia kesi hizo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana Mwenyezi Mungu akujaalie afya. *(Makofi)*

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante sana nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo na mimi nikapata mawili matatu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema na amani kunijaalia nikasimama hapa na nikawa na kauli ya kuzungumza leo katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mwenyekiti wa kamati na wa pili nawapongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Waziri wa Afya katika kamati hii. Moja kwa moja niende katika Vyuo vya Amali vya Unguja na Pemba cha Daya pamoja na cha Makunduchi. Vyuo hivi bado mpaka sasa hivi havijafanyiwa kazi yake vinavyopaswa, kwa sababu bado ujenzi haujaendelea.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Mtambwe Daya mpaka sasa hivi kiko *foundation* tu na hiyo *foundation* yenyewe haijamaliza kufukiwa. Mhe.

Rais katika ziara zake zilizopita alitoa agizo lake la kuwa hivi vyuo vifanyiwe kazi, lakini mpaka sasa hadi leo havijafanyiwa kazi yake, sijui limekwama nini katika agizo lake hili Mhe. Rais alilolitoa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende katika ajira ya walimu. Kuna wimbi kubwa limejitokeza kuhusu ajira za walimu na wengine waliostaafu wengine wameshafariki. Mpaka sasa bajeti bado haihitaji kupangiwa bajeti nyengine mpya ya fedha, mishahara ya bajeti hii ipo. Je, ni kikwazo gani kinachokwaza kutokana na ajira hizi za walimu na hivi sasa ni changamoto kubwa hasa skuli za *primary* na sekondari hasa Pemba. Mimi ndani ya jimbo langu hizo nafasi zilizotoka mbili tatu mlizokuwa mmeshazigawa, wamekwenda walimu kuomba nafasi na hakuna mmoja aliyepewa hata nafasi moja katika skuli zangu na kuna usumbufu mkubwa sana wa walimu, hasa Skuli ya Uondwe hakuna walimu wa aina hata moja, kwa sababu walimu wengi wa *primary* wameshastaafu pale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja katika masuala ya udhalilishaji. Suala la udhalilishaji Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali mimi nina kilio cha masuala ya uzio wa maskuli. Changamoto kubwa inayotukabili wanajamii au na walimu, ni kuwa hizi skuli mbali mbali zilizopo Pemba na Unguja bado baadhi yao hazina uzio, ndio changamoto hasa inayochangia kwa wanafunzi kutoka na kutoroka maeneo hayo kwa kupenya penya humo, wakawa wahalifu wamo pembeni wakaanza kuwahujumu wanafunzi hao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano mdogo hivi karibuni kuna skuli ya Kitope kuna wanafunzi watatu kwa wanne, ikiwa mmoja ni mwanamme na watatu ni wanawake wakiwa ni wanafunzi wa darasa la pili na la tatu. Kuna mlinzi mmoja wa kanisa aliwafanyia unyama watoto hao na mlinzi huyo akakamatwa kapelekwa kwenye Kituo cha Polisi, lakini ametolewa, sijui hadi sasa wazazi wanalipigia kelele na watoto hao walidanganywa kupewa rangi za kutumia skuli, peremende na pesa. Kwa hivyo, suala hili jamani waziri namuomba au ushauri wangu nazungumza kuhusu habari ya uzio kwa skuli zilizokuwa hazina zitengenezwe uzio, ili wale wanafunzi watakuweko pahala pamoja hata

walimu katika kuwashughulikia wanafunzi watakuwa na upeo mkubwa kuweza kuwadhibiti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sina zaidi isipokuwa hayo, naunga mkono hoja hii na mimi kuchangia mawili matatu niliyokuwanayo. Ahsante sana nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Khadija Omar. Sasa nimpe nafasi Dkt. Makame Ali Ussi akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuchangia katika Kamati hii ya Ustawi wa Jamii. Kwa kweli kwanza nachukua hatua ya kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii kwa kazi nzuri aliyoifanya, amebainisha mambo mengi sana kama ni changamoto ambazo zinahitaji kutatuliwa na kwa kweli changamoto hizi na mimi nashauri zaidi zifuatiliwe na zitatuliwe ili shughuli za Wizara ya Afya ziweze kwenda kama zilivyopangwa.

Nikiingia kwenye changamoto za jumla ambazo wameziainisha hapa nathubutu kusema kwamba kwakweli changamoto hizi ni nzito, kwa mfano kamati imebaini kuwa vituo vingi vya afya havina hati miliki ya maeneo ya vituo vyao. Hili suala la hatimiliki nalo limezungumziwa siku nyingi sana itafutwe hatimiliki kwa kila kituo ambacho ni cha Serikali kipatiwe hatimiliki ili kijulikane mmiliki halisi wa sehemu ile. Lakini bado kuna tatizo la hatimiliki kwa hivyo nashauri sana mvitafutie hatimiliki hivi vituo ili viweze kuwa mali ya serikali na watu wasivivamie.

Halafu kamati ilipata malalamiko mengi katika vituo vingi vya afya ilivyovitembelea kwa baadhi ya wafanyakazi kukosa nafasi za masomo ambapo baadhi yao wanalalamika kuwa tayari walilipia kwa gharama zao na baadae walipatiwa taarifa kuwa wasubiri wasiendelee na masomo hayo hadi mwaka mwingine. Nasema hii kwa kweli inavunja moyo kwa kiasi fulani, wakati tunalalamika kwamba Wizara ya Afya haina *staff* na ni moja katika changamoto haina *staff* wa kutosha, bado wako wenye moyo vijana wanatoa fedha zao halafu hatimae wanakatishwa kwa kweli hii haileti sura nzuri. Nashauri sana

tuwarudishe vijana hao waende masomoni wakasome ili tuweze kupata wafanyakazi katika Wizara hii tupate wafanyakazi wa aina zote.

Halafu sasa nikiingia kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sitaki kuchangia sana kwa sababu mwenyewe mwenyekiti kaogolea sana kwanye sehemu hii, lakini kabla ya Wizara ya Elimu samahani ningependa niseme kwamba Wizara ya Afya nawashauri sana hospitali binafsi tuzisimamie vizuri, hospitali binafsi hivi sasa mfumo wao wa uendeshaji kwa kweli hauridhishi. Nikitaja tatizo moja ambalo ni baya sana linaweza likazua wagonjwa wengi sana hapo baadae ni tatizo la kuchoma taka taka ovyo. Niliwahi kulizungumzia hapa na leo nalizungumzia tena suala hili ni kwamba Hospitali tunachoma taka ovyo ovyo kwenye maeneo yanayoishi watu harufu mbaya ambayo, hiyo harufu mbaya wala sio neno yale madhara ya hizo harufu mbaya zenyewe ambazo wanazifuta kwenye moyo wao, tunaweza tukaja tukapata maradhi ya ajabu ajabu hapa kipindi kifupi kijacho tusiposhughulikia suala hili.

Kuna wengine wanasema wamepewa vibali wachome karatasi lakini hata karatasi kwenye maeneo ya watu yakipeperuka yale mabaki yale bado majivu na moshi unawakera, kwa hivyo tunashauri sana wasiruhusiwe kuchoma chochote kwenye maeneo ya watu waende wakachome sehemu nyengine, kama hawawezi kupata sehemu nishauri Wizara ya Afya wawapeleke maeneo ambayo watachoma. Napendekeza sana Wizara ya Afya waangalie namna ya kudhidhibiti taka taka za hospitali, taka taka za hospitali zina matatizo sana lazima tupate ma-*incinerator* ambayo yatachoma takataka na kuziangamiza ili zisije zikaleta madhara. Nasema ni vizuri sana takataka za hospitali zikatenganishwa zile sindano zikachomwa mbali na hiya za mabaki ya binaadamu na matambara tambara ya kusafishia haya yakachomwa mbali ili kuepusha miripuko ya maradhi ambayo yanaweza kutokezea hapo baadae.

Sasa naingia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na kwenye Wizara ya elimu kidogo nitaingia kwenye *program* ya elimu ya maandalizi ya msingi, *program* hii inahusu utoaji wa elimu ya maaandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na moja. Katika kipindi cha kuanzia mwezi wa Julai 2017 Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar imegatua baadhi ya kazi zinazofanyika chini ya *program* hii na kuzipeleka katika Serikali za Mitaa. Ni kweli ni vizuri sana kuzipeleka katika Serikali za Mitaa kwa sababu hao wanafunzi wako huko mitaani huko kwenye Serikali za mitaa ndiko kwenye wanafunzi wengi. Lakini sasa napendekeza sana waandaliwe wanafunzi kwa masomo ya kivitendo ili ufahamu wao uwe mzuri, kwa sababu ukiwapa ma-*theory* kila siku hawaoni vile vitendo vinakwenda kwendaje. Matokeo yake hata wakiwa wakubwa huko hawana upeo wa kufahamu mambo mengi sana na matokeo ni kufeli kama huku ambako kumetokezea mara hii. Hapa tunashauri sana shule za maandalizi ziweze kupatiwa vifaa vya *practical* yaani vya vitendo ili waweze kujifunza mambo mengi kwa vitendo. Kwa sababu mtu akijifunza kwa vitendo anakumbuka zidi kuliko akijifunza kwa nadharia tu.

Halafu nasisitiza pia kwenye hizo Sekondari na kadhalika huko kuwe na vifaa vya maabara wakati wenzetu huko nchi za nje huko wanatengeneza sasa hivi nyuklia na wanakatazwa wasitengeneze nyuklia, wanaitetea wao kwamba wanatengeneza nyuklia kwa ajili ya manufaa yao na kwa uchumi wao. Lakini sisi hapa hata kutengeneza kifaa ambacho kitakuwa ni silaha ya nyuklia kusaidia kupambana na hiyo silaha ya nyuklia hatuna kwa sababu hatuna hata maabara, hatuna hata vile vifaa kwa hivyo watu wetu nao tuwafundishe ili pengine na sisi hapo baadae tutakuja kuvumbua kitu kikubwa zaidi kuliko nyuklia kikaweza kutulinda sisi na tukapata umaarufu duniani.

Nashauri sana Wizara ya Elimu hii kwa sababu ndio msingi wa kila mtu na kila mtu kapitia Wizara ya Elimu, kwa hivyo tunawashauri sana vifaa vya maabara vipatikane katika kila skuli na wanafunzi wafundishwe kwa vitendo mambo ya *Chemistry* na mambo mengine mengine ili waje wataalam wa *Chemistry*. Tunalalamika kila siku kwamba hatuna walimu wa sayansi lakini hatuna maabara vifaa vya maabara havipo tutawapata wapi. Siku zote tutaomba tusaidiwe kutoka Nigeria kutoka wapi sijui wao wenywe wana matatizo. Kwa hivyo nashauri sana najua kuna wanafunzi hapa mahodari sana wanajaribu kubuni mambo mbali mbali kwa hivyo tukiweza kuwapatia vifaa ambavyo vitawasaidia kuwa wataalam wa sayansi basi tutapata hapa wataalam wa sayansi na tutapeleka kwengine wakafundishe sayansi huko.

Kwa hivyo mimi baada ya kusema hayo nadhani nimeridhika sana na kamati hii ya Dkt. Mwinyihaji Makame kwa sababu kabla tulizungumza sana kwa upeo sana mambo mengi nimemuuliza hapa, kwa hiyo nimeridhika na ripoti hii na nampongeza sana, naipongeza Wizara ya Afya yenyewe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi kubwa wanazochukua katika kuleta maendeleo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana Dkt. Makame Ali Ussi, sasa ni zamu ya Mhe. Suleiman Makame Ali baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Said Omar Said, waheshimiwa mnaendelea kuniletea maombi ya kuchangia nilikuwa naomba tu wale ambao watachangia sasa hivi muda wao wafupishe ili na wengine waweze kuchangia vile vile, bado nafasi ya maombi ya kuchangia. Ahsante Mhe. Said Omar Said karibu.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *subuhanahu wataala* kwa kuniwezesha tena kuwepo katika kikao hichi jioni ya leo. Lakini nichukue nafasi hii nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Nianze kuwapongeza Waziri wa Afya pamoja na Naibu Wake, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Naibu wake kutokana na majukumu mazito wanayoyatekeleza asubuhi na jioni mpaka usiku. Lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa kamati hii ya Ustawi pamoja na wajumbe wake kwa kututayarishia ripoti hii tukaelewa ambayo tulikuwa hatuyaelewi kwa hivyo wametusaidia ili na sisi tuweze kutoa angalau maneno yetu mawili matatu.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze moja kwa moja kwenye ukurasa wa nne mpaka wa tano ambao Kamati husika imeeleza changamoto ilizozigundua katika ziara zao, lakini mimi niende kwenye Mabano (f) ambapo panasema hivi nitanukuu japo kidogo.

"Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya wauguzi wanapomaliza masomo yao hasa *General Nurse* hukataa kufanya kazi za uuguzi na ukunga na wengi wao hubakia *clinic* na kuwaachia wenzao kazi kubwa."

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa hapa ina maana kuna baadhi ya wafanyakazi wa wizara hii wanafanyakazi kinyume na fani zao lakini pamehusishwa *general nurse*, lakini wako wengine ambao ni muhimu mno kuwepo pahala hapo walipopangiwa lakini hatimae akaenda *clinic* au akaenda sehemu nyengine hili ni tatizo kubwa sana ambalo linaweza likasababisha mambo mawili nadhani. Kwanza gharama isiyo sababu pili vifo vya mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilishuhudia tukio moja kuna mwanafunzi mmoja aliumwa akenda hospitali alipofika hospitali yule muuguzi ambaye ndio mwenye dhamana ya pale hayupo, lakini yupo mtu ambaye ni mzoefu tu mwanamme mmoja lakini hana fani yoyote, alivyokwenda mtoto yule akamwambia mimi ninaumwa na tumbo basi akaingia ndani kwa sababu ndio kashawekwa pale atoe huduma na yeye hana fani akaingia ndani akampa dawa yule mtoto akenda hatua nne tano hivi akaomba maji ya kunywa akanywa dawa ile. Lakini baada ya kupiga hatua sita tu akaanguka ikawa anatoka vipovu. Sasa wakaja wazazi wake pale vipi ndio amepewa dawa hospitali huyu sasa ilipogunduliwa ikabainika kwamba dawa aliyopewa ya kujipaka, kwa nini akapewa dawa ya kujipaka amepewa na mtu ambae hana fani ya uuguzi, kwa bahati hakupoteza roho, lakini hilo sio katika jimbo langu jimbo langu hakuna wabishi wa aina hiyo jimbo langu hakuna wafanyakazi ovyo ovyo kama hao.

Kwa hivyo wapo baadhi ya wafanyakazi ambao hawatumii vipawa vyao, hawatumii taaluma yao, hawatumii maagizo waliyopewa kwa kuyafanyia kazi badala yake huweka watu mbadala. Hili ni tatizo kubwa ambalo husababisha wagonjwa wetu wengi wakapoteza maisha yao bila ya sababu yoyote. Kwa hivyo hili Mheshimiwa Naibu Spika, lazima lizingatiwe sana katika mahospitali. Kwani inakuwaje mpaka itokee hivyo na pale yupo mkuu wa kituo na hususan hospitali kuu kwa mfano Mnazi Mmoja, Abdalla Mzee mambo hayo yanaweza yakawa kama humo sio vituo vidogo vidogo na kwa nini yawe hivyo mimi namuangalia sana Mkuu wa kituo wa pale ndio aliyechangia matatizo hayo yaani mfanyakazi aliyemuweka chumba fulani kwa kazi fulani akaondoka yeye akamuweka mtu badala yake.

Kwa sababu kama huyu atakuwa yuko makini hayo hayatotokea na Mheshimiwa Mwalimu wa kiswahili akapewa kufundisha *Chemistry* ambayo si fani yake pale anapotosha lakini hauwi. Hadhari ipo daktari ambaye hufanya kazi ya utibabu bila ya fani hapo anaua hilo ni tatizo kubwa sana, kwa hivyo tulizingatie sana husan katika mahospitali yetu makuu.

Lakini tukio jengine kuna mgonjwa alitokea Wingwi akapalekwa Hospitali ya Abdalla Mzee akalala siku mbili tatu baadae akapata uhamisho kuja Hospitali ya Mnazi Mmoja, akaambiwa hapa hutibiki wewe uende hospitali ya Mnazi Mmoja Unguja. Sasa wakatoka watu watatu pamoja na yeye watu wanne gharama ngapi hizo. W\alipokuja huku Mnazi Mmoja kule wakaangaliwa Dokta akamuuliza nani aliyekuleta huku aa ni Daktari tu kule Abdalla Mzee aa hii si kesi yao hii ilikuwaje akakuleta huku hili ni tatizo dogo tu, hili ni moja mbili tatu basi kule kule. Akaambiwa basi akapewe vidonge kama vitano akaondoka hapa ni mzima na huyo ni Sheha wangu ambae ni Sheha wa Shehiya ya Mtemani. Kwa hivyo hili kwa nini likatokea ni kutokana na uzembe sijui tuseme daktari mbadala huyo kwa hivyo masuala kama haya lazima yaangaliwe vizuri jamani yatasababisha haya mambo mawili niliyoyataja gharama isiyo sababu au vifo vya papo kwa papo.

Lakini nikitoka hapo niende ukurasa wa kumi na moja, katika ukurasa wa kumi na moja kamati imetwambia kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi wanapopata uhamisho Unguja kwenda Pemba kama Abdalla Mzee pale baada tu ya kuripoti pale basi wanarejea kwao, kwa sababu gani pia hili ni tatizo Mhe. Naibu Spika, na tuangalie ni nani anayefanya hivyo yeye haendi kule akakata tiketi akaingia melini akaja huku itakuwa kuna agizo fulani limetoka wala haiwezekani mkuu wa pale kumuomba yule kutoka Unguja kwenda Pemba akifika yeye amruhusu kutoka Pemba aje tena arudi huku hawezi akafanya hivyo lakini itakuwa hapo pametumiwa gia kubwa muache aje huku yeye hana uwezo.

Kwa hivyo tunawaomba sana na sisi mutuhurumie ile ni hospitali ambayo imejengwa kwa gharama kubwa na ina nafasi kubwa, mgonjwa akiingia tu pale anaanza kupata ahuweni kutokana na lile jengo tu atakaloliona pale, akishuka tu gari pale anaanza kupata ahuweni anaona

hee hapa nitatibika, hospitali nzuri mno, tumpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Alhaj Ali Mohamed Shein kwa huruma yake aliyotufanyia pale. Sasa huruma hii watendaji muijali na muiboreshe ile hospitali kiasi ambacho waweze kutoka hata huku wagonjwa waje kule kutibiwa. Wameshawahi kutoka wagonjwa huku wakachukua wenyewe bila ya kupewa *transfer* kutoka kwa waguzi wa huku, wenyewe wameamua watoke huku waende wakafanyiwe kule *operation* na wamevuka salama. Tunawaomba sana kwamba hizi zote ni hospitali zote mbili tunazozitegemea.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Wizara ya Elimu japo kidogo, niendelee kumpongeza sana Mwenyekiti, wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kufanya ziara katika skuli ya Sizini. Alipofanya ziara yake katika Skuli ya Sizini amekuja na taarifa hii nanukuu:

> "Ongezeko la wanafunzi na uhaba wa madarasa katika skuli mbali mbali maandalizi na msingi kwa Unguja na Pemba, Kamati ya Ustawi imeona baadhi ya skuli zina idadi kubwa ya wanafunzi katika darasa moja kuanzia wanafunzi 80-120 mfano Skuli ya Sizini"

Mhe. Naibu Spika, napenda kumkumbusha tu rafiki yangu kwamba idadi ni hiyo ya wanafunzi darasa moja, nadhani ameshaijua na hili suala nilimpa juzi tu na akanijibu kwamba baada tu ya bajeti lile banda atalimaliza. Kwa hivyo nakukumbusha tu rafiki yangu kuwa idadi ni kama hii ambayo hayo yanatokana na Kamati, wenyewe wamekwenda na wameona msongamano wa wanafunzi wa Sizini. Nakuomba sana Mheshimiwa.

Nimalizie kuhusu Elimu Mbadala, nimpongeze tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Mohamed Shein kwa uamuzi wake na huruma zake kwa kuja kuamua kutujengea Kituo cha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali, nimpongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, kituo kimemalizika, kimeshafunguliwa, wanafunzi tayari wanaendelea lakini kuna changamoto ambazo ningependa kila muhusika atajua nini afanye. Siwezi nikasema hakuna umeme, umeme upo lakini ulioko hautoshelezi mahitaji kama yaliyotakiwa katika chuo.

Umeme uliopo unatumiwa kwa *computer* nne, taa na mafeni tu basi. Zile huduma za amali haziwezi zikatumia umeme huo, umeme huo umeungwa kutoka skuli nyengine ya Mtemani mpaka pale kwenye jengo lile. Pale wanatumia kwa shughuli hizo tu lakini kwa shughuli zilizopangiwa hasa za amali bado panahitajika umeme wa kutosha kwa matumizi ya kituo kile.

Mhe. Naibu Spika, nipende kumkumbusha Mhe. Waziri mengine yanayohitajika pale ni maji, maji hapana. Juzi juzi mwalimu mkuu wa pale alikwenda ZAWA kwenda kutoa taarifa ile. ZAWA wakamwambia kwamba paipu inatakataka lakini abakie wiki moja tu baadaye watakuja lakini mpaka leo mwezi wa pili huu, moja ni hilo.

La pili ni walimu wa fani hawapo pale, waliokuwepo pale ni vijana tu ambao wamejitolea kwa moyo wao, mmoja anatoka Konde na wengine wanatoka Chakechake. Kwa hivyo tunahitaji walimu wa fani zifuatazo, fundi umeme, upishi, seremala, fundi bomba na fundi gereji. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii ya kushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara zetu hizi mbili muhimu moja Wizara ya Afya ambayo inayoweka maisha yetu sisi wananchi lakini pili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo inatupatia maendeleo sisi wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza na Wizara ya Afya, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za makusudi anazozifanya kuhakikisha Sekta ya Afya Zanzibar inaimarika katika kipindi chake. Nataka kusema leo pasina Wizara ya Afya ku-*improve* katika kipindi cha Rais Dkt. Ali Mohamed Shein basi mimi huwa nafikiria kama Wizara ya Afya haija *improve* muda huu sijui tena lini ita-*improve* kwa sababu Mhe. Rais ana jitihada za makusudi kwa sababu ni Sekta yake kila uchao halali kwa kuhakikisha Wizara ya Afya ina *improve* kwa sababu yeye ndio taaluma yake, ni mtaalamu katika mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, watendaji wa Wizara ya Afya wanafanya kazi nzuri, leo siyo siku ya kulaumu bali leo ni siku ya kuchangia ripoti. Ripoti yao ni nzuri tumeipokea ripoti iliyowalishwa na Mwenyekiti, mzoefu Daktari Mwinyi Haji Makame, amewasilishwa akiwa amependeza kwa madaha mengi na makubwa yanayoonyesha uzoefu na udaktari.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nitagusia mambo kadhaa. Zanzibar ni nchi ya Kimapinduzi, nchi ambayo Mapinduzi matukufu Januari 1964 yamekuja kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima wa Zanzibar. Unaposema wakwezi na wakulima ni wale watu wanyonge kina sisi ambao ndio maana na lengo halisi la Mapinduzi. Cha kusikitisha na ninachokiomba leo hatusikitiki tunamuomba Mhe. Waziri wa Afya ajitahidi, ajitahidi.

Naishukuru sana Serikali bajeti yote inampatia lakini bado leo tukenda Wizara ya Afya hasa Hospitali ya Mnazi Mmoja unaambiwa X-ray haifanyi kazi, unaambiwa MRA haifanyi kazi, unaambiwa kifaa hichi hakifanyi kazi. Unaambiwa wende Global au uende Al-Rahma au uende Kilimani. Sisi ni wanyonge wakwezi na wakulima, shilingi laki mbili unusu kwa ghafla utaipata wapi ya kwenda Kilimali kupima X-ray na mambo mengine. Lakini kinachositisha kwamba kule vya mtu binafsi vinafanya kazi, hivi vya serikali havifanyi kazi. Hakuna mtu binafsi au mfanyabiashara duniani anoishinda serikali kwa pesa. Lakini utashangaa na jitihada zilizokuwepo za Mhe. Rais anazozifanya kila siku lakini bado utaambiwa uende Kilimali, utaambiwa uende Al-Rahma, uende wapi na Mhe. Rais anajitahidi anahakikisha na Mhe. Waziri wa Fedha, Wizara ya Afya inapatiwa fedha zote.

Naomba sana hivi vipimo viwepo na vifanye kazi masaa 24. Nilisema jamani hatujasema na Mwenyezi Mungu kwamba ajali inatokezea mchana tu kuanzia saa 3 mpaka saa 9 na usiku pia ajali ipo, kuumwa na usiku kupo ndiyo *emergence* mfanyekazi masaa 24.Sio ukenda usiku saa 2 saa 3 unaambiwa subiri asubuhi, asubuhi ukija mtu unopata *internal bleeding* kama zako zipo ndio zako zipo, lakini kama zako hazipo ule mfungo maarufu wa Mnazi mmoja unaitwa mfungo wa pipi tena unaelekea kaburini yako yameshakwisha.

Mhe. Mwenyekiti, chengine Hospitali ya Mnazimmoja naomba sana Mhe. Waziri wajitahidi kwa usafi, usafi hauridhishi na tumeshausema sana mpaka tumeshachoka. Mpaka leo nguvu za kusema tumekuwa hatuna kwa sababu tumeshasema sana tumeshachoka. Usafi Mhe. Mwenyekiti, Mnazi Mmoja hauridhishi hata kidogo, tunaomba kwa heshima kubwa Mhe. Waziri hebu aende huko vyooni vya Mnazi Mmoja, hebu atembelee aone hali halisi ya usafi Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo ninakwenda uhaba wa watendaji. Watendaji kuanzia madaktari, Manesi, wauguzi wako haba hawatoshi ndio maana maradhi ya matatizo mengi yanatokezea kwa sababu ya uhaba wa watendaji na naomba watendaji wanakumbwa na mambo mengi yakiwemo maposho yao, wote tuhakikishe tunawapatia. Chengine nasikitika sana tumeunda mashine ya gesi mpya serikali naishukuru sana imenunuliwa mashine ya *gas* mpya sijui imetoka nchi gani mashine ile. Kama nnasikia mara nne tangu iwekwe mashine ile imehariibika na hata mwaka haijafika. Nauliza ile mashine haina *guarantee* au mashine iliyonunuliwa siyo mashine sahihi ni mashine bomu kwa nini kila siku iharibike. Kipindi kilichopita katolewa mtaalamu kutoka Dubai katumia karibu dola chungumzima za Kimarekani kuja hapa kuitengeneza mashine na juzi imeharibika tena, kila siku mashine inaharibika mpaka napata wasiwasi mashine hii si bomu lakini au ndio vile tunavyosema kileo changa la macho.

Naiomba serikali itizame mashine hii, serikali naishukuru, namshukuru Rais mashine mpya lakini kila siku inaharibika, kulikoni mashine hii mashine gani, baada ya sisi tuende mbele inaturudisha nyuma, kila siku tunaitengeneza, sijui kiasi gani tumeshatumia kuitengeneza mashine hii ambayo ni mpya haina *guarantee* imenunuliwa wapi hasa, mambo ya kujiuliza.

Mhe. Mwenyekiti, vifaa vingi vinaharibika Mnazi Mmoja na hakuna mafundi waliosomea, tunaomba sana hawa mafundi waliosomea *bio engeneering*, tunaomba sana hawa mafundi waliosomea bio *engeneering* watafutwe japo kukodiwa ili baadhi ya vifaa waje kuvitengeneza vinaharibika vingi na hakuna mafundi, wale mafundi waliokuwepo wote kumbe siyo utaalamu wao huwo, hawajui hasa kuzigusa zile mashine, siku nyengine wanaziharibu wao. Chakusikitisha

wanaomba wale wapate mafunzo ya kutengeneza vifaa lakini hawapatiwi wenyewe wanasikitika.

Mhe. Mwenyekiti, nikotoka hapo nakwenda Wizara ya Elimu kama nilivyosema hizi ni Wizara mbili nyeti. Wizara hii nampongeza sana dada angu *comrade* Riziki Pembe anafanya kazi nzuri nampongeza sana Mwalimu wangu wa Kiswahili Katibu Mkuu Bi Khadija na Watendaji wote pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, wanafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sijawi hata siku moja mimi kuchangia Wizara ya Elimu kwa sababu radhi za walimu zinapata lakini leo nimeamua kuchangia kwa kutoa mchango wangu kwa maendeleo sio ku *criticize no* kwa maendeleo. Sasa naomba nianze Wizara ya Elimu kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu kama tunavyojua ni Wizara nyeti ambayo sote tunasema elimu ndiyo ufunguo wa maisha, elimu ni nuru, elimu *is every thing* hata Mwenyezi Mungu amesema *"iqra bismirabbikal khalaq"* kwamba tafuta elimu, soma, kwamba umuhimu wa elimu jinsi gani elimu ina umuhimu kwa maisha ya mwanadamu. Tunaijua elimu, tuliposoma sisi enzi hizo ilikuwa kuna Kidongechekundu, Lumumba, Fidel Casro, Hamamni, Haile-Selassie, zote zinafanya vizuri unafurahi hasa, lakini leo Mhe. Mwenyekiti, zimezuka skuli za matajiri za watu wenye fedha hizo ndizo, nashukuru safari hii mitihani Wizara ya Elimu imefanya vizuri lakini uzuri wake ukilinganisha Skuli za *Private* na Skuli za Serikali utakuta Skuli za *Private* zimefanya vizuri zaidi kuliko Skuli za Serikali. Mimi huwa najiuliza mbona zamani sisi tulikuwa tunafanya vizuri maskuli, leo kuna nini na ukitizama mwalinu ndiye yule yule Mwaka, mwalimu ndiyo yule yule Hassan, mwalimu ndiyo yule yule Bi Asha, lakini kule *Private* anafanya kazi nzuri, huku Serikalini hafanyi kazi nzuri, kula *Private* wanapasi watoto wengi, huku Serikali aah! Tatizo nini? Kwa hili naomba sana tufanye *research* tujue tatizo nini kwa nini Skuli za *Private* zifanye vizuri Skuli za *Government* zishindwe na Skuli za *Private*, mimi hapo sijapakubali.

Mhe. Mwenyekiti, nchi za wenzetu kwa mfano Marekani huko Uingereza, hakuna hasa Skuli za Private kwa sababu Skuli za

Government zinatosha, lakini tukumbuke ilivyofika miaka ya 25 ya Mapinduzi ya Elimu bila ya Malipo tuliimba nyimbo pale Amai na mimi nilikuwepo, tuliimba hivi

Robo karne hiyooo leo imetimu tunashangiria,
Kutangazwa kwa elimu kuwa haina fidia.
Ni siku yetu adhimu
Sote tunashangiria.

Kusoma kwa matabaka tajiri na masikini
Sasa tunafaidika sote tulio nchini,
Robo karne hiyo leo imetimu tunashangiria"

Sasa ukiangalia robo karne tulisema sasa tunafaidika sote tuliyo nchini, kusoma kwa matabaka tajiri na masikini sasa tunafaidika. Ninapata wasiwasi, Mhe. Mwenyekiti, tuliimba nyimbo nzuri, imepangika vina, zimepangika beti, lakini leo yale matabaka tuliyoyaondosha naona mbona yanarudi anasoma sanma matajiri kuliko masikini mkwezi na mkulima. Tajiri ndiyo anayekwenda skuli ya fedha, tajiri ndiyo anaekwenda Skuli ya Glorias, tajiri anakwenda skuli za pesa, lakini miye mkwezi na mkulima nimemaliza Kidongochekundu, nimetoka Kidongochekundu nimekwenda Lumumba Skuli ya pesa sijawahi kwenda hata siku moja. Sasa je mtoto wangu wa Welezo atakuwaje na skuli inayopasish vizuri ni skuli ya *private*.

Mhe. Mwenyekiti, hapa napata wasiwasi kweli kweli, pananikera kweli kweli, namuomba sana dada angu *comrade* Waziri wa Elimu ajitahidi skuli za *government* ziwe bora kuliko skuli ya *private school* mpaka tufike pahali pa-private skuli wafunge wenyewe kwa sababu skuli za *government* ni bora kuliko *school za private*.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika majengo, naishukuru sana serikali inafanya kazi nzuri sana ya kujenga majengo mazuri, majengo imara, majengo ya kisasa. Sasa nina wasiwasi mkubwa baada ya kufanya *research.* Isijekuwa majengo haya tunayajenga lakini kila nikiliangalia jengo la skuli ya Lumumba na jengo la Skuli ya Kidongochekundu naliona lipo imara kuliko jengo la Skuli ya Mtule lilojengwa miaka miwili iliyopita, Kidongochekundu hata upige nyundo gani halianguki

na wala haivuji. Lakini skuli ya Mtule inavuja rovu rovu na mpya imejengwa juzi. Sasa unajiuliza tunakwenda mbele tunarudi nyuma kunako haya majengo ya Wizara ya Elimu, isijeikambiwa ile hadithi ya konokono mchana konokono anapanda kisima futi nne na nusu, lakini ikifika usiku anashuka futi tano kasorobo, sasa tutafika? Unaambiwa u-*calculate* konono atakipanda kisima cha futi mia nne thalathini kwa muda gani, jawabu lake utakuwa hulipati. Mhe. Mwenyekiti, nina wasiwasi, majenzi haya lazima tufikirie, tuangalie *value for money*, tunayajenga ghali tujiulize je, majengo haya *value for money* ipo, mbona serikali inajitahidi, mbona serikali inafanya vizuri, je majengo haya yana ubora au tunawapa watu wanatupiga changa la moto. Hawa matajiri wanaotujengea maskuli, hawa ma-*contractor* wanatupiga changa la moto na mapesa yao si kidogo wanayoyataka, kweli tutafika hivi, *value for money* ipo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kabla hatujajenga skuli yoyote lazima tujiulize maswali, tuunde Kamati, tuangalie skuli tunayoijenga je, ina *value for money* au tunajenga kumtajirisha mtu. Isijekuwa tunajenga hizi skuli kuwatajirisha mtu au watu lakini wanatuachia majengo mabovu hapa, hilo nimeona niliseme.

Nikitoka hapo nakwenda kwenye michezo kupitia Wizara ya Elimu, tulipokuwa sisi wadogo ilikuwa ikifika Elimu Bila ya Malipo kuna UMISENTA, kuna UMISHUTA kuna kitu gani wachezaji wa mipira wote wazuri walitoka katika maskulini wakati huo kina Dua Said kina nani. Sasa najiuliza leo iko wapi ile shamra shamra ya michezo katika Wizara ya Elimu tuliyokuwa nayo zamani, ilikuwa ikichezwa Haile Selassie na Kidongochekundu hapatoshi, Kidongochekundu na Lumumba hapatoshi na mule ndimo tunamopata vipaji lakini namshukuru sana Mhe. Rais kwa kuanzisha Idara ya Michezo katika Wizara ya Elimu.

Lakini naomba sana ile shamra shamra ya michezo tuliyokuwa nayo zamani irudi katika kuimarisha michezo, tukumbuke michezo ni kwa afya lakini pia michezo ni kwa uchumi wa maendeleo ya mwananchi maendeleo ya binadamu. Nchi za wenzetu kina Ghana, Cameroon na nyengine zimeendelea kupata mchezaji mmoja tu yale mabilioni ya pesa anayolipwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache leo kwa niaba yangu kwa niaba ya wana mapinduzi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Welezo, kwa niaba ya wakwezi na wakulima walionichagua naomba kuwasilisha maneno yangu haya machache na ninaomba machache sana kwa niaba ya maendeleo ya mapinduzi, kwa niaba ya maendeleo ya Zanzibar na taifa kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mwenyezi Mungu mubariki Mhe. Rais wa Zanzibar, Mwenyezi Mungu wabariki Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono ripoti hii mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh sasa nimpe nafasi Mhe. Miraji Khamis Mussa na baadaye atafuata Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi machache katika ripoti hii ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti na kamati yake kwa kutupa ripoti nzuri imeainisha changamoto katika maeneo mengi lakini na mafanikio kwa ujumla wake, lakini niwapongeze mawaziri wa wizara zilizotajwa kwenye ripoti hii wote kwa pamoja manaibu mawaziri...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Miraji kidogo kaa waheshimiwa wajumbe kidogo nimepata dharura kwa hiyo naomba nimpishe mwenyekiti aweze kuja kuendelea. Mhe. Mwenyekiti karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee mheshimiwa

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa Wizara ya Afya naenda moja kwa moja kwenye Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukuwe nafasi hii kwa namna ya pekee nimpongeze Katibu Mtendaji wa wakala huu wa Chakula, Dawa na Vipodozi kwa hivi karibuni tu kupata *certificate* ya ubora wa viwango wa *East Africa* (AISO). Hii ni hatua moja kubwa ya Bodi yetu ile au Wakala wetu ule umefika katika hatua nzuri, lakini pia naomba nimpe pongezi kiongozi huyu na wafanyakazi wote wa wakala huu wa Dawa, Chakula la vipodozi kwa kazi nzuri waliyoifanikisha kwa hasa wale wauzaji wa chakula na vitoweo aina ya kuku, nyama, samaki kwa namna ya ukaguzi wao bora vitoweo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi hizi nazipeleka moja kwa moja kwa ukaguzi wao walioufanya wa JMP katika utaratibu wanaoufanya na mazingira yao ya kazi lazima nimpe pongezi sana japokuwa na mimi ni mdau katika eneo moja la wale wauza kuku, lakini kwa pamoja wamefanya kazi nzuri ameshirikiana nasi wauza kuku, wauza samaki na wauza tomato na kuhakikisha katika maeneo haya wameweza kufanikisha ukaguzi huu mzuri.

Lakini nimuombe tu kiongozi wetu huyu katika maeneo kama haya ya kutafuta ubora wa chakula lakini na wenzetu wanaouza vyakula vya makopo, michele, biskuti kwa sababu na wao wanaingiza vyakula hivi nchini, basi katika utaratibu huo wa kawaida basi na wao wenzetu wafanyiwe kama ambavyo wengine walifanyiwa, ili haki ya msingi ya vipimo vya kupitia vyakula hivi na kukagua maeneo hasa yale yanayotoka katika viwanda vyao basi tuweze kutambua au aweze kutambua kwa faida ya Wazanzibari.

Lakini kwa ujumla pongezi zangu pia na unajua ukifanya biashara kuna maeneo pia unakuwa una maduka, una sehemu ya kuuzia kwa hivyo kwa wale wa Mkoa wa Mjini na Mkoa wa Kusini wamefanyiwa ukaguzi na kupewa baadhi ya *certificate* ambazo wanatoa kwa hivyo, naomba na maeneo mengine wakala huyu watufanyie kazi kama ambavyo amefanya katika maeneo hayo niliyoyataja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya sina mengi wamesema wenzangu na nayaacha mimi nilikuwa kwenye bodi lakini naomba niende Wizara ya Elimu na nianze

moja kwa moja katika eneo la Programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi kuna changamoto zimetajwa lakini na maagizo ya kamati yametajwa, kuna eneo moja limeguswa sera.

Sera hii Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mdau ambaye niliichangia sana na leo naamua kuichangia kwa sababu mapitio haya ya sera kwa kipindi kirefu tulikuwa tuna mashaka sana na eneo hili sisi la sera ambayo tunakwenda nayo ina mtihani kweli hasa kwa skuli zetu hizi za SMZ. Kwa sababu sera hii ni nzuri lakini kama huku chini tunakotokea hakuna maandalizi mazuri hatuwezi kukabiliana na sera hii.

Leo sera hii inatuambia hata ule umri wa watoto kuanza shule umepungua lakini kuna maeneo sera hii tunawachupisha wanakwenda form I maana yake kuna karibu miaka mitatu hapa tunaitoa lakini je mtoto huyu tunapomuanzisha katika elimu ya msingi lakini ndani ya darasa ukakutana na watoto 250 watoto hawa msingi wake tokea huku mwanzo maana yake unapotea hatuwezi kuwaandaa vizuri, hatuwezi kuwapa msingi mzuri wa elimu maana yake watafika darasa la nne hawajajitambua. Kwa sababu kuanzia alau la nne, la tano ndio unawakuta ile *package* yao inaanza kupungua kama *roll* ina 250 au 150 ndio alau unaweza ukaikuta mia na sasa chini huku mwalimu wa kawaida kwa kufuatana na utaratibu huu wa sera kuendelea kuwa na sera hii, bila ya kuwa na huduma nzuri zile *facility* zote kwa ujumla wake zilikuwa zinapatikana utaratibu wa kuwachupisha hawa, matokeo yake hatutoyaona sasa tutakuja kuyaona 2022 watapofanya mitihani hawa watoto wa form II tuliowatoa juzi.

Leo watoto wa form II tulikwenda mpaka kile kiwango cha D na E tuliwapeleka karibu wastani wa asilimia themanini unawapeleka mbele je dhahiri maana yake hawa tunapokwenda kuingia katika mitihani ya *O level* moja kwa moja utakuja kumkuta asilima 25 ndio inafaulu. Sasa sera hii mapitio yake ni muhimu sana hasa katika umri wa watoto kwa sasa wakati hatujatimiza yale mahitaji maalum ambayo ndani ya shule zetu yanahitajika kwa huku mwanzo tu wanakoanzia na naomba hili tukubaliane sana. Madarasa yetu alau kwa mfumo huu tungekuwa tunakwenda kama huko *private* alau darasa unalikuta lina watoto ishirini na tano, thelathini basi mwalimu anaweza kutoa huduma nzuri kwa wale watoto na wataweza kusoma vizuri. Lakini *roll* ya watu 250 mwalimu

kuita majina tu anaita kwa kibomba kama hajapiga kibomba mtu nyuma hasikii wakati wa kuwasomesha anawasomesha vipi.

Ikisha ikifika darasa la sita wachupe mpaka form I hatuwezi kufika katika eneo hili tutaandaa mazingira ya kuwafelisha vijana wetu siku hadi siku, vyenginevyo huduma ile ya kuendelea kujenga majengo kwa kasi sana basi iende sambamba na mazingira tunavyowatoa wanafunzi wetu. Kwa sasa kunako eneo la sera nakubaliana na mwenyekiti agizo hili liende ili mapitio ya sera alau kuna mambo tuyapunguze kwa sasa unaweza ukatumia sera hii lakini ukafika pahala ukapunguza alau ule umri ukaongezeka kidogo lakini na kuliacha darasa la saba ukawachupisha mpaka form I ni tatizo kubwa. Kwa hivyo, tukiweza kwenda na kasi ya kurekebisha basi turekebishe kwa ubora wake katika mapitio ya sera hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika changamoto katika Chuo Kikuu cha SUZA kuna changamoto ya kuunganishwa vyuo, vyuo hivi vilivyounganishwa kukosa fedha na matumizi kwa ajili ya uendeshaji. Wenzetu wanakamati wameliona hili lakini mimi naomba ku-*declare interest* mimi ni mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa SUZA.

Kwanza nikupongeze sana Mhe. Mwenyekiti, katika dhamira hii ya kuunganisha vyuo serikali ilikuwa ina nia thabiti na tulifika pahala tukaona katika eneo hili tutafika vizuri, lakini mimi wa mwanzo ambaye nakiri ziko changamoto ambazo wakati fulani hata lile baraza lenyewe tukizisemea hazifi katika utatuzi wake. Sasa leo wenzetu wameliona na limekaa katika sehemu ya maagizo mimi niungane kabisa na mwenyekiti wa kamati hii changamoto hii ipo na mjadala wake unaendelea kujadiliwa lakini mimi niseme nikiwa ni sehemu ya ujumbe wangu hapa, changamoto hii ya kuendelea kuviunganisha vyuo katika SUZA kwa sababu sasa hivi tunafanya *study* nyengine ya kuvitoa vyuo vyengine vilivyobakia kwenda kuvikwamisha kule, maana si kwenda kuviendeleza tunakwenda kuvikwamisha kwa asilimia mia moja tunakwenda kuvikwamisha. Nawaomba mimi wajumbe wenzangu katika utakapokuja mswada wa aina hii uangalieni kwa makini hatuwezi kufika katika utaratibu huu.

Tumeitoa *Nkrumah* tumeipeleka kule mazingira sasa hivi ya walimu tunaowapata maana yake tuna *approve failure* kabla hawajaingia darasani. Maana yake leo *Nkrumah* haipo ni chuo ambacho kinaenda kufundisha zile *ethic* za uwalimu ambao tunazipata moja kwa moja lakini leo tunakwenda mtu kasoma *education* haifanyiwi ile *study* yake ni kawaida tu *qualification* zake ziko vipi lakini yale maadili hasa hayapati na yake mafunzo hasa ya ule uwalimu hayapati. Tunampeleka tu wewe nenda katufundishie watoto wetu hatuwezi kuandaa wanafunzi wanaotoka sasa wakawa wanafunzi bora, wakawa wanafunzi au wafanyakazi wa kesho maana lazima watokane na Wizara hii ya Elimu. Sasa leo tukiviondoa vyuo vyote *package* yake tukaiweka pale unaenda tu kusomeshwa *education* hatuwezi kufika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hili nakuunga mkono kwa asilimia mia moja changamoto hii ipo na wapo najua umeambiwa mengi wako watu wanafika pale wanatoka Chwaka kule Chuo cha Uongozi wa Fedha kilichokuwa wanakuja na madumu Tunguu tunayasemea unafika pahala mpaka yanakuwa yanakithiri hatuwezi kufika. Tunafika pahala tunaangusha ile misingi ya kawaida ya uendeshaji hata mazingira ya vyuo vyetu. Saa leo vyuo vyote ukenda ukavikandamiza kwa wakati mmoja ukimkuta kiongozi dikteta unauwa vyote, sasa lazima tufanye *study* kwa wakati huu tusije tukenda tukakiua na chuo chengine hicho tulichokibakisha kuna chuo cha IPA, kuna chuo hiki tulichokibakisha chengine cha Uwalimu Chuo cha Kiisliamu, tusije tukafika pahala tena vyuo vyote tunakwenda kuvitia shimoni pahala pamoja lazima vyengine vikae juu ili hivi vyengine vikawa havina pumzi ya kupumua hivi vyengine vinapumua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee katika changamoto za utekekelezaji wa progamu, pamoja na mafanikio hayo kamati imeona changamoto zifuatazo ujenzi wa Chuo cha Amali Daya Mtambwe wenzangu wamezungumza lakini kulikuwa na ahadi ya kiongozi wetu mkuu hapa mpaka leo changamoto hii inazungumzwa katika utaratibu wake. Mimi niungane na Mhe. Mwenyekiti lakini niwambie wenzetu wa Wizara ya Elimu kama ahadi hii ilitolewa na kiongozi wetu tufikie pahala basi tuwekee katika hali nzuri na msisitizo mkubwa wa kuweza kuitatua kwa wakati. Lakini Chuo cha Amali Makunduchi asilimia iliyofika ni asilimia ishirini na tano na muda mrefu sana sasa sijui Mhe.

Waziri hapa wa Elimu asilimia hii na udororaji huu nini kinachotupelekea mpaka hapa tatizo mkandarasi, upatinaji wa fedha lakini kuna kitu gani. Tunafika pahala tunajiuliza maeneo mengine mambo yanamalizika haraka lakini kitu kilichoelekea Makunduchi kinacheleweshwa sasa lazima Mhe. Waziri kunako eneo hili na sisi tunaotokea Makunduchi utuone.

Mhe. Mwenyekiti, naomba changamoto ya utekelezaji wa progamu nyengine ya uhaba wa walimu wa fani mbali mbali ya sekondari tatizo hili kubwa hasa kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi, lakini ukisoma ripoti hii vizuri liko eneo jengine unalikuta wazi linaonaneka kuna walimu wanastaafu kwa kasi sana, mishahara yao inakuwa ipo wakistaafu maana yake inakuwa kutegemea bajeti mpya labda uje uwatengee na uwaombe upya. Kwanini mpaka sasa maana inafika pahala tunawajua wafanyakazi au walimu 400 ikifika tarehe fulani wanastaafu kwanini tusijiandae mapema kuzitangaza nafasi zile wanapotoka tu kustaafu tuchukuwe watu wengine kwasababu wao vibali vyao havitaki msukumo vinapatikana tu moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sina mengi naomba nimalizie kwa kuwapongeza tena wanakamati lakini pia kuwapongeza mawaziri wote wawili, makatibu wakuu na wakurugenzi wote wanaoongoza sekta hii changamoto hizi tulizozisema tumesema tu kwa ufupi lakini naomba mumpe mashirikiano mwenyekiti ili kutatua changamoto hizi. tukitatua hizi kwa umapema wake basi watoto wetu tutawafaidisha maana kunako mazingira ya elimu kwa kweli kasi yake sio ile ambayo tunaitarajia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla na atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu naye ajiandae.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukuwe fursa hii kumshukru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* ambaye ametujalia jioni hii tukaweza kukutana mahala hapa tukiendelea na mijadala yetu ya ripoti za kamati.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza mawaziri wetu hawa wawili wa Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na watendaji wao wote niwachukuwe fursa hii kuwapongeza walimu kila ambaye amepitia fani ya uwalimu na hata akawa sasa hasomeshi lakini ameweza kuwakomboa wananchi wa nchi hii, kwa hiyo Mwenyezi Mungu awajaalie kheri watu waliofanya kazi hii ya kuwasomesha watu, waliokuwa wamekufa Mwenyezi Mungu awarehemu kwa rehema njema na walioko duniani Mwenyezi Mungu awaongezee ujuzi ili waweza kutusaidia kupitia elimu zao.

Mhe. Mwenyekiti, wizara mbili hizi ni wizara nyeti kabisa ambazo ndizo zina mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu, kwa hiyo ni wizara ambazo zinataka kuangaliwa kwa jicho la huruma sana ili tuweze kuendelea. Ili uwe na maendeleo lazima uwe umepata elimu tena elimu iliyo bora na ili uipate hiyo elimu uweze kwenda hiyo elimu ni lazima uwe na afya bora ili uweze kwenda kuipata hiyo elimu kwa hiyo hizi wizara ni wizara muhimu sana na nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwamba wizara hizi amekuwa akiziangalia kwa mtazamo wa hali ya juu kabisa ili waweze kujikimu katika kuwahudumia wananchi kila siku.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi zangu hizo naomba niendelee pia kuwapongeza wachangiaji wote ambao wamenitangulia katika kuchangia kwa michango yao mizuri ambayo inaendelea kutuletea ufanisi katika kazi zetu. Lakini nataka niungane na Mhe. Machano Othman Said kwa mchango wake ambao alimuomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kulimazia jengo la skuli ya Donge, skuli ya ghorofa. Naomba sana mheshimiwa hili uliangalie tumekuwa tukijitahidi sana lakini ndio unajua nguvu zetu zilivyo, tunaomba uingize na wewe nguvu zako hapo ili skuli ile iweze kumalizika.

Pia niungane na Mhe. Khadija Omar Kibano aliposema kuhusu vyuo vile vya amali ambacho ni Chuo cha Daya na Chuo cha Makunduchi bado ujenzi wake unasuasua. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana sana lazima tujitahidi kuvisaidia sana vyuo vya amali kwa sababu ndio mkombozi wetu mimi niseme, kwa sababu tunajua hapo vijana wetu wengi wanashindwa kuendelea na masomo ya juu lakini bado nyinyi

mmetengeneza utaratibu wa kuweza kuwasaidia wanafunzi wetu hao mnapoona wamemaliza na hawakufanikiwa kwenda usoni lakini mmetengeneza utaratibu. Naipongeza serikali kwa utaratibu huu lakini sasa lazima vyuo vya amali tuviwezeshe viweze kuwa na zana ambazo zitaweza kuwasaidia wanafunzi katika kupata masomo yao ambayo yakujiendeleza katika elimu hii mbadala ambapo kule wanapata ujuzi wa kuweza kuwasaidia kuendesha maisha yao. Kwa hiyo, mimi naomba sana vyuo hivi vya mbadala tuwe na vitendea kazi vya kutosha ambavyo vitaweza kuifanya elimu hiyo iendelee na kuwaondosha vijana wetu katika vijiwe.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameeleza mengi na mimi nataka niungane nao hasa katika fani hii ya elimu ambapo tunaona muda mwingi tuna mapungufu ya walimu. Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme katika upungufu huu wa walimu tunaweza tukajiuliza masuali mengi, pengine kwa nini tunapata matokeo mabaya, kwa nini wanafunzi wetu wanafeli. Hili la upungufu wa walimu ni suala moja ambalo linaweza likasababisha matokeo mabaya, kwa sababu wale wanafunzi watakuwa hawawezi kupata masomo yao kama vile inavyohitajika. Kwa hiyo, ni suala moja ambalo la kuliona kama walimu tuna upungufu nao lazima tutengeneze utaratibu wa kuweza kupata walimu.

Mhe. Mwenyekiti, pia mimi niseme ukaguzi wa maskuli wa kuwakagua walimu katika utendaji wao wa kazi, pia ni suala moja ambalo linaweza likaondosha pengine ile changamoto ya matokeo mabaya, kwa sababu mwalimu akiwa anapata kukaguliwa mara kwa mara ataweza kufanya kazi yake katika uadilifu mzuri na ataweza kuwasaidia wanafunzi katika hali nzuri na matokeo hapo yanaweza yakawa mazuri. Kwa hiyo, walimu na wao kukaguliwa huu ukaguzi nauona pia nao una nafasi yake katika kuwasaidia wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi changamoto hii ya walimu tuna walimu ambao wanakuwa wanajitolea, wamejitoa muhanga walimu hawa wanafanya kazi ya kujitolea katika kuondosha ile changamoto ya walimu pale. Lakini bado walimu hawa hatuwatambui maana yake hatujawatambua kwamba waweze kuendelea na lile jambo la kujitolea pale. Kuwatambua kwenyewe ni kuwapa kipaumbele zinapotokea nafasi hizi kwamba na wao waajiriwe ili ambao wamekaa pembeni na wao

watapata moyo wa kuja pale kujitolea. Sasa tukiondosha changamoto hiyo mimi niiombe sana serikali, na serikali niiombe ile Tume ya Utumishi ambayo inafanya uajiri walione hili, wizara pelekeni kilio chenu pale nyinyi ndio wenye mahitaji haya. Pelekeni kilio chenu kwa tume ili ionekane kwamba nyinyi ni watu wa mahitaji ya kila wakati, kwa sababu kila mwaka wanafunzi wanaongezeka si lazima na walimu itabidi waongezeke. Sasa tume hii mimi naomba serikali ingefanya tume mkapewa nyinyi wenyewe wizara Tume hii ya Uajiri ambayo nyinyi ndio mnajua zaidi mahitaji yenu ya walimu na nyinyi mna wataalamu hao walimu ambao tayari nyinyi mnawaelewa. Kwa hiyo, mimi ningeiomba sana serikali kufikiria hili jambo la kuona haya maombi ya kupewa tume wizara yenyewe iweze kuajiri walimu wake ni suala la msingi changamoto hii pengine ingeweza kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, niende tena katika ukurasa wa 24 ambapo hapa kuna Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hapa wameonesha changamoto zile ambazo katika elimu ya mikopo ya juu wamesema kwanza kuna kusitishwa mikopo ya elimu ya juu kwa wafanyakazi wa serikali wanaojiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, tuwape hawa wenzetu ambao wanajiendeleza kwa sababu kuna fani mbali mbali zinahitajika lazima waweze kupatiwa mikopo hii ili na wao waweze kuendeleza taifa hili. Lakini kuna ucheleweshwaji wa fedha kwa baadhi ya wanafunzi hasa wa vyuo vya nje ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hili naomba sana wizara iliangalie kwa mtazamo wa hali ya juu, kwa sababu hili mwanafunzi aliyekuwepo nje hana mjomba kule, hana shangazi. Kwa hiyo, tunaweza tukasababisha yale matatizo ya udhalilishaji ambayo sisi tunayakataa na tunayapiga vita kwa nguvu zetu zote yanaweza yakawakumbuka watoto wetu wanaosoma kule wanapokubwa na kadhia hii ya ucheleweshaji wa fedha hizi ambazo zinategemea ziwaendeshe katika masomo yao. Kwa hiyo, mimi naiomba sana serikali bado iendelee hili kuliangalia kwa mtazamo mzuri ili wanafunzi kule wakiwa nje wasiweze kuteseka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna Chuo chetu Kikuu cha Taifa (SUZA). Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) hakipatiwi fedha kwa maendeleo kwa ajili ya miradi mbali mbali ya chuo ambayo inasuasua

kutokana na ukosefu wa fedha mfano wa miradi ya uimarishaji wa miundombinu ya majengo.

Mhe. Mwenyekiti, hiki ndio chuo ambacho tumekibebesha mzigo, kwa hiyo lazima nacho tukijengee mazingira ya upataji wa hizi fedha kwa sababu hapa wakati tunapitisha sheria hapa sisi wengine tulisema hivi jamani vyuo hivi mbona bado mapema. Si kama tulikuwa tunaona labda ile dhamira ya serikali sio nzuri, tulikuwa tunaiona kama dhamira ni nzuri na imekusudia kuleta mambo mazuri. Lakini tulikuwa tunaona bado sisi mbavu zetu changa kidogo ilikuwa tujisogeze sogeze na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametupa kijana mzuri katika ukusanyaji wa mapato Waziri wetu wa Fedha na Mipango tunampongeza sana na yeye kwa juhudi zake ambazo anajitahidi katika kukusanya hivi, lakini mahitaji yetu ni mengi kwa wakati mmoja.

Kwa hiyo, inawezekana ukaziona hizo fedha zinajitahidi kukusanywa lakini utakuta hazijakidhi haja kwa sababu yale matatizo ni mengi. Kwa hiyo, ndio maana tulikuwa tukigoma goma sana hapa wawakilishi kwamba kuvichanganya hivi vyuo kwa wakati huu ilikuwa bado ni mapema, lakini kwa kuwa sasa imeshafanyika basi bado tunaiomba serikali juhudi za makusudi zifanyike ili chuo hiki kiweze kusimama kwa dhamira ile ambayo imekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika suala zima la ugatuzi. Mhe. Mwenyekiti, suala la ugatuzi kuna mafanikio yake lakini kuna na changamoto zake. Kuna changamoto hapa zimeoneshwa katika suala hili la ugatuzi wa elimu. Wamesema kuna kukosekana miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za elimu zilizogatuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili bado ni geni kwetu kwa hiyo elimu inahitajika sana sana kule chini. Kwa hiyo, bado tuwasaidie wenzetu katika suala hili, kwanza lina changamoto nyingi kwa sababu kwanza kule tumepeleka wafanyakazi ambao walikuwa hawapo, majengo kule hayapo ya kutosha. Kwa hiyo, bado huku kunahitajika sana elimu iweze kusaidia katika sehemu hii, wenzetu bado hawajalifahamu kwa haraka tuwasaidie mpaka pale watakapoweza kusimama wenyewe kwa miguu yao basi tutaweza kuwaachia. Hili ni suala zuri na ni muhimu sana

litaweza kupunguza mzigo mkubwa katika serikali kuu lakini bado elimu kubwa inahitajika ili suala hili liweze kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema mengi lakini si busara kama napo Wizara ya Afya sijaigusa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya wenzangu wamesema mengi na nawapongeza yale waliyoyasema tunaiomba serikali iyafanyie kazi kwa sababu hii ni wizara ambayo sisi ndio tunategemea maisha yetu wanatusaidia wao, na niwapongeze sana madaktari wetu ambao wanatuhudumia kila wakati.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna wenzangu hapa wamesema kamati imeonesha changamoto…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu eeh.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Haya ahsante mheshimiwa namalizia.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wameonesha changamoto hizi za afya hasa kule Pemba ambapo walipotembelea kile kituo cha Kojani. Mhe. Mwenyekiti, niiombe sana jamii ya wenzetu kule Kojani ambao wao wamefanikiwa kupata daktari ambaye anaishi ndani ya kijiji chao anatoa huduma. Niwaombe sana sisi wenzao huku tuna nyumba za madaktari na hatuna daktari tunalilia wizara kila siku hapa, nyumba ipo ya daktari imeshajengwa lakini hamna daktari ambaye anaishi katika kijiji, wao wamepata neema hii tunaomba neema hii waiyengeyenge na wasimbughudhi yule mfanyakazi ambaye yupo pale kwa ajili ya kuwasaidia wao. Tunawaomba sana wenzetu waweze kuona hiyo ni neema kwao imetokea kwa hiyo lazima wamuenzi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameeleza mengi katika changamoto hizi za afya na mimi naungana na wenzangu, ni kweli katika afya tunaomba sana hii ni kazi ya uadilifu mkubwa kabisa, kazi hii unapoifanya kiuadilifu una thawabu nyingi sana. Kwa hiyo, tunawaomba wenzetu waweze kutoa huduma hizi kwa njia sahihi ili waweze kutuhudumia, waweze kuisaidia serikali kwa sababu wanapotoa huduma wao maana yake wanaisaidia serikali yao iweze kufanya vizuri. Kwa hiyo Mhe.

Mwenyekiti, mimi naungana na wenzangu katika kuunga mkono ripoti hii ya Kamati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya kwa asilimia mia moja na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atupe nguvu na uwezo tuweze kuyatekeleza majukumu yetu yale ya kila siku ili kuwafikishia wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako, nilimwita Naibu Waziri wa Afya lakini kabla ya Naibu Waziri wa Afya Mhe. Jaku Hashim Ayoub umeniomba dakika tano uzitumie dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru unachopewa hicho hicho kidogo binadamu hutakiwa ashukuru, pokea hidaya.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni katika wizara moja nyeti sote humu ndani tunahitaji afya, bila ya afya humu ndani tusingekuwepo sisi. Kila kiumbe hai kinahitaji afya na nichukue fursa hii niendelee kusema siku zote hata saa tisa ya usiku mpaka saa kumi usingizi unakuwa mkali, maana yake unakuwa ni usingizi mzito. Hata nikaja kuamshwa Mhe. Jaku au Jaku Mhe. Rais kafanya mambo gani la mwanzo nitasema sekta ya afya, bila ya kuchechefya macho saa tisa ya usiku ndio usingizi unakuwa kidogo mzito. Nikiulizwa Mhe. Jaku unayajua mambo anayoyafanya Mhe. Rais la mwanzo nitasema sekta ya afya bila ya kuchechefya macho au kufikicha macho, nimpongeze kwa dhati kabisa na sisi sote ni mashahidi hakuanza juzi wala jana tokea kuingia *field* hii amefanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo la kusikitisha huko juu watendaji wa Wizara ya Afya hakuna baada ya mmoja labda Dkt. Buruhani wa Bodi ya Vyakula, tutafanya kazi vipi, nathubutu kusema hivyo nimekwenda nikachungulia mimi, tulikuwa tushazoea watendaji hawapo baada ya Dkt. Burhan tu mimi ninafikiri tutafanya kazi vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub yupo na Mkurugenzi wa Utumishi wa Afya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Basi kama wawili watatu hawazidi na huyo mmoja ni Bodi ya Chakula, Wizara ya Afya ya Mnazi Mmoja ndio kwenye uhai wa watu itakuwa tunafanya kazi yote bure humu ndani, tutawaonea siku zote hawa ndio yale ninayosema ng'ombe wa mbele hataki kwenda unampiga ng'ombe wa nyuma. Kitu cha kusikitisha lakini tuachie huko mheshimiwa mimi nitagusa mambo matatu. Nitagusa kuhusu lifti, nitagusa *Ct. Scan*, nitagusa banda la wagonjwa Mnazi Mmoja ambavyo vitu hivyo muhimu kwa binadamu, na hiyo moja ikawa ni ahadi na *hansard* hii hapa ya banda la Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, lifti ni kitu muhimu sana nafikiri tokea enzi sijui kama alikuwa waziri au Waziri wa Fedha Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini lifti alivyoifanyia marekebisho, lakini mpaka sasa hivi hali ya lifti hairidhishi. Mgonjwa anaweza kupandishwa juu mle kwa mitihani mikubwa, ngazi yenyewe nyembamba, hairidhishi mtu pengine keshatiwa gesi, keshaharibika kichwa hujui namna gani ya kumpeleka juu. Kwa hiyo, serikali niiombe sana tena sana iangalie lifti ni kitu muhimu katika uhai wa hospitali ya Mnazi Mmoja inayotegemewa ya rufaa. Lifti ghali ina umuhimu wake mgonjwa huwezi kumpandisha na ikiwa mtu mzito kabisa ni mtihani, utambebaje ngazi ile, lifti ni kiungo muhimu katika hospitali ile. Kwa hiyo, niiombe serikali sana Dkt. Khalid hapa nikuombe sana kama pana hali ya pesa uwasaidie na lifti ni milioni mia moja na ishirini au milioni mia moja na hamsini unapata lifti mpya. Kwa hiyo, serikali niiombe sana tena sana lifti ile iangaliwe hili ni ombi langu wagonjwa wanapata shida, uhai wa ile hospitali ni lifti. Leo mgonjwa katiwa gesi anapandishwa juu maana yake hata hayasemeki, kwa hiyo hospitali serikali iangalie kufanya haraka huduma ya lifti.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili nije kwenye *Ct. Scan* imeharibika karibu mwezi mmoja na kidogo kama sikosei. Hapa Mhe. Rais kafanya kazi kubwa sana, kipimo kile hospitali nyengine hakipungui shilingi laki mbili au mbili na nusu. *Ct. Scan* ile inatoa vipimo ishirini mpaka thalathini nafikiri kwa siku tufanye shilingi ngapi hesabu hiyo kwa mwezi shilingi ngapi, kwa mwaka shilingi ngapi? Bure bure kwa hiyo Mhe. Rais kafanya kazi kubwa sana kwenye sekta ya afya, laki mbili na nusu kwa mnyonge si pesa kidogo. Kwa hiyo, nimpongeze kwa dhati

kabisa jitihada anazochukua Mhe. Rais na wizara vile vile kwa baadhi ya watendaji.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Waziri nafikiri hayupo hapa sijui katoka au kadharurika, kama kuna mtendaji wake katika hiyo *Ct. Scan* inavuja dari yake, hata *Ct. Scan* ikatengenea basi itakuwa mtihani kuna vitu pale vitaharibika, dari inavuja. Hiyo ni changamoto moja kubwa kwani *Ct. Scan* ni kipimo muhimu na pale daktari anatakiwa masaa ishirini na nne awepo sio kama hivi tunaweza tukafanya akachukuliwa kwa ambulance kwenda rudi. Pawe na utaratibu wa kuwepo daktari wa kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hili suala la banda, hili naomba ninukuu maneno haya ya tarehe 05/06/2017, nilizuia mshahara au nilipiga buti hapa na jawabu niliyoipata ni hii naomba kuinukuu.

> "Mhe. Waziri wa Afya, mheshimiwa maamuzi ya serikali hayaendi hivyo hata siku moja itolewe *document* tu litolewe banda, mheshimiwa baada ya miezi sita sisi tutawasilisha ripoti tumefikia wapi naamini itakuwa tumeshamaliza lakini haiwezi serikali itoe neno tu la banda kumpa Mhe. Jaku nilitaka kujitolea kulijenga hili".

Hapa nafikiri alikuwepo Mhe. Mgeni Hassan Juma akatoa, mheshimiwa ni mara ya tatu tumeshaongeza nafikiria tumefika pahali wao wanaahidi watalijenga ndani ya miezi sita. Hebu nisaidieni mwezi wa sita, wa saba, wa nane, wa tisa, wa kumi, wa kumi na moja, wa kumi na mbili, moja, mbili miezi tisa karibu unaingia mwaka tunakwenda kwenye bajeti. Nilisema pale hapapikwi pilau wala biriani wala hapatolewi sadaka, wananchi wanaumia wanapeleka wagonjwa na wao mwisho wanakuwa wagonjwa kwa kusota kwenye sakafu ni ahadi ya serikali hii, *hansard* hii hapa. Kwa hiyo, bado hatujui kinachoendelea hii hapa *hansard* ni maneno ya Mhe. Waziri haya.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kipindi kilichopita hapa cha uwakilishi uliopita nilisokotana na Mhe. Juma Duni Haji kuhusu *ICU* na alifika hata kujiuzulu humu ndani alitoa miezi sita tu na imejengwa. Lakini ahadi zetu au maneno mengine nasema siku zote Mhe. Mwenyekiti tuweke akiba tusiyamalize yote ukiyamaliza yote utakuwa huna akiba

tena. Haielekei kama kitu nilichokifanya kazi kubwa pale kutoa kibali na Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban nimshukuru kwa dhati Waziri wa Ardhi kahangaika wenyewe hospitali kimewashinda kupata sehemu ile, Mwenyezi Mungu ni wa kwanza na wa pili ni mimi mpaka ikatoka pale ikapatikana sehemu. Leo jitihada yote hakuna kinachoendelea na *hansard* ziko huko, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban nimshukuru sana tena sana akatoa eneo lile wenyewe wizara imeshindwa kulitafuta hilo eneo. Kwenye kamati hiki sijui ni ahadi gani miezi sita, huu mwezi wa tisa unaendazake ahadi hii hapa. Kiongozi anatakiwa awe kioo.

Jengine kuhusu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa dakika zako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Katika kitabu humu ukurasa wa 10 kamati ilipofanya ziara katika Hospitali ya Wete ilipata taarifa kuwa kuna nyumba ndani ya eneo la hospitali ambayo inamilikiwa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Awali nyumba hiyo ilikuwa ikitumika kwa matumizi ya hospitali hiyo baadae uongozi wa hospitali uliarifiwa na hii nimeshuhudia. Nyumba ile nimeiona naijua na si hiyo tu hata Chake Chake ipo, hizi nyumba tunazungumza na serikali zirejeshwe wapewe wenyewe hospitali. Tokea wakati huo wanatumia hospitali leo wanakuja wenye mamlaka ya nyumba wanasema nyuma zao, hii serikali inafanya kazi kwa pamoja sasa daktari akipelekwa uhamisho pale atakwenda kukaa wapi? Msikitini au kanisani. Nyumba zirejeshwe, Dkt. Karume hayupo hapa lakini ingebidi limkute nyumba warejeshewe Wizara ya Afya hii ni changamoto kubwa, nimeiona Wete nimeona Chake Chake.

Chake Chake kuna moja wamechukua Wizara ya Elimu na moja sijui kama Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Wilaya yeye keshahamishwa pale hayupo, kwa hivyo nyumba zile zirejeshwe katika Wizara ya Afya. Niiombe sana serikali hii inafanya kazi kwa pamoja kwa hivyo, serikali ni wananchi na wananchi ni serikali, vyenginevyo tunawabebesha mzigo Wizara ya Afya. Nyumba za Chake Chake, nyumba za Wete warejeshewe Wizara ya Afya ili madaktari wakifika pale wapate kukaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo na mimi nikushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Jaku Hashim kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Naibu Waziri wa Afya atafuatiwa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini naomba niwakumbushe mtumie muda mchache sana ili tupate tumpe nafasi Mwenyekiti wa Kamati.

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mheshimiwa mapendekezo ya Hospitali ya Abdalla Mzee kuhusu usafi waajiriwe vijana kama tunavyoona barabarani wakisafisha wawepo japo wiki mara moja. Kuhusu kugatuliwa bado kuna manunguniko ya walimu hususan watu hatuna na maandalizi na pesa za mshahara.

Kuhusu suala la maabara skuli zangu zote hazina ukiacha ya Chwaka, Tumbe shida ya walimu ni kero za skuli.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Nawapongeza mawaziri wote wa Wizara ya Afya na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Manaibu Mawaziri wao. Pongezi pia ziwaendee mwenyekiti pamoja na wajumbe wote wa kamati kwa kazi nzuri walioifanya hadi kuwasilisha taarifa hii. Naipongeza serikali kwa kuongeza wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya cha Fuoni ambacho kimewarahisishia sana mama zetu ambao ni wajawazito kuweza kupata huduma kwa urahisi na ufanisi. Naunga mkono kwa hospitali ya jeshi Bububu na KMKM Kibweni kuweza kupata mgao wa dawa kutoka *Central Medical Store*.

Aidha, suala la ugatuzi litolewe elimu zaidi ili wananchi wetu waelewe dhana na dhamira ya ugatuzi. Pia Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ninashauri serikali iwapatie wafanyakazi wakutosha ili waweze kumudu baadhi ya majukumu. Pia wapatiwe ufanisi wa bajeti ya kutosha ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi vizuri. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe pamoja na Naibu Spika, na Spika, kwa uongozi wenu mzuri ambao mnaliendesha Baraza hili na tukawa tuna utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda nichukue nafasi hii adhimu kwanza kuchangia kwa kuipongeza kamati kwa ripoti yake hii ambayo imewasilishwa ya Ustawi wa Jamii. Nampongeza sana Mwenyekiti pamoja na wajumbe wake wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyonayo na waliyotuonesha Wizara ya Afya. Kwa kweli sasa hivi tuna wasiwasi, kwa sababu tunajua kwamba kamati zinachaguliwa nyengine kuwakosa wajumbe wale wa kamati kwa kweli kwetu ni tatizo, lakini kwa sababu imeshabidi basi Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atatupangia wajumbe wengine ambao wana kheri zaidi na sisi.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ya kamati imekamilika kwa kueleza na kubainisha kila changamoto zinazoikabili wizara pamoja na wafanyakazi wake, pamoja na mazingira yanayohusu huduma za afya kwa ujumla. Wizara yetu inapongeza sana juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein katika kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanaendelea kuwa na salama huku wakiendelea kupata huduma muhimu za kijamii zilizo bora, ikiwemo huduma ya afya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya tunajua kwamba sisi ni dhamana kubwa ya afya za wananchi na binadamu wote kwa ujumla. Hivyo, tunalihakikishia Baraza lako tukufu kwamba, tutaendelea kushirikiana na kufanya kila itakavyowezekana kuanzia wafanyakazi, wataalamu hadi viongozi kwa kuleta ufanisi zaidi na kupunguza changamoto zinazoikabili sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kupitia ripoti hii basi niwapongeze wafanyakazi wote wa sekta ya afya Unguja na Pemba wakiwemo wataalamu wetu mbali mbali kwa juhudi zao za kufanya kazi na kuokoa

maisha ya wananchi, yaani wagonjwa wanaofika vituo vya afya na hospitali zetu kila siku.

Mheshimiwa siku moja tu wafanyakazi hao wakisema leo tunapumzika basi maisha ya Wazanziabari yatakuwa yako hatarini. Tuna kila haki ya kuwapongeza na kwa wale wafanyakazi wachache ambao hawana maadili mema ya kazi kwa njia moja au nyengine wizara inakamilisha uchunguzi juu yao na ikithibitika adhabu kali dhidi yao itatolewa, ikiwemo adhabu ya kuwanyang'anya leseni, kwani watakuwa hawana haki ya kuendelea kutoa huduma kwa wananchi huduma ambazo ni mbovu na huduma ambazo ni za usumbufu na ukatili kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, wizara pamoja na serikali tutakuwa tuko tayari kusamehe huduma zao na tutaajiri wafanyakazi wengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimalizie mchango wangu kwa kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kwa mashirikiano yao makubwa kwa Wizara yetu ya Afya kwa ushauri wao, na kwa kutuelekeza yale ambayo yanaonekana kwamba yana manufaa makubwa kwa wizara yetu. Tunawashukuru sana na yote ambayo wanayasema, wanayaeleza sisi tunayapokea kwamba anayekulaumu anakupenda na kupitia lawama zao, na kupitia maelekezo yao, ndio sisi tunaondoka hapa na ari ya kwenda kufanya kazi na kuleta ufanisi kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba niendelee kuipongeza ripoti hii na kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mwenyekiti na mimi kunipa fursa hii kueleza machache juu ya ripoti ya kamati. Kwanza na mimi naipongeza kamati hii kwa kazi kubwa iliyofanya na kwa kweli kwa asilimia kubwa sana maelekezo yanayotokana na ripoti hii tutayafanyia kazi kwa asilimia kubwa. Mengine na sisi itabidi tufanye utafiti zaidi ilikutoa maamuzi ambayo tutakuja kueleza hapo baadae.

Nagusia kuhusu baadhi ya mambo tu machache kwa ajili ya kuweka sawa. Kuna suala la hoja ya matokeo, kulikuwa na kauli kwamba matokeo hayaridhishi. Kwa kweli kwetu sisi Wizara ya Elimu tunaona

kwamba matokeo yaliyotokea ya viwango mbali mbali darasa la nne, la sita, la kumi na la kumi na mbili yanaridhisha na ushahidi wake tutakuja kutoa hapo baadae tutakapoleta ripoti kamili. Lakini kwa ufupi tu niseme darasa la nne wanafunzi wamefikia asilimia zaidi ya 90, darasa la sita asilimia 97, darasa la kumi asilimia 70 na zaidi na kidato cha nne asilimia 70.8.

Kuhusu suala la miundombinu ya madarasa tunakubali kwamba madarasa yetu ni machache na juhudi ya wizara tunaiona, inajenga skuli za ghorofa lakini pia tunakamilisha madarasa 200 katika wakati huu. Kazi hiyo inaendelea na imefanyika vizuri sana kwa sababu tunaifuatilia kwa karibu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la kurejesha wanasema Vyuo vya Ualimu. Tuseme kwamba Vyuo vya Ualimu vipo kuna Chuo cha Kiislamu kwa sasa tunacho, lakini pia tuna sehemu nyengine ambayo inatoa mafunzo ya ualimu Vyuo Vikuu. Pia vinatoa mafunzo ya ualimu. Kwetu sisi katika Wizara ya Elimu tunapozungumzia kuhusu vyuo vya walimu ni chuo ambacho kinatoa mafunzo ya ualimu katika sehemu mbili, sehemu ya masomo yenyewe ambayo mwalimu atakuja kusomesha baadae na masuala ya mbinu, falsafa na *Phychology***.** Sasa kama huo ndio ualimu basi vyuo hivyo vinaendelea kutoa.

Kuhusu suala la wenzetu imetolewa mfano Chang'ombe na kadhalika. Chang'ombe wako katika mfumo kama wetu sisi, kule pia sasa hivi imekuwa *university* ambayo inatoa masomo yale yale ya ualimu kama tunavyofanya sisi. Nadhani tuko katika njia sahihi lakini tumesema nalo pia tutalifanyia utafiti zaidi ili kuja kutoa maelezo sahihi hapo baadae.

Kuhusu suala la mapitio ya sera. Hili kwa kweli ni kazi ambayo tunaifanya na tumeshakutana na baadhi ya wadau na tutaendelea ili baadae kuja kutoa mawazo ambayo ni sahihi kwa wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mawazo yaliyomo ndani ya sera yalikuwa sahihi kwa wakati wake na Baraza la Wawakilishi hili likapitisha, lakini kuwa sahihi wakati ule haina maana ni sahihi mpaka leo na ndio maana tunalifanyia mapitio tutakuja kuona hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala tunakubali ukosefu wa vifaa vya maabara vifaa ni vichache lakini wizara inajitahidi na jana nilisema kwamba katika mwaka ujao wa fedha Wizara ya Elimu itaongeza fedha katika fungu hili la vifaa vya maabara.

Kuna suala la malimbikizo ya madeni ya walimu kama ni sehemu moja ya haki yao lakini pia ni motisha. Hili tumesema kwamba, Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na taasisi nyengine za serikali wizara inayohusika na Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha suala hili litafanyiwa kazi na *Inshaallah* walimu waendelee kuvuta subira na litatatuka.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri naomba nikukumbushe tena leo sio siku ya majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu: Sijibu nagusia mambo madogo madogo. Mwisho kabisa nataka kuzungumzia suala la Mfumo wa Elimu. Mheshimiwa mmoja alisema kwamba wanafunzi wanaomaliza darasa la sita wako nje, la saba wako nje, nataka kuweka sawa tu, kwamba sasa hivi mfumo wa sasa wanafunzi watakwenda mpaka darasa la 12. Hata mwaka huu hakuna aliyepelekwa nje darasa la sita, wameendelea waliokuwa alama zao chini kidogo watarejea masomo yao na darasa la kumi hivyo hivyo hakuna mwanafunzi ambaye amewekwa nje kwa darasa la sita.

Mwisho kabisa kama mwakilishi napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana madaktari wote na wauguzi katika hospitali zetu Unguja na Pemba. Waheshimiwa Wawakilishi watu hawa kwa kweli wanafanya kazi kubwa na kwa maana hiyo haifai hata kidogo kuwabeza, haifai. Hebu tujiulize maisha ya watu wangapi yameokolewa kwa madaktari hawa, madaktari ni watu kama sisi na kama wako kama sisi kwa hivyo wana mapungufu yao lakini wana uzuri wao. Hebu tuutizame huu uzuri wao na madaktari na wauguzi pia wana fani zao, *profession* zao, hebu tuziheshimu hizi *profession* zao; pale wanapokosea *profession* zao zitawahukumu, si vizuri hata kidogo kuwahukumu na kuwasema na kuwalani hili si jambo zuri kwa kweli. Hawa vijana wanafanya kazi tuwaheshimu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia machache katika Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema kuweza kuwa hapa leo hii na kuendelea na kikao chetu cha Baraza la Wawakilishi. Lakini pili nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunaishukuru sana, sana, kamati kwa michango yao mikubwa ambayo tunaipata kutoka kwao. Tokea tumeanza kufanya kazi na kamati hii mengi yamejitokeza lakini mengi vile vile tumeweza kuyatatua na kuyajua kutokana na ufuatiliaji wa kamati. Kwa hivyo, tunaishukuru sana kamati na tunaiomba kamati izidi kushirikiana na sisi ili kuona kwamba maendeleo ya elimu yanazidi kuimarika siku hadi siku ndani ya nchi yetu.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi kwa michango yao mbali mbali ambayo wameitoa kwa Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Tuseme na tukiri kwamba michango yote tumeipokea na *Inshaallah* ikifika muda wa kutoa majibu mwezi wa tisa tutatoa majibu ya maswali yote ambayo yametolewa ndani ya kamati. Lakini ningependa kusema machache tu Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako dakika mbili.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitangaza elimu bure kwa skuli ya maandalizi na msingi, na hii ni kwamba ina maana hakuna mchangio wowote ambao mzazi anatakiwa kuchangia kwa upande wa skuli ya maandalizi na msingi. Kwa hivyo, kwa suala hili ningependa sana Waheshimiwa Wawakilishi hasa wa majimbo tulifahamu kwamba hakuna mchango wowote na kama kuna skuli ambayo inachangisha basi tunaomba sana tupeane taarifa na tusisubiri mpaka tuje katika kikao ndio tunapeana taarifa hizi. Kwa sababu binadamu ndio sisi tunaunda sheria lakini ambao wanavunja sheria vile vile ni hao hao binadamu. Kwa hiyo, kama kuna skuli ambayo inavunja sheria hizi na inakwenda kinyume na agizo la Mhe. Rais wetu mtukufu wa Zanzibar basi naomba sana tuambizane ili tuweze kuchukua hatua kwa skuli husika.

Hii inajitokeza sana katika suala zima la uandikishaji wa wanafunzi kuna baadhi ya walimu wanawaambia wazazi wachangie pesa, si sheria, si haki wala haitakiwi. Kwa hivyo, kwa hili tunaomba sana waheshimiwa tushirikiane ili kuona kwamba tunatokomeza suala hili.

Suala jengine Mhe. Machano Othman Said aliomba skuli ya Donge pamoja na Mhe. Panya Ali Abdalla umalizaji wa skuli ya Donge ya ghorofa. Nipende tu kulitaarifu Baraza lako tukufu ni kwamba mwaka 2017 tulitiliana saini mkataba na Shirika la *Kinder Hans Foundation* na tayari ujenzi wa skuli ya Donge umeanza rasmi mwezi huu wa Febuari mwaka huu 2018. Ujenzi umeanza na kwa wale waheshimiwa ambao labda hawajapita njia ya Donge ningeomba sana wapite, kwa sababu hili eneo la skuli tayari limezungushiwa uzio kwa kuanza matengenezo na tayari yameshaanza. Kwa hivyo, kwa muda wa miezi 12 skuli hii itakuwa katika majenzi na itamaliza kujengwa vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa ni kwamba sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunakuwa tunapokea majengo kutoka kwa wananchi, tunapoyapokea ndipo tunayamaliza majengo haya. Kwa jengo la skuli ya Chimba bado Halmashauri ya Chimba haijatukabidhi lile jengo, kwa hivyo kama hatujakabidhiwa tunakuwa hatuna mkono wa kuweza kutia, lakini watakapotukabidhi kama kuna tatizo la vyoo au matatizo mengine yoyote ambayo yapo hapo Wizara ya Elimu itamaliza ujenzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache tumepokea taarifa tutaleta majibu rasmi ya serikali mwezi wa Septemba, 2018 *inshaallah*. Lakini tunashukuru sana na mimi kwa upande wangu naomba kuunga mkono ripoti ya kamati. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu kwa muda mchache uliotumia lakini namuomba na Waziri wa Afya aige nyayo zako. Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuiga nyayo za Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii

lakini la pili nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuipongeza Kamati ya Ustawi wa Jamii ambayo inasimamia wizara mbili muhimu zinazogusa jamii nzima ya wananchi wa Zanzibar, yaani elimu na mafunzo ya amali pamoja na afya za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nitajikita zaidi kueleza *experience* yangu niliyopata na hii kamati na nitaeleza mafanikio makubwa ya kamati hii. Kwa hivyo, nawapongeza sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake wote wa kamati hii na wewe mwenyewe ukiwemo uliyekaa hapo juu ambaye ni mjumbe wa kamati hii pamoja na watendaji wa Baraza la Wawakilishi. Nasikitika sana kamati hii itakuwa inavunjwa kuundwa kamati nyengine, ningeomba sana kama kamati hii itaendelea basi naweza kusema wameshakuwa wazoefu wao wa kubobea katika sekta ya elimu na sekta ya afya na nitaeleza sababu zangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshawahi kuwa mjumbe wa kamati mbali mbali pamoja na Kamati ya *PAC*. *PAC* ni kamati ambayo inakuwa hata katika Kanuni za Baraza inapewa muda zaidi, hata katika Kanuni za Baraza inapewa bajeti zaidi kwa sababu inapitia wizara zote za serikali. Hiyo ndio Kamati ya *PAC* na mimi nilibahatika wakati huo kupata mafunzo ya ndani ya nchi na nje ya nchi Kamati ya *PAC* inatakiwa kufanya kazi vipi pamoja na *Auditor General*.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka kuizungumzia Kamati hii ya Ustawi wa Jamii. Kwa kweli kamati hii chini ya uongozi wa Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini imeweza kufanya mambo matatu muhimu sana.

Jambo la kwanza baada ya kumaliza kazi zake tu ilikuwa inasisitiza kukaa na sisi mawaziri pamoja na Manaibu Waziri na watendaji wetu wakuu ili kuyapitia yale yote waliyoyaona na kuomba pale pale ufafanuzi. Kwa sababu wao hawakuwa wanasubiri mpaka wafike Barazani ili kuomba ufafanuzi kwa sababu wizara zetu ukisubiri mpaka Baraza watu 20, 30 inawezekana wameshatoka roho. Wao walikuwa wanakuja kila baada ya kupitia kufanya kazi zao na kupata yale yote na hasa yale maeneo muhimu ambayo yanagusa roho za wananchi wa Zanzibar, maisha ya Wananchi wa Zanzibar walikuwa wanakuja wanakaa na sisi. Kwa hivyo, hilo ni jambo moja zuri sana na ninaomba

iwe mfano kwa kamati nyengine zote zitakazokuja lakini pia iwe mfano kina Dkt. Mwinyihaji Makame kama wataondoka basi wawaachie hao wanaokuja wigo huu uendelee tuendelee kuufuata.

La pili Mheshimiwa, katika kamati hii nimejifunza mimi wako *very fair*, jambo la ukweli watakwambia hawakwambii jambo la kukusingizia hata siku moja, jambo kukiwa na kasoro wanakwambia ukweli kasoro yako pale pale, hata kama kuna usanii wanakwambia hapa kuna usanii, kama umedanganywa waziri watakwambia hapa Mhe. Waziri umedanganywa na kweli wakati mwengine kwa sababu hizi wizara zetu kubwa. Wizara ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ina takribani wafanyakazi elfu kumi na tano *almost* unakwenda kwenye *data base* ile ya serikali nzima unapita moja yaani robo moja unaipita unaelekea kwenye nusu.

Wizara yetu sisi wafanyakazi zaid ia elfu tano, sasa ukichanganya wizara hizi mbili na hii kamati moja kwa kweli kazi hiyo wanafanya ilikuwa *very fair* wanatwambia ukweli hawasubiri. Mheshimiwa umekuwa mtindo wa Baraza Waheshimiwa wengine naomba niwaseme ukweli. Imekuwa mtindo wa Baraza mtu anapata kitu anakificha anasubiri wakati wa Bajeti aje nacho hapa.

Sasa mimi nahisi unakuwa hujamtendea haki yule mwananchi aliekuchagua, hujamtendea haki yule unayemtumikia, hujatendea haki kupeleka zile huduma kule kunakotakiwa. Wewe fika nalo mapema eleza kwenye Baraza eleza kama kawaida kwa sababu unatafuta sifa kwa wale wananchi wanaokupa kura, ni wajibu wako upate zile sifa wananchi waone sifa zile wewe unastahiki umekwenda kuwatetea pale wakuchague tena.

Lakini lile jambo lieleze mapema ili yule mwananchi apate kupata ile huduma. Waheshimiwa wengine wanakaa nali jambo kwa muda mrefu sana. Sasa mimi nashukuru sana kamati hii imekuwa haikai kwa muda mrefu kila panapotokezea jambo Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini na Wajumbe wake wa kamati wote wamekuwa mstari wa mbele.

Lakini la mwisho kabisa mimi niipongeze ripoti hii ilivyaondikwa, nimekaa na watendaji wangu wako pale juu ingawa Waheshimiwa

wengine wamesema hawaonekani naomba hizi kamera ziwachukuwe wako pale juu, kusali ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, tupo na kama hatupo serikali ndio hii nzima kuanzia kule kwa Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman mpaka kwa Mhe. Said Soud Said ndio serikali hii na sisi serikali tutafanya kazi kwa umoja wetu kwa mashirikiano na kwa upendo na ndio maana juzi Mhe. Mohammed Aboud Mohammed pale akazimama Waziri wa Nchi Afisi wa Makamu wa Pili wa Rais akatoa tamko rasmi la serikali. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa naomba mimi niseme kwamba hii *document* ilivyoandikwa kwa kweli mmeandika vizuri na nikilinganisha na kamati nyengine yoyote. Kwa kweli *document* hii naweza kusema inaongoza kuliko *document* nyengine yoyote na watendaji wetu wataweza kuifanyia kazi vizuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakuja kutoa majibu mwezi wa Septemba.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa utaratibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Kubwa zaidi jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Namalizia moja ambalo ningepneda kusema kabisa hapa wazi serikali haiongozwi na Mwakilishi mmoja wala Wawakilishi wawili wala wawakilishi watatu. Serikali ina mipango yake ambayo inapanga na ile mipango inaweza kubadilika wakati wowote hata kukiwa na *hansard* ya miaka ishirini iliyopita serikali inaweza kubadilisha mipango yake na muelekeo wake na ikatoa sababu, serikali haiendeshwi na akili ya mtu mmoja hilo.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kuhusu utaratibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kaeleza vizuri pale kwamba katika *policy* ya nchi hii inaweza kubadilishwa wakati wowote. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii na nikitakiwa kutoa ufafanuzi mwengine basi niko tayari kutoa ufafanuzi huo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nimemuona Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Simai Mohamed Said kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kuhusu utaratibu kanuni ya 63 na nasimamia hoja ya (59).

Mhe. Mwenyekiti: Enh kanuni gani imevunjwa?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kila Mjumbe lile jambo ambalo liko katika mjadala na hatarudia rudia maneno yake. Ninakuja katika hoja ya tatu. Mjumbe yoyote atakapokuwa akisema kaa Barazani atawajibika kuwa sababu ya msingi kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. Spika, Mjumbe mwengine yoyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi huu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hatukuja kujitia adabu wala kuoneshana misuli, wala mwamba hii nyumba yetu wote sisi ni moja. Lengo wanotumia Waheshimiwa Mawaziri kutaka kutugombanisha na wananchi wetu, vyenginevyo sivyo mmetupa muongozo basi tuusimamie. Hapa hatukuja kutafuta umaarufu wala hatukuja kutafuta uwaziri wala unaibu waziri *hansard* hizi na Mhe. Waziri nimwambie hili jambo kalikuta toka yuko Mhe. Juma Duni suala hili na mimi niliyehangaika na Mwenyezi Mungu anajua na *hansard* zipo. Sasa kama serikali anasema haiendeshwi na mtu mmoja na Mwakilishi mmoja hivyo sivyo afute kauli yake. (*Makofi*)

Yeye kama kachaguliwa na sie tumechaguliwa na haya mambo yanageuka upepo unakwenda huku wengine wanakwenda huku na sivyo kazi ya Muakilishi ni kuisimamia serikali na kuihoji. Sasa anavyotaka yeye kutupelekesha hatuwezi kwenda afute kauli yake. *Hansard* zipo sie maneno yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekufahamu...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Basi afute kauli yake Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu nimekuruhusu umeusoma na watu wameusikia. Lakini nilichomfahamu waziri wewe umezungumzia kuhusu *hansard* ambazo ziko na za zamani ziko. Lakini alichokisema serikali zina taratibu zake ikiwezekana katika taratibu hizo *hansard* hizo zipo lakini pengine anaweza akajipanga na pengine hiyo *hansard* iliyokuwepo ikapingwa na maelezo au na jawabu ya serikali ikawa bora kuliko ile iliyokuwepo.

Mheshimiwa nakushukuru naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said huogopi ila umeridhika. Nashukuru sana. Naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa fursa hii alaasiri ya leo kufanya majumuisho kwa ufupi sana wa hoja yetu ya Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia hapa ukumbuni na wale ambao walichangia kimaandishi na wengine ambao kwa bahati wakati kuwa mchache hawakupata fursa. Lakini wote naamini kabisa wanataka huduma za afya nchini mwetu ziimarike. Lakini pia tufate ile *theme* ya Wizara ya Elimu inayosema "Elimu Bora kwanza" huo ndio msimamo. Kwa hivyo, haya mambo tu-*balance* tupate afya nzuri, tusome vizuri, tuendeshe nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, waliopata fursa ya kuchangia jumla ni 29. 22 walipata wasaa wa kuchangia hapa ukumbuni na 7 walichangia kimaandishi. Naomba sasa nitambue wale waliochangia ukumbini kama ifuatavyo:

1. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Ali Khamis Bakar
4. Mhe. Simai Mohamed Said
5. Mhe. Mussa Foum Mussa
6. Mhe. Machano Othman Said
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
9. Mhe. Asha Abdalla Mussa
10. Mhe. Suleiman Sarahan Said
11. Mhe. Nadir - Abdul-Latif Yussuf
12. Mhe. Khadija Omar Kibano
13. Mhe. Dkt Makame Ali Ussi
14. Mhe. Said Omar Said
15. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
16. Mhe. Miraji Khamis Mussa
17. Mhe. Panya Ali Abdalla
18. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
19. Mhe. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
20. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
21. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
22. Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi.

Waliopata nafasi kuchangia kimaandishi ni kama hawa wafuatao.

1. Mhe. Yussuf Hassan Idd
2. Mhe. Zaina Abdalla Salum
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
5. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
6. Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Malum (Juma Ali Khatib)
7. Mhe. Saada Ramadhani Mwenda.

Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru wote kwa michango mizito yenye hamasa na yenye kutaka maendeleo. Haya yote tuliyozungumza tuliyabaini wenyewe *physically field* haya si ya kukaa ofisini tukayaandika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nataka kusema Wahseshimiwa mawaziri wametoa ahadi kama ulivyo utaratibu mwezi wa Septemba watatoa majawabu kwa ufasaha na wakati huo wakati sisi tunaendelea na awamu nyengine.

Mimi niseme moja tu, kuna hili jambo la matokeo ya mitihani hasa hii ya kidato cha nne na sita. *NECTA* wanatoa matokeo ya mitihani na wanapotoa wao vyombo vyote vya magazeti, redio, nchi nzima wanatoa. Sasa kama wale wanakosea basi wana- *distort* jamii yetu maana yake jamii inapata *message* kwamba Zanzibar hatufanyi vizuri hiyo ndio m*essage* inayotoka.

Sasa naiomba sana wizara kama wana wasiwasi na takwimu zile basi wakae chini waje na wao watakwimu wai-*convince* jamaa kwamba *NECTA* hawasemi ukweli, hilo naliomba sana. Kwa sababu habari inaenea sana, habari inakwenda, habari inatoka unaona magazeti yote vichwa vile nafasi kumi za chini zimechukuliwa na Skuli za Zanzibar. Kwa kweli haipendezi hakuna anaefurahi kuona vile. Sasa kama si kweli basi tunaomba wizara wakae chini wa-*compute* takwim halafu watwambie. Hiyo itawakuwa wanasafisha lile *black spot* lililoletwa na *NECTA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa nakushukuru kwa mara nyengine tena, nashukuru wizara zote mbili, nawashukuru mawaziri, naishukuru kamati yangu kwa kweli, tumejikongoja tumekwenda Kisiwa Panza, tumekwenda Kojani tumekwenda mpaka visiwa vyote na safari hii tuaendelea na upande mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba ahsanteni sana naunga mkono na mimi hoja hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dimani na naomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa niwahoji wanaokubaliana na

hoja hii wanyoshe mikono, wanaokataa, wanaukubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nachukuwa nafasi hii kuwashukuru nyote mliochangia hoja hiyo. Lakini pia namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ambaye ndie mtoa hoja.

Lakini nashukuru serikali kwa jumla na mawaziri wa wizara zote mbili wanaosimamiwa na Kamati ya Ustawi wa Jamii na mategemeo yetu kwamba ikifika mwezi 9 basi zile changamoto zote zilizoonekana za kiutendaji basi watakuja na majibu ili Waheshimiwa Wajumbe waridhike na yale yaliokuwemo katika ripoti zile. Nawashukuru sana naakhirisha kikoa hichi mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1.35 Usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/2/2018 saa 3.00 asubuhi)